Nipashe
Jumanne Desemba 6, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581151
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



Nipashe TESA
Jumanne Desemba 6, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Illivyofungua dunia kwa wasichana kurudi kwa kasi madarasani
Kukosa vyoo shuleni kulitafakarishe taifa baada ya miaka 61 ya Uhuru
Kilivyowatisha wadau wa elimu wataja chanzo ni ukosefu maadili, adhabu ndogo
ELIMU NA ABATO KASIKA
MIAKA 61 YA UHURU
Kiboko kiwepo au kiondolewe shuleni?
• Walimu waambiwa ni ruksa 'kutandika' ila kwa maelekezo

UKURASA 13









**Marafiki** wanne jela kwa mauaji ugomvi mpenzi katika kigodoro

UKURASA 3



# Mahakama Kuu: CAG Assad aliondolewa kinyume cha katiba

• **Kesi** mpya kufunguliwa Mahakama ya Rufani madai kumng'oa madarakani CAG mpya... *Endelea ukurasa 3*



Mwonekano wa tuta kuu la kuhifadhia maji na mahandaki ya kuyapitisha kwenye Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHP). **PICHA: MPIGAPICHA MAALUM**

## Samia afuta sherehe Uhuru, fedha kutumika kujenga mabweni

UKURASA 10



# Kumekucha mradi Bwawa la Nyerere

• **Maji** yaanza kujazwa umeme uzalishwe... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** MAYELE AIRUDISHA YANGA SOKONI UK.32 **KATUNI** UK.6



Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Mahimbo Mndolwa (wa pili kulia), akiongoza ibada ya mazishi ya Askofu mstaafu Boniphace Kwangu. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Kumekucha Bwawa la Nyerere

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

KUMEKUCHA! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na hatua iliyofikiwa kwenye Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHP).

Serikali imesema itaanza kuruhusu maji kujaa kwenye bwawa hilo kuanzia Desemba 15 mwaka huu yaani siku tisa zijazo, huku matarajio ya kujaa kwa kiwango kitakachowezesha kuzalisha umeme yakiwa ni Aprili mwaka huu.

Ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 77.15 na itakapofika tarehe ya kuanza kuruhusu maji, utafikia zaidi ya asilimia 80, huku kukamilika kwa mradi na kazi ya kufua umeme kukitarajiwa kuwa Juni 14, 2024. Mradi huo utakaogharimu zaidi ya Sh. trilioni 6.5 ukiwa na uwezo wa kufua megawati 2,115 za umeme.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi hadi sasa kwa wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari waliotembelea eneo la mradi kuona maendeleo yake, Mhaifrolojia David Munkyala alisema kazi hiyo inasimamiwa kwa karibu na umakini na makandarasi wazawa kwa kushirikiana na makandarasi Arab Contractor na Elsewedy Electric.

Alisema wataanza kujaza maji wiki ya pili ya mwezi huu kwa kuwa utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), umeonesha kutakuwa na mvua nyingi ambazo zitaendelea hadi Aprili mwakani, na kama lisipojazwa sasa itakuwa vigumu kwa mwaka unaofuata.

"Kwa kiasi kikubwa kazi inakwenda kwa kasi kubwa, tunajitahidi tuwezavyo ifanyike kwa haraka na kwa ubora mkubwa, tumeshakamilisha ukuta maalum wa kuzuia na kuwezesha bwawa kupata maji, sasa tunaziba pale tulikochepusha mto tunaurudisha kwenye njia yake halisi maji yaanze kujaa," alisema.

Kwa mujibu wa Munkyala, kuna kiwango cha maji kinatakiwa kujaa ndipo uzalishaji uanze ni urefu wa mita 163 na kiwango cha juu ni mita 184 kutoka usawa wa bahari huku ujazo wa bwawa ni mita bilioni 32.7, na kwamba kuna utaratibu wa kisasa wa kuzuia maji bila kuathiri kuta za mradi.

Alisema wakati wa kujaza maji hakutazuia shughuli nyingine za utumiaji maji kusimama kwa kuwa wananchi wanaoendesha shughuli zao na viumbe vinavyotegemea mto Rufiji baada ya eneo la mradi watendelea kupata maji kama kawaida.

Mkandarasi huyo alisema teknolojia ya ujenzi wa bwawa hilo ni ya kisasa na litaishi kwa zaidi ya miaka 100, uwezekano wa uchafu kujaa ndani na kuathiri uzalishaji ni mdogo kwa kuwa walifanya utafiti wa maji yanayoingia Mto Rufiji kutoka kwenye mikoa 10 na kubaini ni kidogo sana.

Aidha, alisema Watanzania wamepewa kipaumbele kwenye mradi kwa kutoa huduma, ulinzi, chakula, malighafi kama saruji tani 850,000, rebars tani 70,000 na pozzolana tani 250,000.

Naye Kaimu Mkurugenzi Huduma kwa Wateja wa Shirikal la Umeme Tanzania (TANESCO), Martin Mwambene, alisema maji ya kujaza bwawa hilo yanategemewa kutoka mikoa 10 nchini ambayo ni Tabora, Pwani, Singida, Morogoro, Mbeya, Lindi, Ruvuma, Iringa, Njombe na Dodoma.

"Tunaiomba jamii itumie maji kwa utaratibu endelevu kwamba kuna watumiaji wengine likiwamo bwawa hili lililojengwa kwa fedha zetu Watanzania na wananchi wanaotegemea Mto Rufiji kuendesha maisha yao, tupande miti na kutunza mazingira kwa faida ya wote," alisema.

Alisema kujaa kwa bwawa hilo kunategemea mvua na chemchem nyingine na kwamba kukiwa na matumizi endelevu umeme utapatikana na kuchagiza shughuli za uchumi kwa wananchi wengi kuachana na shughuli hatari kwa mazingira na kutumia nishati hiyo kujinufaidha kiuchumi.

"TANESCO tunatoa elimu kila siku kwamba megawati moja, mti mmoja, maana yake tuwajibike kupanda miti na kulinda iliyopo. Tunashirikiana na wizara nyingine kuelimisha umma kuwa na matumizi endelevu," alisema.

Mkataba wa ujenzi wa JNHP ulisainiwa Desemba 15, mwaka 2018, ikiwa ni kazi ya miezi 42 kati yake sita ni ya kujiandaa na 36 ya ujenzi, kazi ilianza rasmi Juni 15, mwaka 2019 na ilitakiwa kukamilika Juni 14, mwakani, lakini kutokana na kuchelewa kwa baadhi ya vifaa kutoka nje kwa sababu mbalimbali ikiwamo COVID uliongezwa mwaka mmoja.

Mradi huo umeajiri jumla ya watu 12,298 huku 11,190 sawa na asilimia 90.99 ni Watanzania na 1,108 sawa na asilimia 11.01 ni raia wa kigeni.

# Kanisa lataka uchunguzi askofu aliyeopolewa ziwani

**Na Neema Emanuel,** MWANZA

MWILI wa Askofu mstaafu, Boniphace Kwangu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Nyanza, uliopolewa Ziwa Victoria, umezikwa makao makuu ya kanisa hilo jijini Mwanza.

Vilevile, kanisa hilo limeliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina kuhusu chanzo cha kifo hicho.

Akizumgumza katika ibada ya mazishi, Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglican Tanzania, Mahimbo Mndolwa alisema walifikia uamuzi wa kuzika ingawa hawajajua chanzo cha kifo hicho.

Alisema wana imani na polisi kwamba watafanya uchunguzi ili waliohusika na kifo hicho kwa namna moja ama nyingine wachukuliwe hatua.

"Watu waovu wenye uwezo wa kudhuru mtu mwingine hawatavumiliwa na kwamba Mungu anawajua walioshiriki kuondoa uhai wa mpendwa wetu, hivyo tunaamini vyombo vya usalama vitalifanyia kazi suala hili.

"Tunawashukuru sana kwa namna ambavyo mmeshirikiana nasi na hatimaye kuturuhusu tulaze mwili wa ndugu yetu kwa heshima, asanteni mliofanya kazi ya kutafuta mwili huu tangu tulipopewa taarifa ya kupotea kwake, asanteni familia kwa uvumilivu, pia asanteni kanisa kwa uvumilivu.

"Polisi tusaidieni sisi hatuna moyo wa kufika mbali, lakini ninyi mmepewa, hatuna macho ya kuona mbali, lakini ninyi Mungu amewapa, sisi hatuna mkono wa kumshika muovu, lakini Mungu amewapa mkono, tunawaomba ili kama kuna yeyote aliyehusika na jambo kwa namna moja ama nyingine haki ya Mungu ipate kutendeka na familia ipate amani.

"Kazi ya kanisa ni kuombea na kusamehe. Kama kuna aliyehusika tukimjua tutamleta kwa Mungu na mengine tutayaachia serikali kufanya wajibu wao," alisema.

Askofu wa kanisa hilo Dayosisi ya Kagera, Darlington Bendakeha, alisema kuna watu wengine wanaoishi kana kwamba wataishi milele na kusahau kwamba wameumbwa kwa udongo.

Alisema wanadamu lazima wajifunze kuhesabu siku wanazoishi duniani kwa kuwa maisha ni mafupi, hivyo wanatakiwa kuishi kwa kufuata kanuni mbili muhimu za kumpenda Mungu na kumpenda jirani kama nafsi yao.

"Siku tunaishi kwenye dunia ambayo mauaji ni kitu cha kawaida, kuna mauaji na ukatili mkubwa ndani ya jamii zetu, mtu haogopi kumchinja mwenzake kwa ajili ya kupata utajiri, hatujui nani kesho atafuata, ili kuishi kwa kuhesabu siku, lazima mtu ujenge nguvu ya imani," alisema.

Mtoto wa marehemu, Digracius Ngwira, akizungumza na waandishi wa habari baada ya maziko ya baba yake, alisema walipata mshtuko baada ya kutoweka nyumbani kwao Novemba 28, mwaka huu.

Alisema baada ya baba yao kutoweka nyumbani, waliingia katika maombi kwa kuwa ni tukio la kwanza kutokea ndani ya familia yao.

Alisema kuwa siku chache baada ya kutoweka nyumbani, mwili wa baba yake uliopolewa kwenye Ziwa Victoria eneo la Bukumbi.

"Kama alivyosema Askofu Mkuu, tunaamini katika msamaha na haki na wale waliopewa jukumu la kusimamia wafanye hivyo na sisi tunaamini katika msamaha mara nyingi hatusamehi kwa sababu ya tunayemsamehe, bali tunasamehe kwa ajili yetu sisi," alisema.

Ngwira alisema baba yao alikuwa mpole, mkimya, asiyesependa kusema ovyo na alipita katika vikwazo vingi kwenye maisha yake.

Alisema wanamshukuru Mungu baba yao alisimama mpaka mwisho na ikampendeza Mungu kumchukua kwa njia hiyo.

Akisoma wasifu wa marehemu, mdogo wa marehemu, Benedict Kwangu alisema alizaliwa Februari 7, 1961 katika Kijiji cha Kalebezo, Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza.

Alisema kaka yake alisoma shule za msingi Kalebezo na Busekeseke zilizoko wilayani humo na kuhitimu masomo yake mwaka 1976.

"Mwaka 1977 alijiunga na Shule ya Sekondari Lake iliyoko jijini Mwanza, mwaka 1981 alijiunga na kidato cha tano baadaye alijiunga Chuo cha Ualimu Mkwawa mkoani Iringa kusomea stashahada.

"Baada ya kuhitimu ualimu, mwaka 1984 alijiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Masange, Tabora na 1985 aliajiriwa kama mwalimu katika Shule ya Sekondari Mwanza.

"Mwaka 1986 aliajiriwa katika Dayosisi ya Victoria Nyanza (DVN), akiwa ofisa miradi msaidizi. Askofu Boniface William Kwangu alipata wito wa kumtumikia Mungu mwaka 1987 na mwaka huo huo alijiunga na Shule ya Biblia Nyakato kwa ajili ya kupata mafunzo ya uinjilisti.

"Mwaka 1988 hadi 1990 alisoma stashahada ya Theologia katika Chuo cha St. Philip's Theological College, Kongwa mkoani Dodoma.

"Ilipofika mwaka 1991, alikuwa shemasi na kufanya kazi katika Kanisa Kuu la Mt. Nicholaus na mwaka 2007 aliwekwa wakfu na kusimikwa kuwa askofu wa nne wa Dayosisi ya Victoria Nyanza (DVN)," alisema.

HABARI KITAIFA

## Marafiki wanne jela kwa mauaji ugomvi mpenzi kwenye kigodoro

**Na Grace Gurisha**

MARAFIKI wanne wakazi wa Tegeta cha Simba, Dar es Salaam wamehukumiwa kifungo cha miaka sita jela baada ya kukiri kumuua bila kukusudia, Tamimu Athuman wakati wa ugomvi wa kumgombania mwanamke, baada ya kutoka kwenye ngoma ya kienyeji 'Kigodoro'.

Marafiki hao ambao ni vijana ni Nassoro Hamad, Hassan Salum, Rajabu Juma na Hassan Hamad, walikuwa wakimzuia marehemu asiondoke na Rehema Mohamed kwa sababu tayari alishakubali kuutumia usiku huo na Nassoro.

Akisoma adhabu hiyo, Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam alisema amesikiliza sababu za pande zote mbili kuwa washtakiwa hawana kumbukumbu za nyuma za jinai na pia wapunguziwe adhabu.

Alisema mshtakiwa wa kwanza Nassoro atatumikia kifungo cha miaka mitatu jela ambapo kwa kawaida adhabu ya kuua bila kukusudia ni miaka 11, amerejea muda wa miaka sita waliyokaa gerezani ndiyo maana ametoa adhabu hiyo.

"Hii itakuwa fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama yake. Ungeamua kuachana na Rehema mauaji yasingetokea kwa sababu wewe ndiyo ulikuwa mhusika," alisema Kabate.

Alisema mshtakiwa wa pili Hassan atatumikia kifungo cha miezi sita jela kutokana na utetezi wake aliyoutoa kwamba wakati anakamatwa alikuwa na umri wa miaka 18, alipelekwa mahabusu akiwa na umri mdogo kwa hiyo aliomba apunguziwe adhabu.

Akiendelea kutoa adhabu hizo, Kabate alisema mshtakiwa wa tatu Rajabu atatumikia kifungo cha miaka miwili jela na mshtakiwa wa nne atatumikia kifungo cha miezi sita jela kwa sababu kwenye utetezi wake alidai kuwa kipindi anakamatwa alikuwa na umri wa miaka 17.

Hakimu Kabate alimweleza Hassan kuwa licha ya kwamba alipelekewa mahabusu akiwa na umri mdogo, lakini alikuwa na akiri timamu, alipomuliza yeye alimfanya nini marehemu? Alidai alimpiga ngumi.

Kabla ya adhabu hiyo kutolewa, Wakili wa Serikali Veronica Mtafya, aliieleza Mahakama kuwa hawana kumbukumbu za nyuma za makosa ya jinai ya washtakiwa, lakini anaomba adhabu kali itolewe ili iwe fundisho kwao na kwa wengine.

Mawakili wa Utetezi, waliomba wateja wao wapunguziwe adhabu kwa sababu ndiyo kosa lao la kwanza, wamekaa mahabusu muda mrefu na pia hawajaisumbua Mahakama.

Ilidaiwa kuwa Oktoba 30, 2016 washtakiwa wakiwa eneo la Tegeta cha Simba ndani ya Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam washtakiwa wote wakiwa wakazi wa eneo hilo walikuwa wakimfahamu marehemu kabla ya mauaji.

Alidai kuwa tarehe hiyo washtakiwa walikuwa kwenye mji wa Zainabu kwenye ngoma ya kienyeji inayojulikana kama kigodoro, Nassoro alipanga kuutumia usiku huo na Rehema.

Ilidaiwa ilipofika majira ya saa saba usiku Nassoro alimuona Rehema akiwa ameongozana na marehemu na watu wengine, baada ya mita chake kutoka kwenye nyumba ya Zainabu marafiki wa Nassoro walimvamia marehemu hawakutaka Rehema aondoke nae.

Katika kurupushani ya ugomvi huo ndipo marehemu alipochomwa visu sehemu mbalimbali za mwili wake, alipelekewa katika Hospitali ya Lugalo kwa ajili ya matibabu lakini baadaye alifariki.



Watuhumiwa wa kesi ya mauaji wakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuhukumiwa kwenda jela, (kushoto) ni Rajabu Juma, ambaye amehukumiwa miaka miwili, Hassan Hamad (wa pili kushoto) amehukumiwa miezi 6, Hassan Salum (miezi 6), na Nassoro Shaban (miaka mitatu). **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mahakama Kuu: CAG Assad aliondolewa kinyume cha katiba

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masjala Kuu imetamka kwamba kuondolewa kwa aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad kulifanyika kinyume cha Katiba.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya jopo la majaji watatu Jaji Juliana Masabo, Jaji Edwin Kakolaki na Jaji Dk. Benhaji Masoud kutokana na shauri la kikatiba lililofunguliwa Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe kupinga kuondolewa kwa Prof. Assad madarakani.

Jopo la majaji hao lilisema kwamba uamuzi huo umefikiwa baada ya kupitia hoja za pande zote mbili na kubaini kulikuwa na ukiukaji wa Katiba katika kuondolewa kwa mlalamikiwa wa nne (Prof. Assad) katika Ofisi ya CAG kwa mujibu wa kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma kabla ya kufikisha umri wa miaka 65.

"Kumwondoa mlalamikiwa wa nne katika nafasi yake kunakiuka ibara ya 144(1) ya Katiba," ilisema sehemu ya hukumu hiyo huku Mahakama ikisema haitoi agizo lolote kuhusu gharama kama ombi lilivyokuwa.

Zitto aliwasilisha maombi dhidi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Charles Kichere (CAG) na Prof. Assad aliyeondolewa madarakani Novemba 2, 2019.

**KAULI YA ZITO**

Muda mfupi baada ya kutolewa kwa uamuzi huo jana, Zitto kupitia taarifa yake kwa umma, alisema amefarijika kwa uamuzi huo wa Mahakama Kuu kuhusu shauri hilo.

"Shauri hili lilikuwa linapinga sheria iliyotumika kutenguliwa kwa Prof. Mussa Assad kama CAG na kuteuliwa kwa Charles Kichere. Mahakama Kuu imekubaliana na shauri hili kuwa sheria iliyotumika ni batili.

"Kwamba ukomo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umewekwa na Katiba na sheria iliyoweka muhula inapingana na Katiba. Prof. Mussa Assad alipaswa kuhudumu kama CAG mpaka umri wa kustaafu ufike kwa mujibu wa Katiba.

"Nimefarijika sana kuwa Mahakama Kuu imesimama na Katiba katika shauri hili. Kwamba sasa haitatokea tena kwa mtu mmoja, hata kama ni Rais, kuamua tu kuvunja Katiba ya nchi yetu atakavyo.

"Muhimu zaidi ni kwamba kwa hukumu hii CAG wote wajao katika nchi yetu sasa wamelindwa rasmi kwa uamuzi wa mahakama," alisema.

**KUKATA RUFANI**

Hata hivyo, Zitto alisema mahakama imekataa kukubali maombi yao ya kwamba kuteuliwa CAG mwingine ilikuwa batili.

"Hili tutakwenda Mahakama ya Rufani ili iweze kulitolea uamuzi. Kama kuondolewa kwa Prof. Assad kulikuwa batili, ni dhahiri kuwa kuteuliwa kwa mtu mwingine kushika nafasi hiyo kulikuwa batili pia. Nimeshatoa maelekezo kwa mawakili wangu wakate rufani katika eneo hilo la hukumu," alisema.

Zitto aliwashukuru mawakili wake Rugemeleza Nshala na Nyaronyo Kicheere kwa kazi kubwa ya kumwakilisha pamoja na Wakili Bonifasia Mapunda aliyekuwa wakili wa Prof. Assad katika kesi hiyo.

"Kwa namna ya pekee ninatoa shukrani zangu kwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) chini ya uongozi wa dada Wakili Anna Henga na Wakili Fulgence Masawe kwa msaada wao mkubwa katika shauri hili muhimu sana kwa nchi yetu. Ahsanteni sana," Zitto alisema.

Mhadhiri huyo wa zamani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema anafikiri kusamehe ni jambo muhimu kwa watu wote.

Alipoulizwa kuhusu mipango yake ya maisha baada ya kuondoka katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Prof. Assad alisema: "Sina 'position' (nafasi) yoyote kwa sasa, nipo kwenye kitu kinachoitwa maandalizi ya kustaafu, nimekaa nyumbani nikiwa nina (umri wa) miaka 58," alisema.

Prof. Assad alisema kwa kuwa taratibu za nchi haziruhusu CAG kufanya kazi yoyote ya serikali baada ya kuondoka katika nafasi yake hiyo, atalazimika kurejea nyumbani kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji.

"Ninakwenda kufuga kuku, tuna mashamba tumeyaanzisha, nina mambo mengi ya kufanya," Prof. Assad alisema.

Novemba 4, 2019, ikiwa ni siku mbili baada ya kuondolewa katika nafasi ya CAG akiwa na umri wa miaka 58, Prof. Assad aliahidi kukutana na Kichere Dodoma kumpatia ushauri wake, akitamka kuwa ni mwanafunzi wake.

Desemba Mosi, 2014, Ikulu ilitangaza kuwa Rais Jakaya Kikwete alikuwa amemteua Prof. Assad kuwa CAG na uteuzi wake ulikuwa umeanza tangu Novemba 5, mwaka huo.

Kabla ya uteuzi huo, Prof. Assad alikuwa Profesa Mshiriki, Idara ya Uhasibu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na alichukua nafasi ya mtangulizi wake Ludovick Utouh aliyestaafu kwa mujibu wa sheria.

Prof. Assad ni msomi, mwenye weledi, ujuzi na uzoefu mkubwa wa uhasibu na udhibiti wa fedha ambaye ana Shahada ya Uzamivu wa Uhasibu (PhD in Accounting) kutoka Chuo Kikuu cha Southampton, Uingereza mwaka 2001 na Shahada ya Uzamivu katika Udhibiti wa Fedha (MA in Financial Accounting) kutoka Chuo Kikuu cha Dublin City, Jamhuri ya Ireland, 1991.

# Ndugu wakabidhiwa mwili mlinzi anayedaiwa kuuawa

**Na Julieth Mkreri,** KIBAHA

NDUGU wa mlinzi wa Kampuni ya Ulinzi ya Homasa wamekabidhiwa mwili wa Salim Haji (29), kwa ajili ya taratibu za mazishi baada ya kuridhishwa na majibu ya uchunguzi uliofanyika.

Salim anadaiwa kupigwa risasi na bosi wake wa Kampuni ya Kopa Gesi na baadaye mwili huo kuokotwa huko Misugusugu Kibaha na kuhifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi, Mkoa wa Pwani.

Akizungumza na Nipashe mjini Kibaha, baba mdogo wa marehemu, Frank Shenkawa, alisema mwili huo wamekabidhiwa Jumapili majira ya saa moja jioni wakiruhusiwa kuendelea na taratibu za mazishi.

Alisema wanatarajia kufanya shughuli za maziko leo katika kijiji cha Ngwelo, Bumbuli Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga.

Aidha, walisema baada ya maziko wataendelea kufuatilia kuhakikisha sheria inachukua mkondo wake kwa anayedaiwa kutenda kosa hilo.

Salim anadaiwa kupigwa risasi Novemba 20, mwaka huu, akiwa lindoni eneo la kuhifadhia mitungi ya gesi huko Tegeta Scanska alikokuwa anafanyia kazi ya ulinzi.

Baada ya tukio hilo ndugu walihangaika kumtafuta akiwa hai au amekufa kwa zaidi ya siku saba hadi walipojulishwa mwili huo kuhifadhiwa katika Hospitali ya Tumbi, Kibaha.

Shenkawa alisema katika kuutambua mwili walikuta ukiwa na jeraha juu ya masikio yote mawili, linalodaiwa kutokana na risasi.



Mwili wa aliyekuwa mlinzi wa Kampuni ya Ulinzi ya Homasa, Salim Haji, ukitolewa katika chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Tumbi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge Kishoa ahojiwa kuhusu kiapo alichotoa

**Na Grace Gurisha**

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Jesca Kishoa (33) jana alihojiwa na jopo la mawakili wa chama hicho kuhusu kiapo alichokiwasilisha katika kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama.

Kesi hiyo inayowahusisha wabunge 19 wa chama hicho wakiongozwa na Halima Mdee, waliifungua Julai 21 mwaka huu dhidi ya CHADEMA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wakipinga uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kuwavua uanachama Mei 11 mwaka huu.

Akiwa mahakamani Kishoa aliulizwa maswali na Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam, ambapo awali alidai aliomba aongezwe muda wa kufika mbele ya Kamati Kuu ya CHADEMA.

Kishoa alidai aliomba hivyo kutokana na maneno yaliyoibuliwa na Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika yaliyoleta chuki kwa wafuasi wa chama hicho, alipopata barua ya wito Novemba 25, mwaka jana alitaka kamati hiyo impe muda wa kujituliza kutokana na hali iliyokuwa imeibuliwa na Mnyika. Akiendelea kujibu maswali ya Wakili Peter Kibatala, Kishoa alidai alipoomba aongezwe muda alikataliwa.

Pia alidai barua hiyo ya wito ilikuwa na shida kwa kuwa ingeambatanishwa na hati ya mashtaka na pia ni barua ambayo ilitumwa kwa njia ya mtandao wa WhatsApp ambao siyo rasmi.

Pia alidai hadi sasa yeye ni mwanachama wa CHADEMA, hata kwenye hati yake ya kiapo inaonyesha hivyo kwamba uhusiano wake na CHADEMA umejengwa na Katiba ya chama hicho.

Katika shauri hilo namba 36 la mwaka 2022, wabunge hao pamoja na mambo mengine, wanaiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi huo wa CHADEMA kuwafukuza kisha itoe amri tatu.

Wabunge hao wanaomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza na amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutokuchukua hatua yoyote mpaka malalamiko yao yatakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

## Wanaharakati wafichua faida, hasara ya mitandao ya kijamii

**Na Jenifer Gilla**

WANAHARAKATI wa haki za binadamu na ukatili wa kijinsia nchini wamesema mitandao ya kijamii inaweza kumaliza au kuchochea udhalilishaji wa kijinsia jamii itakavyoamua kuitumia.

Wamesema madhara ya udhalilishwaji wa kijinsia mtandaoni ni makubwa kwa kuwa taarifa zake zinawafikia watu wengi kwa muda mfupi na kusababisha mhusika kupata msongo wa mawazo na kufikia hatua ya kujitoa uhai wake.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema mitandao ya kijamii ina mchango mkubwa katika kupunguza ukatili wa kijinsia ikiwamo kufichua unyanyasaji wanaofanyiwa watu majumbani.

"Kwa mfano hivi karibuni kupitia hii mitandao tumefanikiwa kumkamata mzazi aliyemfanyia tohara binti yake na kutuma kadi za mwaliko kwa watu ili waende wakafanye sherehe, kwa hiyo sisi wanaharakati imetusaidia sana," alisema.

Alisema mitandao ya kijamii inawasaidia taasisi, wanaharakati na serikali kupata takwimu za uwapo wa matendo hayo ikiwamo aina za unyanyasaji wa kijinsia inayofanyika na mikoa ambayo matendo hayo yanafanyika sana.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Binti Makini Foundation, Janeth Kiko, alisema kuwapo kwa mitandao ya kijamii kunachangia kukua vitendo vya ukatili wa kijinsia kutokana na namna watu wanavyoitumia kusambaza matukio hayo na kuwafikia watu wengi zaidi.

Alisema kingine kinachochangia hali hiyo ni jamii kuitumia mitandao ya kijamii kama sehemu ya kulipiza visasi baada ya kuwa na migogoro na ndugu, jamaa au wapenzi wao kwa kutupa picha au video za faragha walizozipiga wakati wakiwa na mahusiano mazuri.

Alisema vitendo hivyo kwa sasa vimeanza kupungua baada ya serikali kuweka sheria ya makosa ya mtandao na baadhi ya watu kuadhibiwa kwa kufungiwa kurasa zao za mitandao au kupandishwa mahakamani.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Ladies Shine, Anita Kabwe, alisema mitandao ya kijamii inachochea kuongezeka kwa unyanyasaji wa kijinsia na hiyo inatokana na matendo ya jamii yenyewe ikiwamo kupiga picha za faragha na kuwatumia watu wao wa karibu.

Mkurugenzi wa Shirika la Zaina Foundation inayojishughulisha na kutetea haki za kidigitali, Zaituni Njovu, alisema jamii inapaswa kukemea vitendo vya udhalilishaji vinavyoendelea mitandaoni, huku wadau pamoja na serikali waendelee kuelimisha jamii kuhusu udhalilishaji wa mitandaoni na madhara yake lakini.

Aidha, alisihi jamii hasa wanawake kuacha kupiga picha au kujirekodi video ambazo zinaweza kuja kutumika kama fimbo ya kuwadhalilisha kwenye mitandao hiyo.

# Joto uchaguzi CCM laongezeka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHAMRASHAMRA za Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, utakaofanyika kesho na keshokutwa jijini hapo, zimepamba moto huku zikipandisha presha ya uchaguzi kwa wajumbe 30 wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC).

Barabara mbalimbali za jiji hilo zimepambwa kwa mabango na bendera za chama hicho huku nyumba za kulala wageni zikijaa kutokana na wageni na wapambe wanaokwenda kwenye mkutano huo.

Mkutano huo pamoja na kuchagua wajumbe wa NEC pia utakuwa na jukumu la kuwachagua Mwenyekiti wa CCM, Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa ratiba ya chama hicho, leo Halmashauri Kuu itafanya uteuzi wa mwisho wa wanachama walioomba kugombea nafasi za ujumbe wa NEC, viti 15 Tanzania Bara na 15 Tanzania Zanzibar.

Pia itateua jina la mwanachama atakayesimama katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa CCM, Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Tanzania Bara.

Baada ya uchaguzi, mkutano huo utatoa fursa ya kuchaguliwa wajumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, wajumbe wa sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa.

Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa Chama hicho, Shaka Hamdu Shaka, hivi karibuni alisema "Maandalizi ya mkutano mkuu wa 10 wa CCM ambao utafanyika Desemba 7-8, mwaka huu yanakwenda vizuri, tunakwenda kuwapata viongozi wa CCM ngazi ya taifa."

Alisema wajumbe wa NEC ambao hupatikana kwa kapu na ndio jukumu la mkutano huo, lakini mkutano utapokea taarifa ya utendaji kazi za chama na serikali kwa miaka mitano.

Kuhusu waliojitokeza kuomba kuteuliwa kuwania viti 30 vya NEC, Shaka alisema zaidi ya wanachama 3,000 wamejitokeza kuomba kugombea nafasi hizo na haijawahi kutokea tangu chama kiundwe.

Miongoni mwa waliojitosa kuwaomba kuwania wamo mawaziri, wafanyabiashara maarufu, waliowahi kuwa wabunge na makada mbalimbali.

**UVCCM WAONYANA**

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti mpya wa Jumuiya ya Vijana wa CCM (UVCCM), Mohamed Ally Mohamed (Kawaida), amewaonya vijana wanaoendekeza makundi na kusisitiza kuwachukulia hatua za kinidhamu wanaolenga kuvuruga na kuwagawa.

Akizungumza juzi na viongozi wa UVCCM pamoja na vijana kutoka maeneo mbalimbali, Mohamed, alisema uchaguzi umepita sasa ni muda wa kukijenga chama na jumuiya hiyo.

"Leo mmefanya mapokezi ya viongozi wenu ikiwa ni tafsiri sahihi kwamba uchaguzi umekwisha ni jukumu letu kulinda na kujenga ujamaa wetu kwa vitendo, na inatupasa makundi ya uchaguzi yaishe na wenye nafasi kubwa ya kumaliza makundi haya ni sisi vijana au viongozi tuliopewa dhamana na wale ambao hawakubahatika kupata dhamana hii," alisema.

"Kilichoshinda ni chama na sio mtu. Kijana yeyote anayeendeleza makundi maana yake ajenda yake ni tofauti na analenga kutugawa na kuvuruga umoja wetu tujue kwamba huyu sio mwenzetu na tunapaswa kumkemea vikali na ikibidi kumtenga," alisema.

Aidha, aliwataka vijana nchini kuepukana na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii kwa kutoa taarifa ambazo si sahihi kwa serikali au kwa viongozi.

"Kila mmoja kwa nafasi yake akatumie vizuri mitandao ya kijamii, twendeni tukahabarishe umma mambo makubwa yanayofanywa na serikali zetu chini ya Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi."

"Nitakuwa mkali sana kwa kikundi au mtu yeyote atakayetumia mitandao ya kijamii kupotosha kwa yale yanayofanywa na serikali ya CCM ni wajibu wetu vijana kusema mazuri yanayofanywa na serikali zetu, tuwe wazalendo wa kweli wa nchi yetu," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa UVCCM, Rehema Sombi, aliahidi kufanya kazi kwa kushirikiana akilenga mabadiliko yanayozingatia aina ya vijana waliopo sasa, aina ya maisha na vikwazo vinavyowakabili vijana.

Awali, Katibu Mkuu wa UVCCM Taifa, Kenani Kihongosi, alisema vijana kuungana na kuwa mstari wa mbele kukisemea chama hicho.




Makamu Mwenyekiti wa Kampuni ya Yapi Merkezi, Erdem Arioglu (katikati), akiongea katika hafla ya utoaji tuzo zilizoandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Halfa hiyo ya utoaji tuzo ilihudhuriwa na viongozi wa kampuni mbalimbali nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwanafunzi wa chuo apotea

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAFUNZI wa mwaka wa kwanza Chuo cha Afya St. Joseph, Zuwena Hamisi (22), anadaiwa kupotea tangu Novemba 20, mwaka huu alipokuwa katika hosteli za chuo hicho Kimara, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe, Raphael Mirambo, mwalimu wa binti huyo alisema siku ya tukio hakumwona darasani alipowauliza mwenzake anaoishi nao katika hosteli walisema kuwa walimwacha hosteli akiwa amelala na kuwa angehudhuria vipindi vinavyofuata, lakini hakufika chuoni hapo.

Alisema baada ya siku mbili wanafunzi hao walikwenda kutoa taarifa za kutoweka kwa Zuwena tangu siku waliyomuacha hosteli huku akiwa ameacha kila kitu ndani ikiwamo simu anayoitumia kwa ajili ya mawasiliano.

Alisema kuwa Zuwena ana matatizo ya kupoteza kumbukumbu, tatizo alilokuwa nalo kwa miaka miwili na wahiji wake ukiwa ni mrefu, mweupe na mara zote huwa anavaa hijab.

"Siku aliyotoweka ndio alikuwa na siku ya pili tangu afike chuoni, kwa kuwa wenzie walimwacha akiwa amelala hata hatufahamu alikuwa amevaa nguo gani, lakini ni binti anayejua kujieleza na kujitambulisha yeye ni nani," alisema Raphael.

Alisema baada ya kumtafuta kwa wiki mbili bila mafanikio walikwenda kutoa taarifa Kituo cha Polisi cha Kimara kupewa kumbukumbu namba KMT/RB/3449/22. Kwa yeyote atakayemwona apige simu 0688 912146 au atoe taarifa katika kilicho karibu na yeye.



# DC ataja vikwazo haki za binadamu

**Na Beatrice Moses**

VITENDO vya rushwa na uonevu unaohusisha kugushi nyaraka zinazotumika kupora haki za wanyonge ni miongoni mambo yanayotajwa kuwa tatizo la upatikanaji haki za binadamu na utawala bora.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, jana wakati alipofungua kongamano la wadau la kujadili haki za binadamu na utawala bora, maadili na mapambano ya rushwa.

Katika kongamano hilo lililofanyika Dar es Salaam, Ludigija aliihimiza taasisi za haki za binadamu kuona umuhimu wa kushughulikia haki za wananchi bila kujali tofauti ya kipato chao ili kujenga jamii yenye usawa.

"Pia kuna utunzaji mbaya wa nyaraka muhimu ambao hufanywa na baadhi ya wanafamilia, kisha nyaraka hizo huchukuliwa na wenye nia ovu ambao huzitumia kupora haki," alisema Ludigija.

Alitoa ushauri kwa wenye dhamana ya kusimamia haki za binadamu kuhakikisha kila mmoja ndani ya nchi hii ana haki zake, kudhibiti kughushi nyaraka na kuzichunguza Ili kudhibiti uonevu.

"Kuna baadhi ya watendaji hudhulumu haki za wanyonge kwa kushirikiana na wenye uwezo wa kifedha wanagushi nyaraka ya mwaka 1976 wakati huo ikichapwa kwa typewriter, lakini inaletwa ikionyesha imechapwa kwa kompyuta jambo la ajabu," alisema.

Ludigija alisema maadhimisho ya Siku ya Haki za Bidanamu ambayo nchi imepiga hatua kubwa wadau wajadiliane kutatua changamoto chache zinazojitokeza.

Ofisa Mfawidhi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora(THBUB) tawi la Dar es Salaam, Shoma Philip, alisema kongamano hilo ni sehemu ya maadhimisho ya Siku za Kitaifa ya Haki za Binadamu, wanatarajia litakuza uelewa na kuliwezesha taifa kutekeleza na kusimamia dhana ya maadili ya haki za binadamu, utawala bora na mapambano ya rushwa.

"Tutafakari wote kaulimbiu hii tukijikumbushe kuwa maadili na haki za binadamu sio anasa bali ni kitu muhimu katika maisha yetu bila kujali jinsia, umri na haki ya uchumi, wote tuna haki ya kufurahia huduma bora zinazotolewa na Taasisi za umma na binafsi bila kutoa rushwa," alisema Philip.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka 2022, "maadili, haki za binadamu, utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa ni jukumu la pamoja kati ya serikali, wananchi na wadau wengine.

Ofisa elimu kwa vijana kutoka Kituo cha Haki za Binadamu, Davis Komba, alisema ni vyema kuwekeza katika kuelimisha vijana na watoto kuhusu madhara ya ukatili na umuhimu wa kujitambua nafasi zao kuzingatia haki za binadamu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# *Wananchi waelimishwe viashiria ukatili kijinsia*

**MATUKIO** ya ukatili wa kijinsia yanapotokea katika maeneo mbalimbali, baadhi ya wananchi hushindwa kuyatambua na kuyaripoti kwa sababu ya kukosa uelewa au elimu.

Kuna matukio ambayo hufanyika katika jamii, lakini anayefanya kitendo hicho au watu wanaomzunguka kushindwa kuelewa kama huo ni ukatili.

Ndiyo maana kunahitajika elimu ili watu waweze kuelewa matukio hayo yanapofanyika waweze kuyakemea.

Pengine kutokuwa na elimu ya uelewa wa matukio hayo husababisha kushamiri na kila mara yakisikika kwenye vyombo vya habari mbalimbali yakiripotiwa.

Matukio ya ukatili wa kijinsia mengi yao yanafanywa na watu wa karibu. Inaposikika kuripotiwa mtoto amefanyiwa ukatili wa kunajisiwa, ikifuatiliwa itagundulika aliyemfanyia hivyo ni mjomba, baba wa kambo na wakati mwingine ni baba mzazi.

Kumekuwa na mtukio kadhaa pia ya watoto wa shule kufanyiwa ukatili wa kingono wanapokuwa wanakwenda shule na kurudi nyumbani kwa kutumia usafiri wa mabasi ya shule.

Watu wanaowafanyia ukatili huo ni wale wanaoaminiwa na wazazi na walimu, yaani makonda na madereva wa magari hayo.

Juzi juzi tu kumeripotiwa tukio la mwanafunzi kufanyiwa unyama wa kuchangiwa na konda na dereva kwa kuwa huwa wa kwanza kuchukuliwa na wa mwisho kurudishwa nyumbani na kufanyiwa unajisi huo.

Wazazi kwa kutofuatilia kwa imani ya watu waliowakabidhi watoto wao, hawawachunguzi au kuongea nao kujua maendeleo yao na watoto hao kwa kuwa hutishwa na wanao wafanyia vitendo hivyo, huogopa kuwaambia wazazi.

Inakisikitisha na kuumiza pale mzazi anapokuja kugundua mtoto akiwa ameshaharibika na wengine kupata ulemavu wa maisha.

Ndiyo maana kuna umuhimu mkubwa wa kuwapo kwa elimu itakayohusisha jamii nzima kufahamu matukio ya ukatili yanapotokea na kuyakemea ili yasiendelee kuwapo.

Katika baadhi ya nyumba vitendo hivyo hutokea na pengine majirani wanashuhudia, lakini wanashindwa kuwajulisha wazazi kwa kutokuwa na ushirikiano au ukaribu.

Wengine wanashindwa kuelewa ukatili wa kijinsia ni upi ili unapotokea mtu aweze kuuripoti.

Baadhi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ni vipigo, ukeketaji kwa watoto, unyanyasaji wa aina yoyote ikiwamo wasaidizi wa ndani kupewa kazi kubwa kuliko uwezo wao na kunyimwa chakula.

Hivyo ni baadhi tu ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na mtu yeyote anapoona vinafanyika katika eneo lake analoishi au kwa jirani yake anapaswa kutoa taarifa, ili kunusuru mhusika asiendelee kupata mateso zaidi.

Katika kipindi cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, elimu na shuhuda mbalimbali zimekuwa zikitolewa ili kuhakikisha vitendo hivyo vinatokomezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, anasema mitandao ya kijamii ina mchango mkubwa katika kupunguza ukatili wa kijinsia ikiwamo kufichua unyanyasaji wanaofanyiwa watu majumbani.

Vilevile, mitandao ya kijamii inasaidia taasisi, wanaharakati na serikali kupata takwimu ya uwapo wa matendo hayo ikiwamo aina za unyanyasaji wa kijinsia inayofanyika na mikoa ambayo matendo hayo yanafanyika sana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# *Kampeni vyoo bora shuleni zianze sasa*

**RIPOTI** ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2020/2021 inaonyesha kuwa halmashauri 77 zinakabiliwa na uhaba wa matundu ya vyoo zaidi ya 111,931.

Inavyoelekea uhaba ni karibu katika mikoa yote na ukweli ni kwamba wanafunzi wana matatizo ya sehemu salama za kujisaidia wakiwa shuleni.

Ni jambo ambalo sasa linatakiwa lifike mwisho kwa vile moja ya mahitaji muhimu ya binadamu wanapokuwa kwenye mkusanyiko iwe ni shuleni, nyumba za ibada, shuleni na hata kazini ni pamoja na chakula, maji na choo.

Inavyoelekea karibu asilimia zaidi ya 50 ya shule nchini huenda hazina vyoo na hiyo ni changamoto kwa wanafunzi wakiwamo wasio na mahitaji maalumu na wanaoishi na ulemavu.

Kinachoonekana sasa ni walimu, wazazi na walezi na viongozi wa kamati za shule kwa zile za msingi na bodi kwa sekondari na viongozi wa halmashauri kufanya utafiti pamoja na kuamua jinsi ya kuwashirikisha wanafunzi na jamii kuchimba mashimo ya vyoo na kukabiliana na ukosefu huo.

Wakati mwingine inaweza kuwa rahisi kujenga vyoo kama kutakuwapo na mashimo yaliyochimbwa kama ambavyo zama hizi wananchi wanajenga maboma na serikali inayakamilisha kwa kuyaezeka, kuweka milango, madirisha, rangi na kumalizia kwa samani na hapa shule imekamilika.

Kushindwa kuwapatia watoto huduma ya choo bora ambayo ni muhimu kwa afya inasababisha watoto hao kuchukia au hata kutoroka shule kwa kuona kuwa ni kero, kwa upande wa mabinti nao ni tatizo, hasa wanapokuwa kwenye mzunguko wa kila mwezi.

Ikumbukwe uhaba wa vyoo umechangia baadhi ya wanafunzi kupata maradhi kama ya tumbo na maambukizi ya njia ya mkojo (UTI) na hata kuwakwamisha kitaaluma kutokana na utoro wa mara kwa mara kwa mara wapo wanaomaliza darasa la saba hawajui kusoma na kuandika.

Ni vyema serikali za wilaya ziandae utaratibu wa kujengwa vyoo vikiwamo vya wanafunzi wenye changamoto za ulemavu zinazowarudisha nyuma wakati wa kujifunza kwa vile ukosefu wa choo au kuwapo na vyoo vibovu, vichafu visivyo na viwango vya mahitaji ya kundi hilo, kunawaumiza zaidi wanaoishi na ulemavu.

Ukiacha madai kuwa jamii haina shule wala mabweni ni lazima pia kuzungumzia umuhimu wa walimu, wazazi na walezi kushirikiana na kujenga vyoo kwani hata wao wana nafasi kubwa ya kuchangia tatizo hili la kukosa vyoo listokee.

Zipo changamoto nyingi zinazomrudisha nyuma mtoto katika kujifunza si shuleni pekee hata nyumbani, ikiwamo kukoseshwa raha na mazingira anayosomea na kuchukuliwa na wanafunzi wengine kama ana tatizo na hata kutengwa na kunyanyapaliwa kutokana na hali unayoweza kuwa nayo.

Eneo hili linawahusu wasichana na wenye ulemavu ambao kutokana na hali ya kimaumbile wanalazimika kuhitaji huduma hiyo zaidi kuliko wengine.

Lakini mtoto hasa binti anashindwa kuzitolea taarifa changamoto anazokutana nazo wakati wa hedhi kutokana na kukosekana maji na vyoo shuleni.

Kwa sababu ya kukosekana mazingira rafiki kati yake na mzazi, mlezi au mwalimu ikiwamo ukali uliopitiliza anaamua kuvumilia lakini akishindwa kujifunza na kurudi nyuma kimasomo na kitaaluma.

Kuna haja ya wazazi na walezi kuongeza ukaribu na walimu watoto wao shuleni ili kutatua mambo yoyote yanayowakwamisha ukiwapo uhaba wa vyoo na kuwasababishia kuichukia shule na kuiona kama sehemu yenye kinyaa, yenye harufu mbaya, inzi na hata inayokera kukaa.

Lakini wazazi na walezi ni wakati wa kutenga muda wa kutembelea shule na kushirikiana na walimu, viongozi wa serikali na watoto wenu ili kutambua changamoto wanazopitia.

Suala la kumsaidia mtoto kielimu linahusisha pia kugundua changamoto zinazokabili katika kujifunza na kuzitafutia ufumbuzi na hilo ni jukumu la mzazi, walimu na mlezi.

Kwa maana hiyo ikiwa wazazi na walezi mmetambua changamoto saidieneni na walimu kuzimaliza ili kuwasaidia watoto wawe darasani kwa furaha na kupenda masomo.

Wazazi wengi na walezi wana dhana ya kuwa suala la elimu ni jukumu la serikali jambo ambalo sio kweli kwa sababu ujenzi wa choo wakati mwingine ni kazi ya serikali lakini hata wazazi pia.

Ni wakati wa wazazi na walezi kuamka na kubeba jukumu hili muhimu la kumsaidia mtoto kupambana na changamoto zinazomrudisha nyuma kimasomo ili kutokomeza tatizo la watoto kujifunza kwenye mazingira machafu yanayopambwa na kinyesi.

# Kesi kocha Simba yapigwa kalenda

**Na Grace Gurisha**

KESI ya tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya inayomkabili aliyekuwa Kocha wa Makipa wa Klabu ya Soka ya Simba, Mwalami Sultan na wenzake watano imeahirishwa kwa njia ya mtandao hadi Desemba 19, mwaka huu, kwa sababu upelelezi haujakamilika.

Mbali na Sultan, washtakiwa wengine ni Mmiliki wa Kituo cha Soka cha Kambiasso Sports Academy, Kambi Seif, Maulid Mzungu, Said Matwiko, John John na Saraha Eliud.

Wakili wa Serikali Caroline Matemu alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa kesi ililetwa kwa ajili ya kutajwa na upelelezi haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Kutokana na hali hiyo, Hakimu Mrio aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 19, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

Hayo yote yaliendelea kwa njia ya mtandao ambapo washtakiwa hawakuletwa mahakamani hapo, kesi iliendeshwa washtakiwa wakiwa gerezani kwenye ukumbi maalum.

Ilidaiwa kuwa Oktoba 27, mwaka huu, huko katika eneo la Kivule, ndani ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 27.1 za dawa za kulevya aina ya herione.

Katika shtika la pili, ilidaiwa kuwa Novemba 4 mwaka huu, huko Kamegele katika Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroine.

Hata hivyo, washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu kitu chochote mahakamani huko kwa kuwa Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kilimo Maendeleo, Mathew Ngwahi (kushoto), akizungumza katika hafla na wadau mbalimbali wa sekta ya fedha na ubunifu iliyoandaliwa na UNCDF pamoja na Infinix jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watatu wafariki dunia kwa ajali ya gari Moro

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WATU watatu wamefariki dunia katika ajali iliyohusisha magari mawili kugongana uso kwa uso kisha kugonga pikipiki mbili kwenye eneo la Magunila -Mkundi barabara kuu ya Morogoro- Dodoma, Manispaa ya Morogoro.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 11:25 alfajiri.

Aliwataja waliofariki dunia ni dereva wa pikipiki Faustine Cornel (28) na abiria wake Ashraff Yusufu (43), wote wakazi wa Kihonda na dereva mwingine wa pikipiki, Robson Mkuchu (25), mkazi wa Mkundi.

Kamanda Musilimu alisema ajali hiyo ilihusisha gari lenye namba za T 514 BAT aina ya Toyota Land Cruiser, mali ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Morogoro ikiendeshwa na Abeid Abeid (53), mkazi wa Mkundi Morogoro akitokea Mkundi kuelekea katikati ya mji.

Kamanda Musilimu alisema dereva huyo aliyapita magari mengine bila tahadhari na kuligonga gari lililokuwa mbele yake lenye namba za usajili 2032 JW 12 aina ya Ashock Leyland, mali ya Jeshi la Wananchi lililokuwa likiendeshwa na Joseph Mollel (46), mkazi wa Kihonda Azimio likitoka Veta - Kihonda kwenda mjini lililokosa mwelekeo na kuzigonga pikipiki mbili zilizokuwa mbele yake.

Kamanda huyo alizitaja pikipiki hizo ni zenye namba za usajili MC 367 DFN iliyokuwa ikiendeshwa na Faustine Cornel (28), mkazi wa Kihonda aliyembeba abiria aitwaye Ashraff Yusufu (43), mkazi wa Kihonda.

Kamanda Musilim alitaja pikipiki nyingine iliyogongwa kuwa ni yenye namba za usajili MC 450 EDL aina ya UB iliyokuwa ikiendeshwa na Robson Mkucha (25), mkazi wa Mkundi ambaye hakuwa amebeba abiria wakitokea Mazimbu kwenda Mkundi.

Kamanda huyo alisema miili ya marehemu hao imehifadhiwa kwenye chumba cha kuhifadhi maiti Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

Alisema chanzo cha ajali ni uzembe wa dereva wa gari T 514 BAT aliyeyapita magari mengine ya mbele yake bila kuchukua tahadhari.

Kamanda Musilimu aliwataka madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani na kuwa na udereva wa kujihami muda wote.

## KABWELA

Fadhili Mohamed



# Wakaguzi wa ndani waonywa usimamizi mbovu wa miradi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAZIRI wa Fedha na Uchumi, Dk. Mwigulu Nchemba, amewaonya wakaguzi wa ndani katika halmashauri zote nchini dhidi ya usimamizi mbovu wa miradi ya maendeleo iliyoko katika maeneo yao, akisisitiza atakayeshindwa kukagua miradi hiyo atakuwa amejifuta kazi.

Amesema halmashauri ambayo itakuwa imepata hati chafu, watumishi wote wa umma waliosababisha kupatikana kwa hati chafu watajitathmini kwa kuwa hawafai kuwa serikalini.

Dk. Nchemba amesema Rais Samia Suluhu Hassan alishatoa maelekezo hakuna kuzuia fedha kwenda halmashauri kwa sababu ya hati chafu, hivyo hatua zitakuwa zinachukuliwa kwa waliosababisha hati chafu kupatikana.

Alitoa angalizo hilo wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Tarafa ya Ndago wilayani Iramba mkoani hapo juzi.

Dk. Nchemba ambaye ni Mbunge wa Iramba Magharibi, alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi lakini miradi mingi iliyojengwa inakuwa hailingani na fedha zilizotolewa.

"Nitaongea na wenyeviti wa halmashauri zote pamoja na wabunge, ukikuta mradi mpaka anakagua mkaguzi wa nje halafu mkaguzi wa ndani hajakagua, mkaguzi wa eneo hilo atakuwa amejifuta kazi mwenyewe," alisema.

"Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) iliyotolewa mwaka huu ilionyesha kuwa katika mwaka wa 2020/21 kulikuwa na jumla ya hati 999 za ukaguzi. Kati yake, hati 185 za mamlaka za serikali za mitaa, 195 za mashirika ya umma, hati 308 za serikali kuu, hati 19 za vyama vya siasa na hati 292 za miradi ya maendeleo.

"Kati ya hati 999 zilizotolewa, hati zenazoridhisha ni 970, sawa na asilimia 97.1, hati zenye shaka ni 19 sawa na asilimia 1.9, hati mbaya ni sita na hati nne za kushindwa kutoa maoni," alifafanua.

Katika ripoti hiyo, taasisi zilizopata hati zenye shaka ni Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe (Pwani), Longido (Arusha), Mlele (Rukwa), Musoma (Mara), Sengerema (Mwanza) na Bunda (Mara).



Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA), Sheikha Mohamed, wakibadilishana hati za makubaliano yanayolenga kuboresha mafunzo ya taaluma za usafiri wa maji, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NIT, ZMA waingia makubaliano kuboresha mafunzo usafiri majini

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeingia makubaliano na Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA) kuboresha mafunzo ya taaluma za usafiri wa majini.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kutia saini makubaliano hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa na Mkurugenzi Mkuu wa ZMA, Sheikha Mohamed, walisema makubaliano hayo yatasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha taaluma katika eneo la usafiri wa maji na kuandaa wataalamu wabobezi kwenye sekta hiyo.

Prof. Mganilwa alisema kupitia makubaliano hayo, ZMA itatoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa NIT, hivyo kuhitimu kama wataalamu wabobezi kwenye eneo la usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji.

"Madhumuni makuu ya makubaliano haya ni kuimarisha uhusiano kati ya NIT na ZMA katika kuboresha ujuzi kwa wanafunzi na wafanyakazi katika maeneo ya usafiri wa njia ya maji. "Tumeingia makubaliano katika maeneo kadhaa, mojawapo ni mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi, mafunzo kwa wafanyakazi, kubadilishana utaalamu, ziara za mafunzo ama masomo na vilevile kukuza uhusiano kwa wafanyakazi," alisema Prof. Mganilwa.

Mkuu wa Chuo huyo aliyataja maeneo mengine ya ushirikiano katika mkataba huo kuwa ni utafiti na ushauri.

"Wataalamu kutoka ZMA watashiriki katika programu za mafunzo katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji," alifafanua Prof. Mganilwa.

Mkurugenzi Mkuu wa ZMA, Mohamed, alisema NIT ni chuo bora kwenye utoaji wa mafunzo kwenye sekta ya usafiri na usafirishaji, hivyo makubaliano hayo waliyoingia yataleta matokeo chanya.

"Tumeona NIT ni chuo bora kabisa kwenye utoaji wa mafunzo katika maeneo yote ya usafirishaji hususani usafiri wa maji, reli, anga na barabara, hivyo katika makubaliano haya tutaweza kuwaleta wafanyakazi wetu kujiendeleza kimasomo hususani kwenye mafunzo ya kozi za marine.

"Vilevile, upande wetu, kupitia makubaliano haya tutaweza kuwapokea wanafunzi na wakufunzi kutoka NIT kwa ajili ya kupata mafunzo kwa njia ya vitendo.

"Tunatarajia kutumia fursa hii kikamilifu katika kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi wetu wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar," alisema.

Alibainisha kuwa makubaliano hayo yatadumu kwa kipindi cha miaka mitano ambapo wanafunzi na wakufunzi kutoka NIT watapata fursa ya kujifunza kwa vitendo katika mamlaka hiyo.

Alisisitiza kuwa kupitia makubaliano hayo, ana imani kuwa kwa miaka michache ijayo, taifa litakuwa na wataalamu wengi wabobezi kwenye eneo hilo.

Mkuu wa NIT alisema makubaliano hayo ni sehemu ya kutimiza malengo ya Mradi wa Kujenga Ujuzi kwa Maendeleo na Uingiliano wa Kikanda katika Afrika Mashariki (EASTRIP).

ZMA ilianzishwa chini ya Sheria Na. 3 ya Mwaka 2009 ya Baraza la Wawakilishi na kukabidhiwa jukumu la kufuatilia, kudhibiti na kuratibu shughuli za sekta ya bahari Zanzibar na kupewa majukumu ya kusimamia Sheria ya Usafiri wa Baharini Na. 5 ya Mwaka 2006.

## TEN/MET yataka ubora mazingira elimu jumuishi

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Elimu Tanzania (TEN/MET) umeomba serikali kuboresha mazingira ya upatikanaji wa elimu kwa watu wenye ulemavu ikiwamo kuongeza bajeti katika eneo la elimu jumuishi.

Kwa mujibu wa Mratibu Taifa wa TEN/MET, Ochola Wayoga, serikali inapaswa kuweka kipaumbele kwa kuboresha elimu jumuishi ili kundi la watu wenye ulemavu lipate haki ya elimu bora inayokidhi mahitaji yao bila kikwazo kama ilivyo kwa wanafunzi wa makundi mengine.

"TEN/MET bado tunasisitiza juhudi za pamoja na ushirikiano na wadau wote ikiwamo serikali, wadau wa maendeleo na asasi za kiraia, kuwekeza katika kuwajengea uwezo walimu katika uhakiki, utambuzi na tathmini ya watoto wenye ulemavu ili walimu wawezeshwe ujuzi na utaalamu wa kuandaa programu ya elimu inayokidhi mahitaji ya wanafunzi ikiwamo wenye ulemavu," alisema.

Katika taarifa ya mtandao huo kwa vyombo vya habari juzi, Wayoga alisema upo umuhimu wa kuongeza juhudi katika kufundisha lugha ya alama kwa wakufunzi wote wa kundi la wanafunzi wenye ulemavu pamoja na kuhakikisha vifaa vyote vya kujifunzia kulingana na mahitaji ya kundi hilo vinapatikana.

Alisema bado kuna umuhimu wa kupatikana kwa takwimu sahihi za watu wenye ulemavu, aina za ulemavu walionao, umri na jinsi katika ngazi ya taifa, mkoa na wilaya. Pia walitaka elimu bila malipo iendane na ubora wa elimu inaokidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu na kwamba elimu hiyo bila miundombinu na vifaa haisaidii.

"Utoaji wa elimu kwa wote lazima uungwe mkono na vifaa na miundombinu katika shule za msingi za serikali na za binafsi kwa kuhakikisha zinafuata viwango vya vifaa vinavyohitajika kusaidia ujifunzaji kwa wote," alisema.

Wayoga pia aliitaka serikali kutoa ruzuku ya matibabu, ukarabati na vifaa vinavyotumika kwa watu wenye ulemavu ili kuongeza upatikanaji wa huduma kwa kundi hilo. Alisema ni muhimu kwa serikali, sekta za umma na binafsi kutafuta suluhu za kiubunifu kwa ajili ya watu wenye ulemavu ili kuifanya dunia kutoa usawa kwa makundi yote.

"Watu wenye ulemavu duniani kote wanaendelea kukabiliwa na changamoto nyingi hususani katika upatikanaji wa elimu, kuna vikwazo vingi ambavyo mtoto mwenye ulemavu anavipitia anapopambana kutimiza ndoto zake za kielimu, imefika wakati vitafutiwe ufumbuzi.

"Kama wadau wa elimu, tunataka watoto wote bila kujali hali zao, wajifunze wapate haki sawa ya kujifunza kadri inavyowezekana, tunataka walimu watumie mbinu za kufundisha hasa ambazo zitasaidia watoto wenye ulemavu," aliwasilisha.

HABARI KITAIFA

## 'Msiwatenge waraibu wa dawa za kulevya'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Taasisi ya Organization Action of Youth Against Risk Behaviors (OYARB) ya Kibaha mkoani Pwani, Yohana Kilonzo, amesema familia zinazoishi na waraibu wa dawa za kulevya, zinapaswa kupewa elimu ili zisiwatenge.

Amesema kuwa familia hizo zinapaswa kuunganishwa na vituo vinavyoshughulika na kundi hilo ili zinufaike na huduma zinazotolewa.

Mwishoni mwa wiki, kiongozi huyo alitoa rai hiyo alipozungumza na Nipashe wakati wa hafla ya vijana 114 waliohitimu mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya mtandao yaliyotolewa na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha.

Kilonzo alisema zipo familia zinawatenga waraibu na kuwafanya wakose msaada hata wa kufika kwenye vituo vya afya kupata matibabu, jambo ambalo linaangamiza zaidi vijana hao.

"Zipo familia hazijakubaliana na wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya, hivyo inalazimu kituo chetu kubaki nao kwa uangalizi hadi pale tutakapojiridhisha kwamba wako vizuri, inahitajika kuwaelimisha wasiwatenge bali wawaunganishe kwenye vituo vinavyowahusu," alisema.

Kilonzo aliipongeza serikali pamoja na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha kwa kulikumbuka kundi la waraibu na kuwapatia mafunzo ya ufundi stadi ambayo yatawawezesha kujiajiri na kuondokana na utegemezi.

"Waraibu wengi wanaopata matibabu katika kituo kilichoko Hospitali ya Rufani Tumbi wanakabiliwa na kikwazo cha uchumi, wapo wanaolazimika kutembea umbali mrefu kwenda hospitalini, tunaendelea kupambana na hali hii kuwasaidia wamalize matibabu lakini familia pia hazitakiwi kuwaacha peke yao kwa kuwa wameamua kuachana na kutumia dawa za kulevya," alisema.

Alibainisha kuwa taasisi yake inatoa huduma kwa waraibu 364 ambao wanapewa elimu ya mabadiliko, elimu ya ujasiriamali, uraia mwema na kuwaunganisha na familia pamoja na Hospitali ya Rufani ya Tumbi ili kupatiwa tiba ya methadone.

Mohamed Mazana, mmoja wa walionufaika na mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya mtandao, aliahidi kwenda kuyafanyia kazi kwa kujiajiri, akikishukuru chuo hicho kwa kulikumbuka kundi hilo.

# HKMU: Serikali iongeze mikopo, ufadhili wanafunzi kada ya afya

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) kimeiomba serikali kuendelea kuongeza mikopo na ufadhili kwa wanafunzi wa fani za afya ili kupunguza uhaba wa watumishi katika sekta hiyo nchini.

Mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Baraza la chuo hicho, John Ulanga alitoa rai hiyo wakati wa mahafali ya 20 yaliyofanyika kwenye viwanja vya chuo hicho, wahitimu 294 wakitunukiwa vyeti mbalimbali.

Katika mahafali hayo, wahitimu 180 walitunukiwa Shahada ya Udaktari wa Binadamu, 38 Shahada ya Uuguzi, 54 Stashahada ya Uuguzi, 10 Stashahada ya Ustawi wa Jamii na 10 Shahada ya Uzamili ya Udaktari wa Binadamu katika Tiba na Afya ya Watoto.

Wakati wa mahafali hayo, pia kulikuwa na mhitimu mwanaume aliyetunukiwa Shahada ya Uzamili ya Upasuaji na mhitimu mwanamke aliyetunukiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Afya ya Jamii.

Ulanga alisema HKMU imetoa mchango mkubwa tangu kuanzishwa kwake kwa kutoa wataalamu wa afya wa kada mbalimbali wakiwamo madaktari bingwa wanaofanyakazi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wahitimu wa chuo hicho pia walionyesha umahiri mkubwa kwenye kusanyiko la wanataaluma kwa namna ambavyo walimudu kuwasilisha mada zao kwa utaalamu wa hali ya juu, hivyo kuonyesha kuwa wamepikwa vya kutosha.

"Juzi wakati ninasikiliza ubora na umahiri wa mawasilisho yao kwenye kusanyiko la wahitimu, nilijiuliza hivi serikali haiwezi kutoa ruzuku kwenye vyuo kama HKMU kutuwezesha kuongeza idadi ya wataalamu tunaozalisha na pia kuongeza idadi ya utafiti unaofanyika? Tunaomba Mkuu wa Chuo utupigie debe tupate ruzuku serikalini kuendesha chuo," alisema Ulanga.

Aliishukuru serikali kwa kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa chuo hicho na wa vyuo vingine kwa kuwa mikopo hiyo inawawezesha wanafunzi kutoka kaya maskini kupata elimu na kuondokana na maisha duni.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao wa Elimu ya Afya (KHEN), Kokushubira Kairuki, alisema sababu kubwa iliyoisukuma KHEN kuwekeza kwenye elimu ya juu, hasa afya, ni uhaba wa watumishi kwenye sekta hiyo nchini.

"Katika mahafali yetu ya kwanza mwaka 2003 wahitimu walikuwa 63 wakiwamo madaktari wanne na wengine wakiwa wauguzi lakini leo hii katika mahafali haya ya 20 tuna wahitimu 294 na idadi hii inafikisha jumla ya wahitimu 3,186, miongoni mwao wakiwa ni madaktari wa binadamu 1,560," alisema.

Kiongozi huyo alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) linapendekeza uwiano wa daktari mmoja kwa wagonjwa 8,000 na kwamba uwiano kwa Tanzania bado hauridhishi kwa kuwa daktari mmoja anatoa huduma kwa wagonjwa 20,000 kwa mwaka.

"Ingawa mahitaji bado ni makubwa, tunamshukuru Mungu kwamba tumeweza kuendelea kutoa mchango wetu kwa taifa katika kupunguza uhaba wa rasilimali watu katika sekta ya afya mwaka hadi mwaka kwa miaka 25 mfululizo," alisema.

Mkuu wa chuo hicho, Anne Makinda alisema chuo hicho tangu kuanzishwa kwake, kimekuwa kikitoa wahitimu bora wenye weledi wa hali ya juu ambao wanafanya kazi kwenye maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

"Juzi tulikuwa na kusanyiko la kitaaluma, walikuja waliowahi kusoma HKMU kwa kweli ukiwasiliza wanavyowasilisha mada zao wanavyojiamini unapata uhakika kabisa kwamba hapa ni sehemu sahihi ya kufundisha watumishi wa kada ya afya," alisema.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Yohana Mashalla aliiomba serikali ipunguze gharama za vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili wanafunzi wengi zaidi wasome kwa njia ya mtandao.

Prof. Mashalla pia aliiomba serikali kuvipa ruzuku kwa vyuo vikuu binafsi ili vijiandae kwa kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu, kusomesha wahadhiri na ununuzi wa vifaa vya kufundishia, maabara na maktaba ili kukidhi mahitaji elimu ya juu nchini.

Alisema katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa wahadhiri, HKMU imeendelea kufadhili masomo ya wahadhiri katika ngazi ya uzamili na uzamivu ndani na nje ya nchi.



Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango (wa pili kulia), akimkabidhi kikombe cha ushindi wa nafasi ya utoaji fursa kwa wazawa Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Kampuni ya Bia Serengeti (SBL), Conrad Msoma, tuzo zilizoandaliwa na ATE, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Kushoto) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako.. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya Stanbic yatoa msaada wa madawati

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya Stanbic Tanzania imetoa msaada wa madawati 140 yenye thamani ya Sh. milioni 19.6 kwa Shule ya Sekondari Kerege wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

Vilevile, benki hiyo imekabidhi miche ya miti 140 ili ipandwe katika shule hiyo kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mkuu wa TEHAMA na Operesheni za Benki ya Stanbic, Mussa Ally, alibainisha hayo jana wilayani humo wakati akikabidhi msaada huo.

Alisema msaada huo ni katika kuiunga mkono serikali kutatua kero za sekta ya elimu kwenye mikoa mbalimbali nchini kwa kuchangia katika kuboresha mazingira ya kujifunzia wanafunzi.

"Tuna nia kubwa na kampeni yetu ya Stanbic Madawati Imitative ambayo hadi sasa imechangia takribani madawati 1,000 kwa shule mbalimbali nchini tangu ilipozinduliwa.

"Mchango huu leo (jana) ni mwendelezo wa jitihada zetu za kuitikia wito wa serikali wa kuchangia madawati kwa lengo la kumaliza kabisa uhaba wa madawati shuleni.

"Kupitia mchango huu, Benki ya Stanbic inachochea uundaji wa nguvukazi ya baadaye ya nchi. Tutaendelea kujitolea kusaidia sekta ya elimu sio tu hapa Wilaya ya Bagamoyo, bali Tanzania nzima," alisema.

Diwani wa Kerege, Saidi Ngatipura aliipongeza Benki ya Stanbic kwa jitihada zake katika kuendelea kusaidia sekta ya elimu na kuwaomba wadau wengine kuunga mkono shule nyingine wilayani humo.

Akipokea msaada huo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kerege, Kasika Mateko alisema kuwa kupitia msaada huo, wanafunzi wa shule hiyo watakuwa na mazingira bora ya kujifunzia, jambo ambalo anatarajia litaongeza ufaulu wao.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi wakuu wa wilaya na serikali za mitaa kutoka Wilaya ya Bagamoyo.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka huu, pamoja na mambo mengine, inabainisha kuwapo uhaba wa madawati katika shule za msingi zilizoko kwenye halmashauri 77 alizozikagua.

# Samia afuta sherehe miaka 61 ya Uhuru

## • Mamilioni yake kutumika ujenzi mabweni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amefuta sherehe za maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara huku akiagiza fedha zote zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya sherehe hizo Sh. milioni 960 zitumike kujenga mabweni katika shule nane za msingi za wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Pia ameagiza maadhimisho ya sherehe hizo mwaka huu kufanyika kwa midahalo na makongamano mbalimbali katika wilaya zote nchini ili wananchi wajadili, kutafakari kwa pamoja na kukumbuka walikotoka, walipo na wanakoelekea.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alitangaza hayo jana jijini hapo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya sherehe za miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara mwaka huu.

"Ninaomba kutumia fursa hii kwa namna ya kipekee sana kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo ameamua kuwa fedha zote Sh. milioni 960 zilizokuwa zimetengwa na wizara na taasisi kwa ajili ya maadhimisho ya sherehe za uhuru mwaka huu zipelekwe Ofisi ya Rais - TAMISEMI na zitatumika kujenga mabweni katika shule nane za msingi za wanafunzi wenye mahitaji maalum nchini," alisema.

Waziri Simbachawene alisema uamuzi huo ni dhamira ya dhati ya Rais Samia ya kuwajali na kuwajengea mazingira rafiki watu wenye mahitaji maalum nchini.

"Hili ni jambo kubwa la kishujaa na la kupongezwa sana na wananchi wote wa Watanzania," alisema Simbachawene.

Alizitaja shule ambazo zitanufaika na fedha hizo ni Buhangija ya mkoani Shinyanga, Goweko ya Tabora, Darajani ya Singida, Mtamba ya Tanga, Nsanzi ya Rukwa, Idofi ya Njombe, Longido ya Arusha na Songambele ya Manyara.

Akizungumzia kuhusu midahalo na makongamano yatakayotumika kujadili na kutafakari hatua ambazo nchi imefikia, Simbachawene alisema yatatanguliwa na ratiba mbalimbali kwa viongozi wa mikoa na wilaya kufanya shughuli za kijamii kama vile usafi katika maeneo ya hospitali, shule, nyumba za wazee na makundi yenye mahitaji maalum.

"Hivyo, sherehe za mwaka huu hakutokuwa na gwaride na shughuli nyingine za kitaifa. Kwa muktadha huu, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameniagiza nishirikiane na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI kufanya usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya midahalo na makongamano hayo ili kujiridhisha na matokeo yake," alisema Simbachawene.

Vilevile, waziri huyo alisema katika kutekeleza maelekezo hayo ofisi hizo zimetoa maelekezo mahsusi na ratiba kwa ajili ya kurahisisha uendeshaji mzuri wa shughuli kwa mikoa na wilaya zote nchini.

"Katika kukuza uzalendo na kusherehekea maadhimisho haya pamoja na maadhimisho mengine ya kitaifa kama vile sherehe za muungano, ofisi zote za serikali zipambwe kwa mapambo ya rangi za Bendera ya Taifa pamoja na picha ya Rais wetu," aliagiza.

"Ninaomba kutumia fursa hii kuwahamasisha wananchi wote kushiriki ipasavyo katika midahalo na makongamano katika wilaya zao na kujadili kwa kina kuhusu maendeleo endelevu katika miaka 61 ya uhuru wetu," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi (katikati), Edda Sauwa (kushoto) na Faraja Nassary wakishikiria tuzo baada ya kutangazwa kuwa washindi katika hafla ya utoaji tuzo kwa waajiri bora mwaka 2022 zilizoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka majengo ya ghorofa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameziagiza halmashauri zote mkoani hapo kuanza kufikiria kujenga shule za ghorofa ili kuokoa maeneo ya ardhi ambayo yangeweza kutumika kwa shughuli nyingine za maendeleo.

Aliagiza hayo juzi alipokagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Halmashauri za Wilaya za Singida Vijijini, Ikungi na Manispaa ya Singida.

Alisema kwa kuwa miji inapanuka kwa kasi na ardhi inakuwa finyu, ni muhimu kuanza kujenga majengo ya ghorofa ili kupunguza matumizi ya ardhi.

Pia alizipongeza Halmashauri za Singida, Ikungi na Manispaa kwa kazi nzuri ya usimamizi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa ambao umefikia asilimia zaidi ya 80.

Awali akiwa katika Wilaya ya Singida, Serukamba alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Ester Chaula kutumia fedha za ndani kuongeza baadhi ya vyumba vya madarasa badala ya kusubiri zinazotolewa na serikali.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Singida Vijijini, Chaula alisema halmashauri yake ilipokea Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 50 katika shule 17 za sekondari.

Alisema kuwa baada ya kupokea fedha hizo, ziliwekwa katika akaunti 17 za shule hizo na kwa sasa shule hizo zipo katika hatua ya umaliziaji.

Aliongeza kuwa hadi sasa Sh. milioni 581.49 zimeshatumika katika utekelezaji wa ujenzi wa madarasa hayo ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 85 na wameahidi kukamilisha mpaka uwekaji wa madawati kabla ya Desemba 15 mwaka huu.

Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu alisema manispaa imepokea Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 50 vya madarasa ya wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Alisema vyumba vinane vipo katika hatua ya upakaji wa rangi, vyumba 26 vipo hatua ya maandalizi ya kupaka rangi (skimming) wakati vyumba 14 vikiwa katika hatua ya kupiga ripu na viwili katika hatua ya upasuaji.

Kaimu Mkurugenzi wa Ikungi, Faraja Maluga, alisema halmashauri hiyo imepokea Sh. milioni 580 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 29 katika shule 16.

Mkurugenzi huyo alisema madarasa hayo yote yamefikia asilimia 80 ya ujenzi na wanategemea kukabidhi kwa muda uliyopangwa.

Mkoa wa Singida umepewa Sh. bilioni 5.8 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 290 ili kupokea wanafunzi wote waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwakani katika halmashauri saba za mkoa huo.

# Idadi wanafunzi wagunduzi kisayansi yaongezeka YST

**Na Elizabeth Zaya**

IDADI ya wanafunzi waliowasilisha maombi ya kufanya kazi za ugunduzi za kisayansi ambazo huratibiwa na Shirika la Wanasayansi Chipukizi (YST), imeongezeka kutoka 579 mwaka jana hadi kufikia 1,143 mwaka huu.

Kazi hizo za ugunduzi hufanywa na wanafunzi kutoka shule mbalimbali za Tanzania Bara na Zanzibar ambazo hushindanishwa na washindi kupewa zawadi za fedha taslimu, medali na kufadhiliwa masomo ya vyuo vikuu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, Mwanzilishi mwenza wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha, alisema kati ya kazi hizo zilizowasilishwa, 530 zimepatiwa usaidizi kwa kuwapatia mafunzo ya namna ya kuziboresha na tayari 380 zimekamilika.

Alisema kazi hizo za ugunduzi ambazo zimefanywa na wanafunzi, zinatarajiwa kuonyeshwa katika maonyesho ya Desemba 8 mwaka huu na zimejikita katika masuala ya njia salama za utunzaji mazao ya kilimo, mazingira, matumizi endelevu ya rasilimali maji, dawa za asili na uboreshaji afya za binadamu.

Maeneo mengine ambayo yameguswa ni upatikanaji na uzalishaji wa nishati ya umeme, matumizi ya muziki katika ufundishaji wa somo la hesabu shuleni, matumizi ya mimea ya asili katika kuboresha uzalishaji wa maziwa ya ng`ombe na kutatua tatizo la udumavu wa kuku.

"Kazi zote hizi zimejikita katika kupata njia za kutatua matatizo ya kimaendeleo kwenye jamii na zitaonyeshwa katika maonyesho ya kitaifa ya YST Desemba 8, mwaka huu.

"Kazi kubwa ambayo tunaendelea kusisitiza ni kuziomba kampuni na wenye viwanda kuwatumia vijana hawa katika kazi za kisayansi kwenye viwanda vyao," alisema Dk. Kamugisha.

Ofisa Mtendaji wa Shirika la Karimjee Jivanjee Foundation ambao ni wadhamini wakuu wa maonyesho hayo, Caren Rowland alisema mpaka mwaka jana shirika hilo lilikuwa limewadhamini wanafunzi 37 kwenda vyuo vikuu na mwaka huu wanadhamini wengine wanne wanaoshinda katika maonyesho hayo ya YST kwenda kusoma katika vyuo mbalimbali vya elimu ya juu masuala ya sayansi.

Rowland alisema shirika hilo limepanga kuendelea kutoa udhamini kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika maonyesho hayo na lengo ni kujenga msingi kwa wanafunzi hao kuwa na ari ya kitaaluma na kupenda masomo ya sayansi pamoja na kuongeza idadi ya wanasayansi na wabunifu nchini.



## Waziri Ummy ampigia debe mgombea udiwani Mnyanjani

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amempigia 'debe' mgombea udiwani wa Kata ya Mnyanjani (CCM), Simba Kayaga, akiwasihi wakazi wa eneo hilo wamwonyeshe upendo, Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kumchagua kada huyo.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetangaza kuwa uchaguzi mdogo wa udiwani katika kata 12 za Tanzania Bara, utafanyika Desemba 17 mwaka huu.

Akizungumza jana katika mkutano wa uzinduzi wa kampeni za udiwani za CCM, Ummy ambaye ni Mbunge wa Tanga, alisema endapo wananchi watamchagua Kayaga watakuwa wamemtia moyo Rais Samia na kuendelea kuukumbuka Mkoa wa Tanga.

"Watu wa Tanga, mwaka 2025 tunakwenda na Rais Samia Suluhu Hassan. Na kwa kuanza tunawatumia salamu wale jamaa zetu, Desemba 17, mwaka huu, kwa kumchagua kijana Kayaga ili kumtengenezea barabara Samia."

Uchaguzi huo unafanyika ili kuziba nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa Diwani wa Kata hiyo, Yakub Nuru ambaye alifariki dunia.

Baada ya kuzinduliwa kampeni hizo mgombea udiwani wa CCM, Simba Kayaga, alisema kata hiyo ina barabara 88 zilizoko kwenye mitaa saba na kwamba iwapo atachaguliwa atahakikisha zinapitika kwa urahisi.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Tanga, Meja Mstaafu Hamisi Mkoba, akizungumza katika mkutano huo, alisema Simba Kayaga, anafaa kuwa diwani.

Kata nyingine zinazofanya uchaguzi mdogo wa marudio ni Majohe (Dar es Salaam CC), Mndumbwe (Tandahimba), Njombe Mjini, Dunda (Bagamoyo), Mwamalili (Shinyanga) na Vibaoni (Handeni).

# Tatizo udumavu kwa watoto Manyara lapatiwa ufumbuzi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TATIZO la udumavu wa watoto linaloutesa Mkoa wa Manyara limewaamsha usingizini viongozi wa mkoa huo pamoja na serikali baada ya kutangaza kuja na mkakati mahususi wa kuzalisha vyakula lishe, kama sehemu ya mapambano dhidi ya utapiamlo kuanzia ngazi ya kaya.

Kaimu Katibu Tawala Msaidizi, Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara, anayeshughulikia uchumi, kilimo na uzalishaji, Samweli Dahaye, alisema mpango huo utasaidia kuepuka madhara yanayoendelea kujitokeza kutokana na kutozingatia lishe bora kwa usahihi.

Dahaye alikuwa akizungumza jana na wadau wa lishe wakati wa kikao kazi cha kamati za lishe za mkoa huo.

"Msimu ujao wa kilimo tumepanga kulima hekta 104 za zao la maboga ili kuzalisha tani 1,294. Mahindi lishe tutalima hekta 338,996 ili kuzalisha tani 848,098, kati ya hizo hekta 200 hadi 350, zitalimwa mahindi ya njano ambayo ni ya lishe," alisema. Alisema kuhusu uhamasishaji wa alizeti wameweka lengo la kulima hekta 181,290 ili kuzalisha tani 261,712.

Dahaye alisema katika maharage wanakusudia kulima hekta 117,114 ili wazalishe tani 144,438 na mbaazi watalima hekta 72,727 ili kuvuna tani 69,659.

Wilaya za Hanan'g, Mbulu na Babati ndizo zinazozalisha kwa wingi maboga huku wakikosa elimu ya kuzalisha mbegu bora kwa ajili ya misimu mingine.

Katika kikao kazi hicho, Katibu Tawala Msaidizi, Uratibu na Mipango wa Mkoa huo, Maarufu Mkwaya, aliagiza wataalamu wa kilimo, lishe na elimu kushirikiana kutoa elimu namna ya kutumia mbegu za maboga na viazi lishe ili kutokomeza udumavu.

Ofisa Lishe wa Mkoa wa Manyara, Mabula Masunga, alisema ataendelea kusimamia utekelezaji wa mkataba wa lishe ambao ulisainiwa na Rais Samia Suluhu Hassan na wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya ili kusaidia kutoa afua za lishe.




Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Civil Social Protection Foundation (CSP), Nemency Iriya, akizungumza kwenye uzinduzi wa mradi wa Tanzanite na uchumi imara wa mwanamke unaohusisha kata tatu za Mirerani, Endiamtu na Naisinyai wilayani Simanjiro mkoani Manyara jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Benki ya CRDB yatekeleza agizo la Rais Samia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HATIMAYE Benki ya CRDB, imeitikia wito wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuitaka ijikite kuwawezesha wadau wa sekta ya utalii nchini ili waboreshe huduma zao kwa wageni wanaokuja nchini kutembelea vivutio na hifadhi za taifa.

Kutokana na wito huo, Benki ya CRDB imetoa mkopo wa Sh. bilioni 139 kwa wadau wa sekta ya utalii.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Kadi wa CRDB, Farid Seif, akizungumza jana katika semina ya wadau wa utalii, alisema mkopo huo utaiinua sekta hiyo hasa baada ya Rais Samia, kutengeneza na kuzindua filamu ya kutangaza vivutio na utalii ya 'The Royal Tour' ndani na nje ya Tanzania.

"Lengo la kikao hiki pia ni kuwapatia fursa wadau kuona jinsi gani watalii wanaweza kulipa kupitia mifumo ya kidigitali na kurahisisha huduma.


"CRDB imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na sekta ya utalii ili kuhakikisha tunazidi kuboresha utalii na kuongeza mapato ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alisema sekta ya utalii ina umuhimu mkubwa katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla katika nchi mbalimbali, ikiwamo Tanzania na inaongoza kwa kuingiza fedha nyingi za kigeni nchini.

Alisema kuwa mchango wa sekta ya utalii katika kipindi cha janga la ugonjwa wa corona pato la taifa lilishuka kwa asilimia kubwa na baada ya Rais Samia kuchukua hatua mbalimbali mchango wa sekta ya utalii katika uchumi uliongezeka hadi asilimia sita.

"Napenda kuipongeza sana Benki ya CRDB, kwa kuwa ndiyo ilikuwa benki ya kwanza kuonyesha nia yake ya dhati ya kukuza utalii, kwa kuja na aina mbalimbali za kupokea malipo kwa njia ya kielektroniki katika sekta ya utalii, ambayo imerahisisha utoaji huduma kwa watalii," alisema.

Mmoja wa wadau wa utalii, Mmiliki wa Hoteli ya Utalii ya Masai Land, Dk.Charles Bekon, alisema semina hiyo imewajengea uelewa mkubwa na wamewasilisha matatizo yao.





# Waziri Mkuu aagiza mchakato kutwaa mashamba kuharakishwa

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza kuanza haraka kwa mchakato wa kutwaa mashamba makubwa ya mkonge, ambayo hayajaendelezwa ili yagawiwe kwa wakulima wadogo.

Akizungumza jana jijini Tanga wakati wa mkutano wa tatu wa wadau wa mkonge nchini, Majaliwa alisema uamuzi wa kuyarejesha serikalini mashamba hayo unalenga kutimiza malengo ya kitaifa ya kuzalisha tani 120,000 za mkonge ifikapo mwaka 2025.

Katika mkutano huo Waziri Mkuu Majaliwa hotuba yake ilisomwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Athony Mavunde.

"TSB (Bodi ya Mkonge nchini), chukueni mashamba yote makubwa ambayo hayaendelezi kilimo cha mkonge, muwagawie hawa wakulima wadogo ili uzalishaji uendelee na hatimaye malengo ya serikali yatimie.

"Tayari serikali ilishatangaza zao hili ni la kimkakati, hivyo ni lazima kutimiza malengo iliyojiwekea kwa wakati uliopangwa."

Mwaka jana Waziri Mkuu Majaliwa aliziagiza halmashauri zinazolima mkonge nchini pamoja na wakulima wakubwa wa mkonge kutenga ekari 10 kwa ajili ya kuanzisha vitalu vya kuzalisha miche ya mkonge ili kupunguza tatizo la upungufu wa mbegu.

Kuhusu uhaba wa mashine za kuchakata mkonge (korona), Waziri Mkuu Majaliwa, alisema serikali iko katika mchakato wa kutoa mashine tatu, ambazo zitatumika kwa ajili ya wakulima wadogo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Mariam Mkumbi, alisema mipango ya sasa ya serikali ni kuongeza uzalishaji wa zao hilo katika mashamba makubwa na wakulima wadogo ifikapo mwaka 2025/2026.

"Tunataka tuvuke hapa kwa sababu wakulima wadogo, kwa sasa wanazalisha tani 17,000 kwa mwaka, wataongeza uzalishaji wao hadi kufikia wastani wa tani 60,000. Na wakulima wakubwa watazalisha tani 60,000 kutoka tani 28,000 wanazozalisha sasa kwa mwaka," alieleza Mkumbi.

Alisema TSB katika kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwa sekta ya mkonge nchini inafikia lengo la kuzalisha tani 120,000 ifikapo mwaka 2025, inaiomba Wizara ya Kilimo, kurejeshewa mashamba yote ya mkonge.

"Tunaiomba serikali irudishe kwa bodi mashamba yote yaliyohamishiwa chini ya halmashauri za wilaya na yale yaliyotelekezwa bila kuendelezwa ili iweze kuyagawa kwa wakulima wadogo na wa kati wa mkonge", "Lakini kuwezesha bodi kupata mitambo ya uzalishaji kwa baadhi ya wakulima waliohamasika kulima mkonge ambao wanakaribia kuvuna," alibainisha.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, alisema asilimia 90 ya wakulima mkoani humo, wanazalisha mkonge kwa zaidi ya asilimia 50 huku Wilaya ya Korogwe ikiwa kinara katika uzalishaji.



Kamanda wa Polisi Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Hadija Sokolo (wa tatu kulia), akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya udereva kati ya washiriki 71 wanaoendesha vyombo vya moto wilayani humo, baada ya kufunga mafunzo hayo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Kilio wakulima wa mkonge chatua kwa Waziri Mkuu

**Na Oscar Assenga,** TANGA

KILIO cha wakulima wa mkonge mkoani Tanga kuhusu wanyama aina ya tembo kuingia katika mashamba yao na makazi na kusababisha vifo na uharibifu wa mali kimetua kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, imekuwa ikiripoti mara kwa mara matukio ya uvamizi wa wanyama hao katika mashamba na makazi.

Jana Mbunge wa Mkinga (CCM), Dastan Kitandula, akizungumza katika mkutano wa tatu wa wadau wa sekta ya mkonge nchini, alimuomba Waziri Mkuu Majaliwa, kuingilia kati tatizo hilo kwa kuwa linarudisha nyuma juhudi za wakulima wadogo ikiwamo kuwakatisha tamaa ya kuendelea kuzalisha zao hilo la kibiashara.

Katika mkutano huo, Waziri Mkuu Majaliwa, aliwakilishwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde.

"Pamoja na serikali kuweka msukumo kwa wakulima wadogo kujiingiza kwenye kulima zao hili tofauti na ilivyokuwa zamani. Sasa tatizo la uvamizi wa tembo kwenye mashamba ya mkonge, linawashusha ari wakulima.

"Hili tatizo inabidi serikali ilichukulie kwa umuhimu mkubwa ili lisiwakatishe tamaa wakulima wa mkonge."

Hivi karibuni, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alinukuliwa akisema amearifiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, kwamba tayari hatua za kudhibiti tatizo hilo zimeanza kuchukuliwa katika baadhi ya mikoa, ikiwa ni pamoja na kujengwa kwa mabanda ya ulinzi maeneo yote yenye tatizo la tembo na kupelekwa askari wa wanyamapori.

Kwa mujibu wa Chongolo, baada ya askari hao kupelekwa katika maeneo hayo, watapima ufanisi wao ndani ya kipindi kifupi ili kuona kama njia hiyo ni sahihi katika kudhibiti wanyama hao au zitafutwe njia nyingine kuwakabili.

# Askofu ampa kongole Samia kuisaidia shule kupata umeme

**Na Anjela Mhando,** SAME

ASKOFU wa Kanisa la Free Pentecostal Church's of Tanzania (FPTC), Dk. Stephen Mshomi, amempa 'kongole' Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Shule ya Sekondari ya New Dawn, inayohudumia yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu kuondokana na adha ya kukosa nishati ya umeme.

Shule hiyo Taasisi ya New Dawn Communities International iliyoko chini ya Kanisa la FPTC.

Akizungumza jana katika Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, wakati wa mahafali ya kwanza ya kidato cha nne ya shule hiyo, Askofu Mshomi, alisema shule hiyo ilikuwa ikikabiliwa na tatizo hilo kwa muda mrefu sasa hali ambayo ilikuwa ikitishia mustakabali wa shule hiyo kitaaluma.

"Tunamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kujibu ombi letu tuliloliwasilisha kwake kupitia kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuitupia jicho shule hii.

"Tumeshapata umeme shuleni hapa, jambo ambalo limesaidia ufanisi wa wanafunzi shuleni na walimu wanaofundisha wanafunzi hawa," alisema Dk. Mshomi.

Katika mahafali hayo ya kwanza wanafunzi 33 walihitimu mahafali hayo ya kwanza ya kidato cha nne.

Rais wa New Dawn America, Ron Sukut, alisema shule hiyo na miradi mingine inayotarajiwa kutekelezwa kuanzia sasa, inalenga kuchangia jamii kuboresha maisha yao.

"Unapotengeneza vijana wa leo wanakuja kuwa wazazi na viongozi bora kwa wakati ujao. Usalama wa taifa lijalo, unahitaji vijana waliolelewa vyema ikiwamo kupata elimu na malezi bora," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward, aliupongeza uongozi wa shule hiyo kwa kuanzisha kituo hicho ambacho kimeleta mabadiliko makubwa katika jamii wilayani humo.

Nipashe
TESA
Jumanne Desemba 6, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




**Kilivyowatisha wadau wa elimu wataja chanzo ni ukosefu maadili, adhabu ndogo**




**Ilivyofungua dunia kwa wasichana kurudi kwa kasi madarasani**




Kukosa vyoo shuleni kulitafakarishe taifa baada ya miaka 61 ya Uhuru

ELIMU
**NA ABATO KASIKA**

MIAKA 61 YA UHURU

# Kiboko kiwepo au kiondolewe shuleni?

• Walimu waambiwa ni ruksa 'kutandika' ila kwa maelekezo

MIAKA 61 ya Uhuru wa Tanganyika, wapo baadhi ya wanafunzi wanaokimbia shule kwa kuogopa fimbo. Hofu ya kuchapwa inawafanya watoto kuogopa kukutana na mwalimu, kwenda shule na hata wengine wakitoroka na kushinda vichakani ili wasikutane na mwalimu.

Hata leo taifa linaendelea kutafakari kuendelea au kutoendelea na adhabu ya viboko shuleni, mjadala wa kuchapa au kufuta adhabu ya viboko shuleni umekuwa ukiibuka mara kwa mara, kutokana na kuripotiwa matukio ya baadhi ya walimu kuwatandika wanafunzi hadi kufariki dunia, kuwapa ulemavu au kuwaumiza.

Januari 31, mwaka 2019, mkutano wa 14 wa bunge la 11, katika kipindi cha maswali na majibu, miongoni mwa mambo yaliyoleta mjadala mkubwa ni swali la Mbunge wa Viti Maalum CCM, Zainab Katimba, akihoji kama kuna utafiti uliofanyika kubaini kama adhabu ya viboko inaongeza ufaulu.

Hoja yake hiyo ilikuwa ni mwendelezo wa mjadala wa kuwapo au kuondoa viboko shuleni.

Hadi sasa suala la kuwapo au kuondolewa viboko shuleni limejadiliwa na wadau mbalimbali wakiwamo wanaotetea haki za binadamu ambao wamekuwa wakitamani ifutwe.

### KUCHAPA RUKSA

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anakoleza moto anapoiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuusambaza waraka wa adhabu za viboko shuleni wa mwaka 2002, ili walimu na wanafunzi wauelewe na kuuzingatia.

Anasema hayo katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Haki za Watoto, yanayofanyika jijini Dar es Salaam wiki iliyopita na kufafanua kuwa ukatili kwa watoto unaendana na kuudhuru miili yao ikiwa ni pamoja na vipigo ikijumuisha adhabu ya viboko vilivyopitiliza na kusababisha madhara.

"Hivyo viboko vilivyopitiliza ni ukatili kwa watoto kwani tunao waraka namba 24 wa mwaka 2002 unaosimamia adhabu za viboko shuleni, ambao unasema wazi ni nani mwenye mamlaka ya kutoa adhabu hiyo na viboko vingapi vinaruhusiwa na kwa utaratibu upi," anakumbusha Dk. Dorothy.

Waziri Dorothy anasema Waraka Namba 24 wa Elimu unaeleza kuwa mwenye mamlaka ya kutoa adhabu ya kuchapa viboko ni mwalimu mkuu wa shule au mwingine atakayeteuliwa naye kwa maandishi, kila mara kosa linalostahili adhabu hiyo linapotendeka.

Pia waraka huo unaonya na kuelekeza kuwa mwanafunzi wa kike anapaswa kupewa adhabu ya viboko na mwalimu wa kike ndiye anayemwadhibu kama shule haina walimu wanawake wa kiume anaweza kuwaadhibu.

"Waraka unaweka wazi kuwa kila mara adhabu ya viboko inapotolewa sharti iorodheshwe katika kitabu kilichotengwa kwa kusudi hilo, la kujaza taarifa zihusuzo kutandika wanafunzi fimbo na sababu za kutoa viboko." Anasema Waziri.

Anafafanua kuwa, hatua hiyo inakwenda pamoja na kuandika jina la mwanafunzi aliyeadhibiwa, kosa alilotenda, idadi ya viboko alivyochapwa, na jina la mwalimu aliyetoa adhabu hiyo.

"Kwa kuwa waraka unamtambua mwalimu mkuu kama mtu mwenye mamlaka ya kutoa adhabu ya viboko, basi unamtaka pia atie saini katika kitabu hicho maalum kila adhabu ya viboko inapotolewa," anasema.


Adhabu kali kwa wanafunzi kunapunguza hamu ya kupenda shule. **PICHA: MAKTABA**

Aidha, Waziri anaongeza kuwa iwapo mwanafunzi atakataa kupewa adhabu ya viboko, sharti asimamishwe shule kwanza, ili kupisha hatua nyingine za kinidhamu dhidi ya kosa lake.

"Waraka pia unawaonya walimu kuwa hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya yeyote atakayekiuka utaratibu ulioidhinisha na waraka huo, na kwamba ni marufuku kwa mwalimu yeyote kuonekana na fimbo mkononi kwa lengo la kumuadhibu mwanafunzi," anasema Waziri.

### VILIPO VIKWAZO

Waziri Dorothy anaongeza kuwa pamoja na kuwapo kwa waraka huo, tatizo ni usimamizi wa utekelezaji wake, na kwamba baadhi ya walimu hawaufuati wanapotoa adhabu na kuwataka wabadilike.

"Vinginevyo wanaoendelea kutozingatia waraka, sitamwaacha mwalimu mmoja asishtakiwe kwa sheria ya mtoto iwapo atatoa adhabu hiyo nje ya maelekezo ya waraka. Sitamwacha," anasisitiza.

Mbali na hilo, anawahakikishia watoto kwamba timu ya serikali, wadau na jamii watakutana kuona namna nzuri ya kushughulikia hoja ya viboko kwa kuzingatia maadili na tamaduni katika malezi.

"Inasikitisha kuona baadhi

INAENDELEA UK.20

ELIMU

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

MIAKA 61 UHURU

# Ilivyofungua dunia kwa wasichana kurudi kwa kasi madarasani

• Ni 'stop' wanaokariri madarasa, wanafunzi waanza tena 'kupasi'

IJUMAA Desemba 9 ni mwaka wa 61 wa Uhuru wa Tanganyika, ambao una mengi ya kukumbuka, kushangiliwa na kuweka mipango zaidi ya kusongambele ili kuwa na taifa bora zaidi.

Baada ya Uhuru mwaka 1961 Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alibainisha ujinga, umaskini na maradhi kuwa maadui watatu wa taifa na kueleza kuwa ili kuwamaliza maadui wengine wa kwanza wa kupambana naye ni ujinga.

Ukawa mwanzo wa juhudi za kufikisha elimu kwa kila Mtanzania, haikuwa kazi rahisi kujenga, shule za msingi, sekondari, vyuo kuanzia vya maendeleo ya jamii, ualimu, ufundi, kilimo, mifugo, reli, nyuki hadi vikuu.


Azimio la Musoma la mwaka 1974 ndilo lililotia mkazo kuondokana na adui ujinga Watanzania wengi walisoma na kumaliza darasa la saba kupitia jitihada hizo zilizoweka mkazo kwenye elimu ya msingi kwa wote, kufanya kazi kabla ya kujiunga na chuo kikuu baada ya kuhitimu kidato cha sita, lakini wasichana waliruhusiwa kujiunga vyuo vikuu moja kwa moja, baada ya mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Elimu ililenga kumkomboa Mtanzania kifikra na ilimaanisha kujifunza na kuthamini kazi, kwa hiyo dhana ya Uhuru na Kazi ilikuwa sehemu ya mafunzo katika kila kulipokuwa na darasa kuanzia msingi, sekondari, vituo vya elimu ya watu wazima na vyuoni, Nyerere akisisitiza elimu kwa wote bila kujali rika hata ngumbaru au watu wazima waliingizwa darasani, kisomo kilichowawezesha kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mwamko mkubwa wa kusoma shule ya msingi ulifanikiwa kwa kiwango cha juu na sasa kazi ikiwa ni kutamani na kukamia elimu ya sekondari. Maelfu ya wanafunzi walitamani kusoma sekondari na kuanzia miaka ya 1970 kila mmoja aliyemaliza darsa la saba, akitaka afike kidato cha nne.

Licha ya mwamko mkubwa miongoni mwa wazazi na walezi kusomesha watoto wao msingi na kutamani waendelee walikwama kutokana na uhaba wa sekondari na mambo mengi yaliyoziba ukuta wa kuingia kwenye elimu ya sekondari, lakini changamoto ikiwa kubwa zaidi kwa wasichana.

Wakati taifa likiadhimisha miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika kwa kushangilia mafanikio ni vyema kuzipitia tena mbigiri na chungu zilizowakwamisha wengi hasa wasichana kusoma sekondari kati ya mwaka 1974 baada ya Azimio la Musoma, yote hayo yakiibuka kufuatia hamasa ya kupenda shule



Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, aliyebeba maono ya elimu kwa Watanzania wote. Hata leo maono yake yanaishi. **PICHA: MAKTABA**

> Leo maelfu ya wasichana wanafaulu, 'kutokupasi' kumeondoka sekondari ni nyingi, fursa zipo za kutosha, sheria na kampeni za kuwalinda dhidi ya unyanyasaji kijinsia zimeimarishwa, miaka 61 imekuwa na tija kubwa kwao.

na kujiendeleza zaidi japo wazazi na walezi waliwapa kipaumbele wavulana.

Miaka ya 1970 hadi 2000 ilikuwa migumu kwa waliotaka kuendelea na sekondari ni kwa sababu pengine hazikuwapo shule za kutosha na pia sekta binafsi ilikuwa na shule chache wakati serikali ikimiliki karibu zote, huku idadi ya wanafunzi ikiongezeka kila mwaka.

Mathalani, mkoani Kilimanjaro sekondari za umma za wanawake zilikuwa tatu Weruweru, Ashira na Machame na kuwapa ugumu kuingia sekondari baada ya kufaulu darasa la saba, si hivyo tu hali kama hiyo ilionekana Mwanza zilikuwapo sekondari za Nganza na Bwiru wakati Kagera au Ziwa Magharibi wakati huo, Rugambwa ilikuwa shule pekee ya wasichana na Morogoro ni Kilakala.

Aidha, itakumbukwa kuwa uhaba huo ulisababisha kufaulu na kuingia sekondari kuwa kazi ngumu, lakini madai kuwa wapo watu walioiba mitihani au kuinunua na kuwafundisha watahiniwa nayo yalisababisha wasichana wasifaulu kwa wingi japo wachache wenye bahati, au wanaotoka kwenye familia zenye uwezo ziwe za wanasiasa, watoto wa walimu, watumishi wakuu serikalini, wafanyabiashara na hata wenye uwezo kifedha walipenya.

Kulikuwa na madai kuwa wapo baadhi ya watu walinunua ufaulu wa watoto wao kwa maelezo kuwa wapo waliofaulu lakini majina yao yakakatwa na nafasi hizo kuchukuliwa na 'waliozilipia' yote hayo yakiwaweka pembeni wasichana na hata wavulana hasa maeneo ambayo watu walikuwa hawajui pa kukimbilia kufuatilia zaidi masuala ya matokeo ya mitihani.

Kulikuwa na tatizo la wanafunzi kurudia mitihani kwa muda mrefu kabla ya kutumika kwa teknolojia ya kutumia picha kwenye fomu za wanafunzi wa shule za msingi. Mbinu ya kutumia jina la mwanafunzi na kurudia au kukariri madarasa ilishamiri sana na kuwakwamisha wanafunzi wengine waliokuwa wakitamani kusoma lakini wakazidiwa na waliokariri.

"Mtu angeweza kukariri hata mara nne hata hivyo bila kufaulu lakini pia shule zilikuwa 'hazipasishi' hata miaka 10 hakuna mwanafunzi aliyefaulu. Ujanja wa kukariri ulitumiwa na familia zilizotaka watoto wao kwa udi na uvumba waingie sekondari, jambo lililowarudisha nyuma wasichana hasa kipindi hicho," anasema Martha Muyango-Lugora, mfanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Anakumbusha kuwa ilikuwa vigumu kwa wasichana wengi kusoma na hali ilikuwa ngumu zaidi vijijini kwa kuwa wengi waliishia kwenye utoro na wakati mwingine, kuachwa nyumbani bila kusoma kutokana na mila na desturi, mazingira magumu, uhaba wa shule jirani na hata majukumu ya kifamilia.

**KUMKOMBOA MSICHANA**

Martha anasema kama wengi walivyojiuliza inakuwaje shule hazifaulishi kwa miaka kadhaa? Kwanini wasichana wengi hawajaendelea na sekondari? Serikali nayo ilikuwa na maswali hayo pamoja na majibu yake.

Mojawapo ni ujenzi wa shule za msingi na sekondari nyingi uliofanywa kupitia mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi na sekondari MMEM na MMES wakati wa awamu ya tatu kuanzia miaka ya 1996 na kuendelezwa hadi sasa ambako ipo Sera ya Serikali Kugharamia Elimu (elimu bure).

Anakumbusha kuwa serikali pia iliruhusu kuwapo wa shule binafsi ziwe za msingi, sekondari, vyuo vikuu vya kati na taasisi nyingine za elimu yote hayo yakiongeza idadi ya wasichana darasani kuanzia msingi hadi ngazi za juu zaidi.

Serikali imejenga shule nyingi za msingi kwa kila kijiji, lakini kila kata ina sekondari, miundombinu kama vyoo bora, nyumba za walimu, mabara, huduma kwa wenye mahitaji maalumu na vyumba vya wasichana kwa ajili ya mahitaji maalumu kila mwezi, upatikanaji wa pedi za mabinti na hata vyakula shuleni yote hayo yamejenga mazingira bora ya soma na kujifunza kwa wasichana. Ni mafanikio makubwa katika miaka 61 ya Uhuru," anaongeza Martha.

Anasema leo maelfu ya wasichana wanafaulu, 'kutokupasi' kumeondoka sekondari ni nyingi, fursa zipo za kutosha, sheria na kampeni za kuwalinda dhidi ya unyanyasaji kijinsia zimeimarishwa, miaka 61 imekuwa na tija kubwa kwao.

Dorice Luhwago ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Ualimu Mkwawa (MUCE) mwaka 2021, anazungumzia hamasa kwa wasichana wakihimizwa kusoma sayansi nayo imekuwa kubwa.

Anataja juhudi za serikali kujenga sekondari za wasichana za sayansi kwa mikoa 26 ili kuhamasisha na kuongeza udahili wao kuanzia msingi, sekondari na elimu ya juu, kazi inayoanza mwaka huu. Anasema yote hayo ni baadhi ya fursa zinazoshangiliwa na wanawake wanaopata nafasi ya kusoma na kuwa wachangiaji kwenye maendeleo yao na taifa pia.

TESA inawatakia wasomaji wake heri na furaha nyingi wanaposherehekea uhuru wa nchi yetu.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Kukosa vyoo shuleni kulitafakarishe taifa baada ya miaka 61 ya Uhuru

TUMEFELI wapi kuwa na miundombinu ya vyoo kwenye shule zetu? Ni lazima kwenye mkusanyiko uwe shuleni, kiwandani au ofisini kuwapo huduma hii muhimu ya choo.

Wakati Ijumaa wiki hii ni sherehe ya kumbukumbu ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika, bado mambo ni magumu shule nyingi za msingi na sekondari zinazungumzia tatizo la uhaba wa vyoo na wanafunzi wanapohisi kujisaidia wanakosa pa kujisitiri. Tujiulize tumeshindwa wapi?

Mfano ni huu, Sekondari Mazinge iliyoko Manispaa ya Shinyanga, ikiwa na wanafunzi 854, wasichana 433 na wavulana 421 wanategemea matundu sita ya vyoo.

Idadi kiuwiano inamaanisha kuwa wanafunzi 142 hutumia tundu moja, yote hayo yakitishia afya zao pamoja na kusababisha kujisaidia kwa foleni, wengine wakijisaidia pembeni ya jengo au ukuta wa choo, vichakani na mashamba jirani hasa wanapobanwa haja muda mrefu.

Shule ya Sekondari Mazinge iliyoanzishwa Desemba, 2007 yenye wanafunzi 854, wasichana wakiwa 433, wavulana 421 wanatumia matundu sita ya choo kujisaidia.

Wasichana 433 wanatumia matundu manne na wavulana 421 wanategemea matundu mawili pekee jambo lisiloendana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 inayoelekeza wasichana 20 wanatumia tundu moja la choo wakati wavulana ni 25 kwa tundu moja.

Wasichana zaidi ya 100 hutumia tundu moja, na wavulana zaidi ya 200 tundu moja pia jambo ambalo ni hatari zaidi kiafya.

Felista Joseph ni mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule hiyo ya Mazinge, anayesema upungufu wa matundu ya choo shuleni hapo unawapa taabu na kero pamoja na kushindwa kujistiri wanapokuwa katika siku zao kwa sababu ya ukosefu wa chumba maalum.

Anasema saa 4.45 wakati wa mapumziko, wanafunzi hukimbia kuwahi kujisaidia kwasababu hakuna matundu ya kutosha na wanaochelewa hulazimika kupanga foleni na waliobanwa huumia zaidi na ikiwezekana huenda wanapopajua wenyewe.

"Ni usumbufu kupanga foleni kusubiri kujisaidia, tena hakuna hata chumba maalumu cha kujistiri japokuwa maji yapo, tunaomba serikali iliangalie hili tupate vyoo vya kutosha tena sasa hivi tunatumia matundu matatu moja limeziba," anasema Felista.

Mwanafunzi mwingine Suleiman Said, anasema wanatumia matundu mawili ya choo na wapo 421, na wakati wa kujisaidia hupanga foleni ndefu, na endapo mwenzao akichelewa wengine hujisaidia haja ndogo pembeni ya ukuta wa choo na kuchafua mazingira ambapo pamoja na kuhatarisha afya zao huongeza inzi na harufu mbaya eneo la shule.

"Tupo wengi hapa shuleni, lakini tunatumia matundu machache kujisaidia, na ukiangilia shule ipo mjini tunapata shida hivi je wa vijijni hali ikoje? " Anahoji Suleiman.

Mwalimu wa Mazingira shuleni hapo Ansiga Mbalale, anasema upungufu wa matundu ya vyoo shuleni hapo ni tatizo kubwa, na amekuwa akitoa elimu kwa wanafunzi kutumia vyoo kwa usahihi, pamoja na kufanya usafi mara kwa mara ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Anasema watoto shuleni hapo ni wengi, na hakuna uwiano sawa wa matundu ya choo na wasiposimamiwa kikamilifu suala la usafi wa vyoo shuleni hapo hatari kiafya kwa wanafunzi inaongezeka.

"Maji shuleni hapa yapo ya kutosha isipokuwa upungufu wa matundu ya choo ni tatizo tena wengine hujisaidia pembeni ya choo na kuhatarisha afya," anasema Mbalale.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mazinge, James Msimba, anasema mahitaji ya matundu ya choo kwa wasichana ni 20 yaliyoko ni manne na upungufu ni 16, wavulana mahitaji 14 yaliyopo ni mawili yakipungua 12.

"Nimeshaandika barua nyingi halmashauri za kuomba kujengewa matundu ya choo hapa shuleni, lakini mpaka sasa hakuna utekelezaji kama unavyoona na wanafunzi wanahangaika," anasema Msimba.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Tambukareli ilipo Sekondari ya Mazinge, Josephat Kisusi, anasema upungufu wa matundu ya choo kwenye shule hiyo walishalijadili sana pamoja na kuingiza kwenye vipaumbele vya bajeti ngazi ya kata lakini imekuwa vigumu kutatulika.

"Suala la ujenzi wa matundu ya choo katika shule yetu ya Sekondari Mazinge tumelijadili sana kwenye vikao vya kata, pamoja na kutoa mapendekezo kwenye bajeti ngazi za kata, lakini utatuzi wake umekwama, hadi imefikia kipindi tukaacha kulijadili sijui shida iko wapi,"anasema Kisusi.

"Tukisema tushirikishe wananchi tunashindwa sababu hali ya sasa hivi siyo nzuri kiuchumi, kutokana na ukame uliopo familia nyingi zinalia njaa," anaongeza Kisusi.

Mwananchi Jeremia Bundala, anasema serikali ingewashirikisha wananchi kutoa nguvu kazi ujenzi wa matundu ya choo shuleni hapo kazi hiyo ingekuwa imeisha zamani, lakini hawa shirikishwi.

Anadai wananchi wa eneo hilo hawajawahi kuitwa kwenye mkutano wa hadhara ili kuzungumzia jambo hilo, na kilichobaki wanasubiri hatima ya viongozi wenyewe kulitatua tatizo hilo la upungufu wa matundu ya choo.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ibara ya 18 kifungu (a) kinasema kila mtu ana uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake, lakini kwa wananchi wa Mtaa wa Tambukaleri hali ni tofauti, wanadai hawashirikishwi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, anakiri kwamba shule hiyo ya Sekondari Mazinge ina tatizo kubwa la upungufu wa matundu ya choo, huku akiitaja na shule nyingine ya Sekondari ya Kizumbi, na kueleza kuwa ujenzi utaanza Desemba mwaka huu shule zikifungwa.

Anazungumzia bajeti kuwa ni ndogo, ndiyo maana kwa sasa wanajitahidi kujenga miundombinu ya uchumi, ili wapate kukusanya mapato mengi ya ndani, ili yatumika kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo kujenga matundu ya choo.

***Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2020/2021 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu inataja halmashauri 77 kuwa zina uhaba wa matundu ya vyoo 111,931.***



Ukosefu wa vyoo vya kutosha unavyotesa wanafunzi. **PICHA: MARCHO MADUHU**

> Maji shuleni hapa yapo ya kutosha isipokuwa upungufu wa matundu ya choo ni tatizo tena wengine hujisaidia pembeni ya choo na kuhatarisha afya.





# Tanzania yaungana na dunia kutambua umuhimu wa benki

**Na Mwandishi Wetu**

Tangu mwaka 2020, dunia chini ya Umoja wa Mataifa imekuwa ikiadhimisha Siku ya Kimataifa ya Benki kutambua mchango wa taasisi hizo katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya mataifa.

Aidha, maadhimisho hayo ya kila tarehe 4 Disemba uzingatia pia umuhimu wa benki kwenye kuboresha maisha na kupandisha viwango vyake, kitu ambacho yamekuwa yanatilia maanani kwa karibu sana miaka ya hivi karibuni kupitia ajenda ya dunia ya ujumuishaji kifedha.

Mwaka huu ni wa tatu kufanyika kwa maadhimisho hayo yaliyofanyika Jumapili hii lakini kama miaka iliyotangulia hakukuwa na shamrashamra stahiki wala sherehe kubwa zilizofanyika si tu nchini bali duniani kote kwa ujumla.

**Siku ya Benki Duniani Ilivyoadhimishwa Tanzania**

Siku hii bado haijawa tukio kubwa la kitaifa na kasoro hii ni kwa dunia nzima. Kwa hiyo haishangazi hata wadau wengi wa sekta ya benki hawatambui hata kuwepo kwake hacha tu maadhimisho yake.

Vyanzo vya kisekta vinabainisha kuwa hata mwaka huu ni benki chake sana zilizoipa siku hii kibaumbele kinachostahili. Benki Kuu ya Tanzania ilisema wao walikuwa wana jambo lao lakini Umoja wa Benki Tanzania (TBA) haukuwa wazi kuhusu mipango yake.

Kampuni ya The Guardian Limited (TGL) inaunga mkono kuadhimishwa kwa Siku ya Kimataifa ya Benki na kupitia magazeti yake ya The Guardian na Nipashe, itakuwa kila mwaka inaungana na dunia kuadhimisha siku hii kwa kuchapisha ripoti maalumu na za kina kuihusu.

Lengo la kufanya hivyo hasa ni kuhamasisha kuwepo sherehe za siku hii na kuwachagiza wadau wote kuzingatia kuadhimishwa kwake. Jambo jingine ni kuujulisha umma kuhusu kuwepo kwake na umuhimu wa kuiadhimisha.

Hata hivyo, swala kubwa katika hili ni dhamira ya kutambua sio tu benki zinavyolihudumia taifa lakini pia kuthamini ushiriki wake katika kufanya maisha kuwa bora kwa wote.


**Usuli wa Kihistoria**

Kuwepo kwa siku na wiki za kimataifa kulianza tangu kuundwa kwa Umoja wa Mataifa mwaka 1945 na chombo hiki kimekuwa kinazitumia kutekeleza ajenda muhimu na maalumu ulimwenguni.

Mwaka 2019, Baraza la Umoja wa Mataifa lilipitisha azimo la kuadhimishwa kwa Siku ya Kimataifa ya Benki kila mwaka.

INAENDELEA UK. 18

## SEKTA YA BENKI TANZANIA
## Faida kabla ya kodi 2015 -2019




# Mtendaji Mkuu Moshingi asimulia safari ya mabadiliko makubwa TCB na faida za mageuzi hayo ya miaka kumi




Mwezi Julai mwaka jana, benki hiyo kongwe ilibadilishwa jina na kuitwa Benki ya Biashara Tanzania (TCB). Mgeni rasmi katika shughuli hiyo alikuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt Mwigulu Nchemba (wa tatu kulia). Wengine ni viongozi wa Serikali pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya TCB, Dr Edmund Mndolwa (wa tatu kushoto) na Afisa Mtendaji Mkuu Sabasaba Moshingi (wa pili kulia).

**Na Mwandishi Wetu**

Miasha ya Benki ya Biashara Tanzania (TCB) yamekuwa na hatua nyingi muhimu na ufanisi mkubwa lakini lipo jambo moja la msingi ambalo ni lazima litajwe katika kila simulizi ya maendeleo ya taasisi hiyo kongwe kuliko zote za fedha nchini.

Jambo hilo si jingine bali ni safari ya mabadiliko ya benki hiyo yanayoendelea ili kuiimarisha kiutendaji na kiushindani sokoni ambayo mpaka sasa yamekuwa na mafanikio makubwa tangu kuanza kwake mwaka 2011.

Huo ndiyo mwaka Afisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Bw Sabasaba Moshingi, alipojiunga rasmi na benki hiyo ya umma. Wakati huo, ilikabiliwa na changamoto nyingi za kiutendaji na haikuwa vizuri kifedha.

Kwa ufupi, TCB ambayo wakati huo iliitwa Benki ya Posta, ilikuwa tahabani na wengi waliichukulia kama chapa dhaifu kuliko zote miongoni mwa benki za Tanzania.

Bw Moshingi anakili na kukubali kuwa hali ya mambo ilikuwa ngumu wakati huo jambo ambalo linadhibitishwa na viashiria vya kiutedendaji.

Moja ya majukumu yake makubwa wakati anaajiriwa na Serikali ya Awamu ya Nne ilikuwa ni kusaidai kurekebisha kasoro hizo, ikiwemo ile ya mwonekano wake usiovutia na kuwa chapa duni.

**CHAPA KUBWA SHINDANI SOKONI**

Leo hii, miaka 11 baadae, hadithi ya TCB inasomeka tofauti kabisa huku jina lake jipya likionyesha ukubwa wake wa kufadhili maendeleo ya kitaifa na jinsi sasa ilivyokuwa chapa kubwa kiushindani.

Bw Moshingi anazikumbuka vizuri changamoto zote za wakati huo na usongo wa mawazo wa kukabiliana nazo uliomkuta na kumpa wakati mgumu kiusimamizi na kiuendeshaji wa taasisi hiyo.

Kutokana na jinsi TCB ilivyoimarika sasa hivi, ikiwa na mizania inayoifanya kuwa moja ya benki tano kubwa nchini, ni dhahiri shahiri kigogo huyo wa maswala ya kibenki amefanya kazi ya ziada kuyashughulikia matatizo yaliyokuwa yanaikwaza taasisi hiyo.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu ya kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Benki, kiongozi huyo wa TCB alisema kipindi hicho cha wakati mgumu bado kiko vizuri kwenye kumbukumbu zake.

**SIKU YA KIMATAIFA YA BENKI**

Tangu mwaka 2020, dunia chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa imekuwa ikiadhimisha Siku ya Kimataifa ya Benki kutambua umuhimu wa taasisi hizo za fedha katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya mataifa na mchango wake kwenye kuboresha viwango vya maisha.

Bw Moshingi anasema mchango wa TCB katika ujenzi wa taifa hauwezi kuelezeka kikamilifu bila kuweka bayana usuli na muktadha wa safari ya mabadiliko ya benki hiyo ambayo yametokea kuwa maarufu sana ndani na nje ya Tanzania.

"Karibu kila kitu kilikuwa katika hali mbaya nilipojiunga na TCB," alikumbuka hali ilivyokuwa na kubainisha kuwa kutokana na maendeleo yaliyopatikana hadi sasa wana kila sababu ya kuitunuku Siku ya Kimataifa ya Benki kwa kila aliyeshiriki na kuchangia mabadiliko makubwa yaliyofanyika TCB tangu mwaka 2011.

Wakati huo, TCB ilijulikana kibiashara kama Benki ya Posta Tanzania (TPB). Jina lake lilibadilika na kuwa TPB Bank PLC mwaka 2016 iliposajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni. Uhamuzi huo mahiri wa kubadilisha utambulisho wake ilikuwa ni hatua nyeti ya kimkakati katika juhudi za kuijenga upya benki hiyo.

## BENKI YA KISASA: MATUKIO MUHIMU YA MAGEUZI YA TCB

Miaka zaidi ya 10 ya safari ya mabadiliko ya Benki ya Biashara Tanzania (TCB) imekuwa na matukio mengi muhimu na hatua nyingi kubwa kimaendeleo.

Mojawapo na ya msingi kwenye harakati za kuiimarisha taasisi hiyo ni muugano wake na benki nyingine tatu za umma. Tukio jingine kubwa katika safari hiyo ni kubadilishwa jina kutoka Benki ya TPB na kuwa TCB mwezi Julai mwaka jana.

**MUUGANO NA TWIGA, TWB NA TIB CORPORATE**

Ndani ya miaka miwili, TCB iliunganishwa na benki tatu zinazomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Muungano wa kwanza ulikuwa ni ule wa mwezi Mei mwaka 2018 uliyohusisha benki ya Twiga Bancorp. Miezi mitatu baadae, iliuganishwa na Benki ya Wanawake Tanzania (TWB).

Mwezi Juni mwaka 2020, muungano na Benki ya TIB Corporate ulikamilika.

**BENKI YA TPB YAWA TCB**

Benki hiyo ilianza kutumia jina la TCB tarehe 14 Julai, mwaka 2021 na kufungua ukurasa mpya katika maisha yake kwa kupanua wigo wa kulihudumia taifa kupitia huduma kwa wateja binafsi na wale wa kibiashara.

## TAKWIMU MUHIMU: KUIMARIKA KIFEDHA KWA TCB

**MAPATO**

Kati ya mwaka 2010 na 2021, mapato ya TCB yaliongezeka kwa asilimia 750 kutoka TZS bilioni 20 hadi TZS bilioni 170. Ukuaji huo ni matokeo ya kuongezeka kwa mapato yanayotokana na riba kutokana na kukua kwa kiasi kikubwa kwa ukopeshaji na kupanuka kwa vyanzo vingine vya mapato.

**FAIDA**

Faida kabla ya makato ya kodi iliongezeka kwa asilimia 22 kutoka TZS milioni 0.9 mwaka 2010 hadi TZS bilioni19.7 mwaka jana.

**KUONGEZEKA KWA AMANA**

Amana za TCB ziliongezeka zaidi ya mara nane na kufikia TZS bilioni 918 mwaka 2021 kutoka TZS bilioni 109 miaka 12 iliyopita. Kiwango iki kilitokana na kuongezeka kwa shughuli za kimasoko, amana ya makampuni ya biashara na akiba za vikoba, pamoja na vikundi vya akiba na kukopa vijijini.

**UKOPESHAJI**

Kiasi cha mikopo iliyotolewa na TCB kilikua kwa zaidi ya asilimia 1,000 kutoka TZS bilioni 65 hadi TZS 719 kati ya mwaka 2010 na 2021. Mafanikio haya ni mchango wa huduma mpya zilizoanzishwa kama vile mikopo kwa wastaafu, Songesha, mikopo ya vikundi, elimu na ile ya kuanzia maisha.

**JUMLA YA MALI**

Ukubwa wa mizania uliongezeka kutoka TZS bilioni 121 hadi TZS bilioni 1,181, ili likiwa ni ongezeko la asilimia 876 kati ya mwaka 2010 na 2021.

**MTAJI WA WANAHISA**

Mtaji kutoka mwa wamiliki wa benki ulikua vizuri kwa kuongezeka kwa asilimia 14.7 kutoka TZS bilioni 7.7 mwaka 2010 hadi TZS bilioni 113.2 mwaka jana. Hii ilitokana na kuendelea kuifanya faida kuwa mtaji na wanahisa kuongeza uwekezaji wao.



**"Kufanikiwa kwa juhudi zetu za kuyakarabati matawi yetu yaliyokuwa yamechakaa nchi nzima na kuupanua mtandao wa matawi mara dufu, tumeweza kuwajumuisha wataeja 500,000 ambao awali walitengwa kwenye mfumo rasmi wa kibenki,"**
**SABASABA MOSHINGI, AFISA MTENDAJI MKUU, TCB.**

**BENKI KONGWE NCHINI**

Benki hiyo kongwe kuliko zote nchini ilibadilishwa jina na kuwa TCB mwezi Julai mwaka 2021 baada ya Benki ya TPB (TPB Bank) kuunganishwa na benki tatu za umma ambazo ni Benki ya Wanawake Tanzania(TWB), Twiga Bancorp na TIB Corporate Bank.

Hilo lilifanyika kama sehemu ya hatua ya Serikali ya Awamu ya Tano kuachana na benki za umma zinazofanya vibaya na kuunda moja kubwa yenye mafanikio.

Pamoja na changamoto zote ilizopitia na masahibu iliyokutana nayo, bado TCB inajivunia sifa ya kulihudumia taifa kwa kiwango cha hali ya juu kwa takribani karne moja.

Kuanza tena kwa uchumi huria nchini miaka ya 80 kulikoambatana na mageuzi ya sekta ya fedha miaka ya 90, kulipelekea Benki ya Akiba ya Posta ya Tanzania kubadilishwa na kuwa chombo tofauti. Mabadiliko hayo yalitokana na Sheria ya Benki ya Posta Tanzania Namba 11 ya mwaka 1991 iliyoitenganisha benki hiyo na Shirika la Posta na Simu Tanzania (TP&TC).

**UFANISI MDOGO NA MTAJI FINYU**

"Nilipojiunga na TCB mwaka 2011, wakati huo ikiitwa Benki ya Posta Tanzania, ilikuwa na hali mbaya ikikabiliwa na changamoto nyingi za kiutendaji ambazo zilihitaji kufanyiwa kazi haraka ili kuinusuru," Bw Moshingi alibainisha.

Ufanisi finyu na kukosekana kwa tija stahiki ni miongoni mwa kasoro zilizokuwa zinaikabili TCB wakati huo. Pia ilikuwepo changamoto ya mtaji ambao haukuwa unakidhi matakwa ya kikanuni.

Uongozi wa juu aliokuta Bw Moshingi nao ulishachoshwa na hali mbaya iliyokuwepo na ulishakata tamaa ya uwezekano wa benki hiyo siku moja kuja kuimarika tena.

"Wakati huo benki ilikuwa na tatizo kubwa kiufanisi kama ambavyo viashiria kadhha vya kiutendaji vinavyoonyesha. Uwiano wa gharama na mapato ulikuwa asilimia 96, kwa muda mrefu uwiano wa mali ulikuwa chini ya asilimia moja na uwiano wa fedha za wanahisa ulikuwa asilimia sita tu," Bw Moshingi alisema.

Hali ya mambo ilifanywa kuwa ngumu zaidi kutokana na morali mdogo wa wafanyakazi waliokuwa hawalipwi vizuri.

**MATAWI CHAKAVU, CHAPA DUNI NA BENKI DHAIFU**

Pia ulikosekana utaratibu wa kuwa na utamaduni wa kuitofautisha benki hiyo na taasisi nyingine. Changamoto za ukwasi na tatizo la mikopo chechefu vilizidi kufanya mambo kuwa magumu zaidi.

Wateja wake wakongwe waliokuwepo kipindi hicho cha majanga wanasema TCB ilipoteza mvuto si kutokana tu na huduma zake kuwa duni lakini pia kutolewa kwake katika mazingira mabaya.

"Karibu matawi yetu yote yalikuwa na taswira chakavu na hayakuwa na vitendea kazi ikiwemo ofisi za makao makuu. Kwa kweli tulikuwa na hali mbaya sana. TCB wakati huo ikiitwa TPB ikionekana kama inaelekea kuporomoka," Bw Moshingi alibainisha.

Kuajiriwa kwake ilikuwa ni kusaidia kuinusuru benki hiyo na changamoto hiyo. Ili kulifanikisha hilo, alifafanua, kwanza kabisa ilibidi wabaini nini haswa kilichokuwa kinaitesa benki hiyo ambayo kwa wakati huo ilikuwa na umri wa miaka 85.

**TATHMINI YA KINA**

"Tulifanya tathmini ya kina na kuja na mpango mkakati wa miaka minne uliojumuisha kipindi cha mwaka 2012 hadi 2015. Baadhi ya hatua tulizozichukua ni kuwaajiri wafanyakazi katika vitengo nyeti kutoka sekta binafsi," Bw Moshingi alibainisha na kusema kuwa safari ya mabadiliko ya TCB ikawa imeanzia hapo.

Katika mchakato huo, vyanzo vipya vya mapato vilibuniwa, bidhaa mpya zilianzishwa na hatua mahususi za ku-

INAENDELEA UK. 18

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# Mtendaji Mkuu Moshingi asimulia safari ya mabadiliko makubwa TCB na faida za mageuzi hayo ya miaka kumi

INATOKA UK. 17

punguza matumizi zikachukuliwa. Kuwavutia wateja wapya na kuwabakiza waliokuwepo, matawi yote chakavu nchi nzima yalifanyiwa ukarabati na mengine mapya yakafunguliwa.

Sasa hivi TCB inajivunia kuwa na moja ya mitandao mikubwa ya matawi nchini wenye vituo 82 vilivyotapakaa nchi nzima. Matawi haya yanatoa huduma kwa kushirikiana kwa karibu sana na zaidi ya ATM 400, mawakala lukuki na huduma ya kidijitali ya Popote, ambayo imekuwa na mchango mkubwa kwenye kuifanya TCB kuwa kinara wa ujumuishwaji kifedha nchini.

Uwekezaji katika huduma na bidhaa mpya za kibenki pamoja na suluhisho nyingine za kifedha ulileta matokeo chanya kwani mapato na faida vilianza kuimarika na hatimaye TCB ikaweza hata kulipa mishahara mizuri.

Bw Moshingi anasema wakati anajiunga na TCB, utamaduni wa kupima utendaji kazi haukuwepo kabisa na ili ilibidi lifanyike mara moja na matokeo yake yamekuwa ni ya kuridhisha sana.

**BENKI INAYOHESHIMIKA NA KUTENGENEZA FAIDA**

Kimsingi heshima iliyonayo TCB sasa hivi sokoni na taswira yake chanya ni matokeo ya mabadiliko yaliyofanyika mwaka 2016 baada ya miaka mingi ya kujipanga na kujiweka sawa kiushindani ili iweze kulihudumia taifa vizuri.

"Tangu wakati huo tumekuwa tunapata matokeo mazuri ya kifedha kila mwaka na tumekuwa na ukuaji wa karibu asilimia 20 kwa mwaka. Hiyo imepelekea kutufanya kuwa moja ya benki kumi zinazoongoza kwa faida katika kipindi cha miaka sita iliyopita," Bw Moshingi aliyegubikwa na furaha tele alibainisha kwa msisitizo.


TCB imekuwa na neema kubwa kifedha katika kipindi cha miaka kumi hadi kuweza kulipa gawio kwa wanahisa wake ambao wanaongozwa na serikali yenye umiliki wa asilimia 83 wa benki hiyo.

Mwaka jana faida iliyopatikana kabla ya kodi zilikuwa ni TZS bilioni 19.7 kiasi ambacho ni mara tano ya faida kama hiyo ya mwaka 2011. Kiwango hicho kilikuwa karibu mara 22 na mara 49 ya faida ya kabla ya kodi ya mwaka 2010 na 2007 mtawalia.

**MUUNGANO NA BENKI NYINGINE NA KINARA SOKONI**

Kuimarika kwa TCB hasa kifedha kuliifanya serikali kuitumia kuzinusuru benki za umma zilizokuwa taabani kwa kuziunganisha nayo.

Zoezi hilo lilianza mwaka 2018 kwa Benki Kuu ya Tanzania kuziunganisha benki za Twiga Bancorp na ile ya wanawake (TWB) na Benki ya TPB. Miaka miwili baadae, Benki ya TIB Corporate nayo ikaunganishwa na TPB Bank Plc hatua iliyopelekea mali yake kuongezeka na kuwa zaidi ya TZS trilioni moja.




"Huu ulikuwa ni muungano wa tatu wa kimabadiliko wa Benki ya Biashara Tanzania katika historia yake, ambao kwa njia moja au nyingine umetusaidia kujipanga vizuri kimkakati kwenye soko hili lenye ushindani mkubwa."

Kwa mujibu wa Bw Moshingi, kuunganishwa kwa TCB na benki hizo tatu kumeipandisha hadhi na kuifanya kuwa kwenye nafasi nzuri ya kutoa huduma kwa umma wote wa Kitanzania hususani zile za rejareja kwa ajili ya wateja binafsi na zile za mashirika ya kibiashara,

Ndoto na matamanio ya benki hiyo ni siku moja kuja kuwa taasisi namba moja ya huduma za kifedha nchini. Bw Moshingi anasema hilo linawezekana kabisa kama wakipewa fursa ya kufanya hivyo na zikawepo rasilimali hitajika kwa ajili ya kulifanikisaha.

## UKUAJI WA TCB SOKONI

| | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matawi | 33 | 38 | 49 | 52 | 59 | 82 |
| ATMs | 17 | 23 | 27 | 30 | 38 | 84 |
| Wakala (POS) | 0 | 10 | 167 | 190 | 250 | 2,701 |






# Tanzania yaungana na dunia kutambua umuhimu wa benki

INATOKA UK. 17

Azimio namba 74/245 lilipitishwa kuonyesha na kuzingatia jukumu kubwa la benki za maendeleo katika kuchangia maendeleo endelevu kote duniani na kuthamini mchango wa mifumo ya kibenki katika maisha ya kawaida na uzalishaji mali.

Kimsingi, siku na wiki za kimataifa ni fursa ya kuelimisha umma kuhusu mambo muhimu ya kimataifa. Matukio haya pia hutumika kuhamasisha utashi wa kisiasa na rasilimali kwa ajili ya kukabiliana na masuala mbalimbali lakini pia kuthamini na kuboresha mafanikio ya binadamu.

**Benki ya Biashara Tanzania**

Afisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Bw Sabasaba Moshingi, alisema wao wanaitoa Siku ya Kimataifa ya Benki ya mwaka huu kwa wote waliochangia mabadiliko yake makubwa na kuifanya kigogo wa huduma za kifedha nchini.

Mageuzi hayo yalianza takribani muongo mmoja uliopita wakati Serikali ya Awamu ya Nne ilipomwajiri Bw Moshingi kusaidia kutatua matatizo ya kifedha na kiuendeshaji yaliyokuwa yanaikabili TCB.

"Wakati huo ikiitwa Benki ya Posta Tanzania, TCB ilikuwa inakabiliwa na changamoto kubwa za kifedha. Ufanisi wake kiutendaji ulikuwa mdogo sana ikiwa na uwiano wa gharama na mapato wa asilimia 96, uwiano wa mali wa asilimia 0.3 na uwiano wa fedha za wanahisa ulikuwa asilimia sita tu," Bw Moshingi alisema.

"Faida kabla ya kodi ilikuwa ndogo na wastani wa mwaka ilikuwa ni TZS bilioni 400 hadi 900. Uwiano wa mapato na wafanyakazi ulikuwa TZS milioni 52 na hali ya kimtaji haikuridhisa kabisa," aliongeza.

Bw Moshingi pia alisema benki ilikuwa na matawi machache yaliyokuwa yamechakaa huku ofisi za makao makuu yake zikikabiliwa na uhaba wa vitendea kazi kitu kilichopelekea utendaji kazi wa kila siku kuwa mgumu.

"Ili kukabiliana na hali hiyo ilibidi mabadiliko makubwa yafanyike," kiongozi huyo aliambia Nipashe katika mahojiano maalumu."Bodi ya Wakurugenzi na manejiment walikubaliana ifanyike tathmini ya kina kubaini tatizo lilikuwa ni nini."

**Ushindani Katika Sekta**

Hilo lilifanyika na matokeo yake ni mafanikio makubwa iliyonayo TCB sasa hivi. Benki hiyo kwa sasa ni moja ya benki 10 kubwa nchini. Kuna zaidi ya benki 40 Tanzania.

Hadi Agosti mwaka 2021, sekta hiyo yenye ushindani mkubwa ilikuwa na benki 48 ambapo 38 zilikuwa ni za biashara, tano zilikuwa ni vikoba, benki ndogo nne, benki za nyumba mbili na mbili za maendeleo.

Takwimu rasmi zinaonyesha kuwa wakati azimio la kuadhimisha siku ya benki dunia linapitishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2019, sekta hiyo ilikwa ikiongozwa na benki 10 zenye mali ya TZS trilioni moja na zaidi.

Vigogo hivyo vilimiliki asilimia 72.2 ya mali zote, asilimia 72.98 ya mikopo na asilimia 74.5 ya amana huku benki za kizawa zikiwa ndizo vinara wa soko.

Kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania, tasnia ya benki inamiliki zaidi ya asilimia 70 ya mali zote za sekta ya fedha nchini inayojumuisha benki kubwa na ndogo, sekta ya bima, soko la mitaji na mifuko ya hifadhi ya jamii.

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

## KITISHO UDANGANYIFU MITIHANI

# Kilivyowatisha wadau wa elimu wataja chanzo ni ukosefu maadili

WANAFUNZI 2,190, wamefutiwa matokeo ya mtihani wa darasa la saba mkoani Dar es Salaam, huku vituo vya mitihani 24 navyo vikifungiwa, kutokana na kile kinachoelezwa kuwa ni kufanya udanganyifu katika mtihani huo uliofanyika Oktoba mwaka huu.

Idadi hiyo ya waliofutiwa mwaka huu ni zaidi ya mara tano ya wale waliochukuliwa hatua hiyo mwaka jana ambao walikuwa ni 393 waliotuhumiwa kujihusisha na udanganyifu wa mitihani kwenye shule na vituo mbalimbali ikimaanisha kuwa tatizo linaongezeka.

Kuendelea kuwapo kwa udanganyifu huo licha ya kwamba Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), hutoa onyo mapema kabla ya mitihani kufanyika, ni wazi sasa jitihada zinahitajika zaidi kudhibiti vitendo hivyo, ambavyo vinawachafua wahitimu wanaoonekana kuwa ni zao la matendo machafu.

Ili kutatafuta mwarobaini wa kudhibiti udanganyifu huo, Nipashe inazungumza na wadau mbalimbali wa elimu kwa lengo la kupata maoni yao ambayo wanaona yanaweza kusaidia katika vita hiyo inayoongezeka kila mwaka.




Suzan Lyimo, anaamini chanzo cha udanganyifu na wizi wa mitihani ni mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii. **PICHA: MAKTABA**

Mmoja wa wadau hao ni mwalimu mstaafu, Suzan Lyimo, ambaye anasema chanzo cha yote hayo ni mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii na kwamba bila kurudi kwenye maadili mema udanganyifu utaendelea kuwapo.

Anasema mwanafunzi hawezi kufanya udanganyifu, bali wanaofanya wanaweza kuwa ni wazazi, walezi au walimu kutegemea kile walichopata au wanachotarajia kukivuna na kunufaika na udanganyifu huo.

"Mwanafunzi wake ni kuchungulia majibu kwa mwenzake, hivyo hana uwezo wa kufanya udanganyifu. Wenye mchezo huo ni hao niliowataja, hivyo kweli tunataka udanganyifu uishe, turudi kwenye maadili mema," anasema Suzan.

Suzan ambaye ni mwanasiasa na mbunge mstaafu wa CHADEMA, anasema kuwa walimu ndiyo ambao wanatumika kwenye siasa kusimamia uchaguzi, na kwamba wamekuwa wakishiriki kufanya udanganyifu wa kura kama ambavyo baadhi ya wanasiasa wanadai.

"Udanganyifu huo ndio ambao wanaotumia hata kwenye mitihani. Kwa ujumla ni kwamba jamii imeoza, bila kurudi kwenye maadili, tutaendelea kushuhudia mengi ila kufutia wanafunzi matokeo ni sawa na kuwaonea wakati hatua zinapaswa kuwadhibiti wahusika," anasema.

Mdau huyo wa elimu ambaye amewahi kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu, anasema jamii yote ikiamua, udanganyifu huo unaweza kumalizika, na kwamba watu wa kada zote wakiwamo wanasiasa wajitokeze kukomea.

### KUKWEPA LAWAMA

Katibu wa Chama cha Kutetea Maslahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), Meshack Kapange, anasema, udanganyifu huo unatokana na kwamba walimu hawasikilizwi kilio chao, wanalazimika kufanya udanganyifu ili shule zao zisiwe na matokeo mabaya wakalaumiwa.

"Imekuwa ni kawaida wanafunzi wanapofanya vibaya, walimu wanalaumiwa hata bila kuangalia wanakabiliwa na changamoto gani katika mazingira yao ya kazi, wala mfumo wa elimu una matatizo gani," anasema Kapange.

Kapange anaongeza kuwa, ili kuepuka lawama, wanatafuta njia ya kujiokoa kwa kufanya udanganyifu huo ili wawe salama, na kwamba hatua hiyo inaweza kuendelea kuporomosha kiwango cha elimu.

"Kuna wakati matokeo ya elimu ya msingi yalifikia kupata wastani wa alama (GPA) kama sekondari, viwango vya ufaulu wakavirekebisha, ili angalau kuutafuta ufaulu wa wanafunzi ambao haupo ili uwepo, lakini matokeo yamekuwa magumu, sasa mwalimu wanafanya maarifa ili liende kukwepa baadaye asilaumiwe," anasema.

Mwalimu Kapange anasema walimu wanalazimika kufanya hivyo, kwa kuwa hawasikilizwi, mafao mengi yamekwama, wanaishi kwa madeni na kuongeza kuwa wengi wao hawakai na kadi zao za benki kwa sababu ya kukopa ziko kwa waliowakopesha.

"Kama nilivyoeleza awali, njia itakayomaliza udanganyifu katika mitihani, serikali kukaa na walimu ili kusikiliza na kutatua vikwazo vinavyowakabili, vinginevyo udanganyifu wa mitihani utaendelea," anasema, lakini hata hivyo hazungumzii ni maslahi ya walimu wa shule binafsi, akilenga zaidi za umma.

> Imekuwa ni kawaida wanafunzi wanapofanya vibaya, walimu wanalaumiwa hata bila kuangalia wanakabiliwa na changamoto gani katika mazingira yao ya kazi, wala mfumo wa elimu una matatizo gani.

### WASHITAKIWE

Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia Kurasini Dar es Salaam, Godwin Gonde, anasema adhabu ya kufuta matokeo au kufuta vituo haitoshi, na kwamba inasababisha udanganyifu kuendelea kujitokeza kila mwaka.

"Umefika wakati sasa wazazi, walezi au wote walio kwenye mnyororo huo waburuzwe mahakamani badala ya kufuta matokeo ya wanafunzi ambao mwaka unaofuata wanaweza kurudia mitihani," anasema Gonde.

Anaongeza kuwa mtihani ni nyaraka ya serikali hata kama ni wa chekechea, unatakiwa kutunzwa kwa gharama yoyote ile, lakini inashangaza kuona watu wakiendelea kufanya mchezo na nyaraka za serikali kila mwaka na idadi ikiongezeka.

"Ninaamini kwamba hatua kali za kisheria zikichukuliwa kwa wale wote wanaotoa fedha ili wapewe mitihani na wale wanaopokea fedha hizo, idadi ya wanaofutiwa mitihani ingepungua sana au kuisha kabisa," anasema.

Oktoba mwaka jana, aliyekuwa Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, alitangaza kuwafutia matokeo ya darasa la saba, wanafunzi 393, waliobainika kufanya udanganyifu katika mitihani kwenye shule ni vituo mbalimbali.

Aidha, akashauri hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa wote waliokuwa wamehusika katika udanganyifu huo, kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo visiendelee kujitokeza, licha ya maelekezo hayo kazi bado imeendelea.

Wiki iliyopita, Kaimu Katibu Mtendaji wa NECTA, Athuman Amasi, alitangaza matokeo ya mitihani ya darasa ya mwaka huu, huku akifafanua kuwa wanafunzi 2,190 wamefutiwa matokeo.

Mbali na kufuta matokeo, akasema vituo vya mitihani 24 vimefungiwa, huku wanafunzi 540 wa vituo sita vya mitihani mkoani Dar es Salaam, wanachunguzwa, ili ikibainika kuhusika katika udanganyifu, watafutiwa.

# Kiboko kiwepo au kiondolewe shuleni?

INATOKA UK.13

ya watoto wanaacha shule kwa sababu ya kukimbia viboko, huku wengine wakipata majeraha makubwa na ulemavu na hata kupoteza maisha eti kwa sababu ya adhabu za viboko jamani haipendezi," anasema.

Anawaambia washiriki kuwa hilo halikubaliki kwa kuwa adhabu ya viboko haikulenga kusababisha mateso kwa watoto na kwamba ndiyo maana kuna waraka unaoekeleza jinsi ya kutoa adhabu shuleni.

"Serikali itaziimarisha Kamati za Ulinzi wa Watoto na Wanawake na Madawati ya Ulinzi wa Watoto shuleni, ili wafahamu maudhui ya waraka huo wasifanyiwe kinyume na wakibaini kuwa ni kinyume wapaze sauti haraka," anasema.



Furaha na kupenda masomo ni mambo yanayopingana na adhabu kupindukia. **PICHA: MAKTABA**

### VIBOKO NI SAWA

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la masuala ya haki wanawake na watoto la LUTOGO Development Initiative, Lulu Mwalubandu, anasema adhabu kwa wanafunzi haziepukiki, lakini zisiwe za kukomoa.

"Wapo baadhi ya watoto hawashikiki bila viboko, hivyo ingawa kuna wengine wanapinga adhabu hiyo shuleni, mimi ninaona ni bora iendelee kwa kuzingatia huo Waraka wa Elimu Namba 24," anasema Lulu.

Anafafanua kuwa adhabu hiyo imekuwa ikichukuliwa kama mateso kwa wanafunzi, kutokana na kwamba baadhi ya walimu wanatoa adhabu kwa lengo la kukomoa badala ya kumrekebisha mkosaji, lakini ni muhimu katika kufundisha na kuwarudi watoto.

"Tunaamini kuwa walimu ni watu wa saikolojia, hivyo wanaweza kuwatambua wanafunzi kwa urahisi wanapokuwa na matatizo na kuwasaidia, lakini hawatumii ujuzi huo, ili nguvu zaidi hutumiwa pale mwanafunzi anapofanya kosa," anasema.

> "Kuna miongozo au uchapaji, idadi ya viboko na sehemu ya kuchapa, mwalimu wa kawaida ni viboko viwili akitaka kuzidisha ni lazima apate idhini ya Mwalimu Mkuu, mbona yote yako wazi tu.



Adhabu kali kwa wanafunzi kunapunguza hamu ya kupenda shule. **PICHA: MAKTABA**

Anaongeza kuwa baadhi ya wanafunzi wana matatizo nyumbani, wanaweza kuchelewa kufika shule au kutofanya vizuri darasani na kwamba mwalimu anapoona hali hiyo, anatakiwa kumdadisi ili kujua ukweli kabla ya kumwadhibu.

"Lakini wengine hawafanyi hivyo, wanachukulia tu kwamba ana kiburi na wanamwadhibu, na kumbe ana matatizo makubwa nyumbani kwao yanayosababisha achelewe au asifanye vizuri darasani," anasema Lulu.

Ofisa Uchechemuzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Wakili Maduhu William, anasema kama waraka huo ungezingatiwa, kusingewapo matukio ya kuumizwa kwa wanafunzi.

"Kuna miongozo au uchapaji, idadi ya viboko na sehemu ya kuchapa, mwalimu wa kawaida ni viboko viwili akitaka kuzidisha ni lazima apate idhini ya Mwalimu Mkuu, mbona yote yako wazi tu," anasema William.

Anaongeza kuwa kama miongozo ya serikali ingekuwa ikitekelezwa, kusingekuwa na malalamiko kutoka kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuhusu adhabu zinazotolewa na baadhi ya walimu shuleni.

### VIONGOZI WA DINI

Mwalimu wa Injili katika Kanisa Katoliki au Mkatekista kutoka jijini Dar es Salaam,( anaomba asitajwe) anasema wanaosema mtoto asitandikwe na adhabu hiyo kufutwa wana nia njema lakini si sahihi.


Ananukuu kitabu cha Mithali 23:13 kikisema "Usimnyime mtoto wako mapigo, maana ukimpiga kwa fimbo hatakufa, ni njia ya kumfundisha, kumkanya na kumrudi mtoto fimbo hazikwepeki ila wafundishwe kwa utaratibu na kupigwa viboko kwa nia ya kuwaelimisha siyo kuwaumiza," anakumbusha Mkatekista.

## CHEMSHABONGO NA -00 26 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. Mzazi wa kiume
5. kinyume cha neno baada
8. hali ya kuwa sawasawa
9. neno la kuuliza
10.fyonya
11.samaki wa kuchomwa
13.elezwa 16.fanya kiumbe
19.mwanazuoni
20.mtutumuko wa maji baharini
21.ghala, bohari
23.mwezi wa nane 24.ubinadamu


Chini:
1. nyumba ya kurekebisha sheria
2. bara kubwa duniani
3. vita
4. tokwa jasho
6. ganja
7. Maksi
10.Mnyama mwenye nguvu na mkali 12.Kale
14.mtungi mkubwa na mrefu wenye shingo nyembamba
15.muziki 17.chelewa
18.mashauri, matendo 22.ubaya



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

GANDAMIZWA
KHOIKHOI
SAFARI
ALAMINA
KANANA
AMANISHA
PANIA
PAKATA
AMALI
NANASI
INAMA
ASKARI
SANAA

KAR
HUA
DA
TISA
AINI
HAI
DARI
KATI
SIKIA
FUONI
SHIA
UFA



Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| J | A | J | I | | M | A | D | A | I |
| I | M | A | N | I | | | H | | B |
| J | A | N | A | B | I | | A | D | A |
| I | N | A | M | A | | | B | | D |
| | I | | I | R | A | N | I | | A |
| M | | M | S | A | M | A | H | A | |
| A | D | A | H | | A | B | U | D | U |
| B | | P | A | N | Z | I | | H | |
| A | | E | | | O | I | L | I | |
| K | A | M | A | | N | | | B | |
| I | | A | | P | I | N | G | U | O |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | U | M | A | | M | U | N | G | U |
| U | M | A | T | I | | | O | | B |
| J | A | L | A | L | A | | A | P | A |
| O | | A | M | A | N | A | | | N |
| | K | I | I | N | I | | N | T | I |
| | I | | A | I | S | E | E | | |
| A | G | A | | | E | L | E | W | A |
| | A | G | O | | | I | M | A | |
| M | L | A | N | G | O | | A | L | A |
| | I | | A | | | | | I | |



# Waomba mabadiliko ya mitaala elimu ya watoto wenye mahitaji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

ASASI zinazohudumia watoto wenye mahitaji maalumu wameiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufanya marekebisho ya mitaala ili elimu inayotolewa kwa kundi hilo iwanufaishe watoto wenye ulemavu ili wafike elimu ya juu.

Wamesema mitaala ya sasa imekuwa ikiwasaidia watoto wenye mahitaji maalum kupata ujuzi pekee.

Ombi hilo lilitolewa na Shirika la kuhudumia watoto wenye mahitaji maalum liitwalo CST mkoani Mbeya wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wenye Ualemavu Duniani yaliyofikia kilele mwishoni mwa wiki.

Meneja Miradi wa CST, Hildergade Mehrab, alisema mifumo ya elimu iliyoko nchini haimwandai mtoto mwenye mahitaji maalum kujiendeleza kielimu badala yake idadi kubwa ya watoto hao huishia kupata ujuzi na kujiajiri wenyewe au kuajiriwa.

Alisema kama ilivyo kwa watoto wengine wasio na ulemavu, mifumo ya elimu inapaswa kuwa rafiki kwa watoto wenye ulemavu ili na wao wawe na uwezo wa kujiendeleza kielimu mpaka kufikia elimu ya juu.

Hildergade alisema Siku ya Walemavu Duniani inatoa fursa kwa serikali na wadau nchini kufanya tathmini ya upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo elimu bora kwa watu wenye mahitaji maalum.

Alidai miongoni mwa maeneo ambayo Wizara ya Elimu inapaswa kufanyia kazi ni marekebisho ya mitaala ambayo itaweka mazingira mazuri ya kumwandaa mtoto mwenye ulemavu kupata elimu jumuishi ili kutimiza malengo waliyojiwekea.

Alisema katika kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanatimiza ndoto zao, CST, wanahamasisha upatikanaji wa haki na huduma za kijamii kwa kundi hilo.

Alidai kuwa wazazi na wadau wengine wamekuwa wakijadili namna ya kuchagiza ubunifu na kuleta maendeleo jumuishi kwa watoto ili kufikia malengo ya kauli mbiu ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani kwa mwaka huu isemayo 'Suluhisho la mabadiliko kwa maendeleo jumuishi nafasi ya ubunifu katika kuchagiza duniani inawafikiwa kwa usawa'.

Alisema wanaendelea kuwaandaa watoto hao kujifunza ujuzi wa aina mbalimbali kulingana na ulemavu walio nao ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi ambalo limekuwa na ushindani mkubwa.

Aliongeza kuwa pia wanawafundisha watoto namna ya kutatua vikwazo vinavyowakabili pamoja na uwezo wa kufanya mawasiliano na watu wengine bila kujali aina ya ulemavu walio nao.

Mratibu Mradi CST, Edward Majura, alisema anatamani kuona nchi inafikia maendeleo jumuishi kwa kuzingatia haki za watu wenye mahitaji maalumu zinapatikana na kulindwa.

Alisema Katiba ya Tanzania inasema watu wote ni sawa hivyo kila Mtanzania anao wajibu wa kulinda haki ya mwenzake kwa kuhakikisha fursa mbalimbali za kiuchumi na huduma nyingine za kijamii zinapatikana kwa usawa.

Mwalimu wa Lugha za Alama kutoka Shule ya CST, Ben Liuvale, alisema ni jukumu la kila mwalimu kutengeneza mazingira rafiki ya ufundishaji ufikiwe kwa asilimia 100 kwani itahusisha ubunifu na vitendo kwa kuzingatia hali za watoto wote wenye mahitaji maalum.

Nuru Mwakitalima, alisema miongoni mwa mambo yanayopaswa kushughulikiwa na serikali kwa sasa ni kutengeneza mazingira rafiki ya utoaji wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum.

## Mbeya-UWWSA yatoa msaada mifuko 50 ya saruji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEYA- UWWSA) imetoa msaada wa mifuko 50 ya saruji kusaidia ujenzi wa ofisi za Kata ya Kalobe iliyoko Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya, Gilbert Kayange, alitoa msaada huo ikiwa ni hatua za kuthamini mchango wa wananchi katika kuboresha huduma za upatikanaji wa maji.

"Msaada huu ni sehemu ushirikiano baina yetu na wananchi kwa sababu hiyo mamlaka imeamua kuchangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Ofisa ya Kata ya Kalobe ili wapate huduma za kijamii,"alisema Kayange.

Alisema mamlaka hiyo ina jukumu la kusaidia jamii shughuli mbalimbali za maendeleo pamoja na kuwahimiza utunzaji wa vyanzo vya maji na usafi wa mazingira, kuzuia upotevu wa maji na kulipa bili kwa wakati.

Kutokana na hayo alisema mamlaka itaweza kutimiza wajibu wake wa kutoa huduma ya maji endelevu na toshelevu kwa jamii inayoihudumia.

Diwani wa Kata ya Kalobe, Ally Bromela, alisema msaada huo utasaidia kukamilisha ujenzi wa ofisi kwa haraka ili wananchi waanze kupata huduma.

Alisema kwa sasa huduma zinatolewa kwenye nyumba za kupanga hivyo kukamilika kwa ofisi hiyo kutasaidia wananchi kupata huduma kwenye mazingira mzuri na yenye utulivu.

Tunaishukuru mamlaka kwa msaada waliotupatia tunaahidi kuboresha mahusiano yetu ikiwa ni pamoja na kuwa mabalozi wa utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji ili huduma ipatikane kwa uhakika na wakati wote.



Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Emmanuel Mjema (kushoto), akipokea tuzo ya kutambua mchango wake katika ujenzi wa majengo ya chuo hicho, kutoka kwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, juzi katika mahafali ya tisa ya chuo hicho jijini Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# CBE kuanzisha programu ya mafunzo atamizi, uanagenzi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), Kampasi ya Mbeya, kinatarajia kuanzisha programu ya mafunzo atamizi na uanagenzi kwa wanafunzi na watu binafsi wenye nia ya kupata ujuzi na maarifa kutokana na shughuli wanazozifanya.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwaandaa wananchi kuwa wabobezi kwenye bidhaa wanazozalisha na kuwawezesha kupata masoko ya uhakika na yenye tija.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe alitoa kauli hiyo juzi kwenye mahafali ya tisa ya CBE Kampasi ya Mbeya.

Alisema programu hiyo inatarajiwa kuanza mwaka wa masomo 2023/2024 na kwamba wananchi kutoka maeneo mbalimbali nchini wanapewa fursa ya kusoma masomo hayo.

Alisema programu hiyo itakuwa msaada kwa vijana katika kutimiza ndoto zao za kujikwamua kiuchumi kwani chuo hicho kitawalea na kuwafundisha ujuzi wa kutosha.

Makamu wa Bodi ya Uongozi wa CBE Mbeya, Peter Mwambuje, alisema programu hiyo itakuwa mwarobaini wa kubadilika mawazo ya biashara kuwa biashara halisi.

Alisema wamejipanga kupokea wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuwafundisha programu za uanagenzi na atamizi wa vitu wanavyovitengeneza.

Mkuu wa CBE nchini, Profesa Emmanuel Mjema, alisema wanafunzi 450 wamehitimu kozi mbalimbali kama vile uhasibu, uongozi wa biashara, masoko, manunuzi na ugavi, teknolojia ya habari, vipimo na viwango na ushauri wa kibiashara.

Alisema wanafunzi hao wameandaliwa vyema kujiajiri na kuajiriwa kupitia taasisi mbalimbali zilizoko ndani na nje ya nchi.



HABARI DODOMA

# Viongozi wa dini watakiwa kuhubiri kupinga ukatili

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Jabir Shekimweri, amesema viongozi wa dini wanapaswa kutoa mahubiri yatakayosaidia jamii kuondokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Shekimweri aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waumini wa Kanisa la Kalmeli Assemblies of God lililoko Ipagala jijini hapo katika hafla fupi ya kutoa misaada mbalimbali kwa wajane, yatima na watu wanaoishi katika mazingira magumu.

Alisema hivi sasa ukatili umeongezeka kutokana na watu kupunguza upendo na kutokuwa na hofu ya Mungu.

"Nyie viongozi mnapaswa kuhubiri mahubiri ya kuonesha upendo kwa jamii ambayo haina uwezo itasaidia kuepukana na unyanyasaji wa kijinsia," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Ipagala, Dotto Gombo, alisema kitendo kilichofanywa na kanisa kwa kuwapatia mahitaji wahitaji ni jambo linaloonesha upendo wa Mungu kwa wahitaji.

"Kanisa limekuwa likifanya matukio ya kuwajali yatima na wajane kila mwaka jambo ambalo linaonesha upendo, umoja na wale wenye uhitaji," alisema.

Kwa upande wake, Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Dk. Evance Chande, alisema licha ya kuwajali watu wenye uhitaji kwa upande wao wataendelea kuisadia serikali kuwafikia watu wenye mahitaji mbalimbali kiroho na kijamii.

"Miongoni mwa misaada hiyo ni pamoja na kuwafundisha elimu ya ujasiriamali ili kuwafanya kujisimamia kwa baadhi ya mahitaji yao kama vile ya kiuchumi."

"Serikali haiwezi kutoa ajira kwa watu wote kama vile wenye uhitaji, vijana, wajane na yatima, hivyo kanisa limeamua kuisaidia serikali kuwafundisha jinsi ya kujitegemea ni wazi wataweza kujitegemea na kujikwamua kiuchumi," alisema.

Askofu huyo alisema kuwa wameanzisha masomo hayo kwa lengo la kuhakikisha vijana kuondokana na tabia ya kufikiria kupata ajira serikalini badala yake wajiajiri wenyewe.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akikabidhi msaada kwa ajili ya watoto yatima uliotolewa na Kanisa la Karmeli Assemblies of God Ipagala Dodoma kwa ajili ya kuwasaidia kimaisha jana, (wa pili kulia) ni Askofu Dk. Evance Chande wa kanisa hilo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Mamalishe wapewa elimu ya ujasiriamali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMALISHE zaidi ya 300 wa Jiji la Dodoma, wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali na kukabidhiwa majiko ya gesi ili kuboresha shughuli zao na kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Mafunzo hayo yametolewa na Ofisi ya Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde kwa kushirikiana na kampuni ya Coca Cola Tanzania na Oryx Ltd kupitia Kongamano maalum la mamalishe 'Mwanamke Shujaa' lililofunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa Umma na Mawasiliano wa Coca Cola Ltd, Nassor Salum, alisema mpango wa kampuni hiyo ni kuweka mazingira wezeshi kwa kinamama kufanya biashara zao.

Alisema lengo ni kusaidia kukuza biashara zao ili ziwe na tija kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira ndio sababu ya kukubali ombi la mbunge huyo.

Naye Mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda, aliwahimiza wanawake kujiwekea malengo ya kukuza biashara zao na kutokubali kukatishwa tamaa na vikwazo vyovyote.

Akitoa shukrani kwa niaba ya kinamama hao, Mbunge Mavunde ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo, alishukuru kampuni hizo kwa kumuunga mkono kwenye mkakati wake wa kuwawezesha kiuchumi.

Aliahidi kuandaa kongamano la uwezeshwaji kiuchumi wa kinamama litakalokwenda sambamba na uanzishwaji wa kampuni na majina ya biashara.

# Waomba ufanyike utafiti mbolea za asili

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SERIKALI imeombwa kuzifanyia utafiti mbolea za asili zinazotokana na kinyesi cha mifugo ili kuepukana na mbolea za kisasa za nje ya nchi ambazo upatikanaji wake umekuwa kikwazo kwa wakulima wanawake.

Wakizungumza jana kwenye kikao cha Jukwaa la Wakulima Wanawake na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe jijini hapo, baadhi ya wakulima hao kutoka mikoa mbalimbali nchini walisema kero ya mbolea itatatuliwa iwapo serikali itazifanyia utafiti mbolea za asili. Mkulima Fredina Saidi kutoka Kishapu mkoani Shinyanga, alisema gharama kubwa za ununuzi wa mbolea imekuwa kikwazo kwa wakulima wanawake na kuiomba serikali kuzifanyia utafiti mbolea za samadi ili kuepukana na kuagiza zinatoka nje.

"Iwapo serikali itakomaa na utafiti wa mbolea zinazotokana na mifugo, inawezekana itaondokana na kero za kelele kutoka kwa wakulima kununua kwa gharama kubwa mbolea kutoka nje ya nchi," alisema.

Naye Sophia Boke, kutoka Wilaya ya Chamwino mkoani wa Dodoma, alisema wakulima wengi wanashindwa kupata mbolea kwa wakati na inapofika wakulima wengi wanakuwa wapo kwenye mavuno.

"Ushauri wetu kwa serikali tunaiomba ituletee mbolea wakati tumeshavuna na kuuza mazao kutokana na kipindi hicho wanakuwa na fedha mkononi...pia zifanyiwe utafiti mbolea za asili," alisema Sophia.

Aidha, Mwenyekiti wa Jukwaa hilo kutoka wilayani Chamwino, Janeth Nyamaya, alisema kutokana na kero ya upatikanaji wa mbolea hususani kwa wakulima wadogo wanawake wanaomba utafiti huo ufanyike.

Awali, Meneja Mradi wa Action Aid, Samuel Mkwatwa, alisema shirika linawasimamia wakulima wadogo wanawake katika baadhi ya mikoa na kuunda majukwaa ili kuwasaidia kuzungumzia kero zinazowakabili.

"Kwa mfano hiki kikao shirika limesimamia baada ya wanawake wakulima kuomba kukutana na waziri kuelezea kero zao...pamoja na kutoonana na waziri, lakini wakurugenzi waliopewa majukumu kusikiliza kero za wakulima zimeonyesha mapokeo," alisema Mkwatwa.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri Bashe, Mkurugenzi wa Idara ya Mipango na Usimamizi wa Ardhi ya Kilimo, Mhandisi Juma Mdeke, alisema serikali inaendelea kuangalia umuhimu wa mbolea ya samadi na kuendelea kufanyia utafiti.

"Nchi ina teknolojia bora ya kisayansi, tunachoshauri ni kutunza udongo na maji wakati serikali ikiendelea kufanyia utafiti mbolea za asili kutokana na kufahamu umuhimu wake," alisema Mdeke.



## Bandari ya Shumba kukifungua kisiwa cha Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini Wilaya ya Micheweni ni sehemu ya mikakati ya kwenda kukifungua kisiwa cha Pemba kiuchumi na uwekezaji na kukiunganisha na nchi jirani za Afrika Mashariki.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, wakati alipofanya ziara kuangalia ujenzi wa bandari hiyo, Wilaya ya Micheweni, Pemba.

Alisema Serikali ya Zanzibar, imejipanga kuhakikisha kisiwa cha Pemba kinafunguka kiuchumi kwa kukiunganisha na mikoa mengine ya Tanzania Bara pamoja na Afrika Mashariki kiuchumi hatua ambayo itasaidia kuwainuwa wananchi kibiashara.

Alisema katika kisiwa cha Pemba jumla ya bandari tatu zimepangwa kuboreshwa ikiwamo ya Wete, Mkoani pamoja na Shumba mjini.

Aidha, aliwataka wananchi wa kisiwa cha Pemba kujipanga zaidi kuzichangamkia fursa za kiuchumi za kuwapo kwa bandari hizo kubadilisha maisha ya wananchi wa Pemba.

"Hiyo ndiyo mikakati ya Serikali ya Zanzibar kuona kwamba kisiwa cha Pemba kinafunguliwa kiuchumi na uwekezaji na kukiunganisha na nchi za Afrika Mashariki katika sekta ya kibiashara," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema hiyo ni fursa nyingine kwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni katika kufunguwa fursa za uwekezaji kwa wawekezaji kuwekeza miradi mikubwa.

Alisema ujenzi wa bandari hiyo utakiunganisha kisiwa cha Pemba na nchi jirani ikiwamo Mombasa, Kenya kwa wafanyabiashara wa pande mbili hizo kushirikiana kibiashara.

"Nachukua nafasi hii kuipongeza serikali kwa kutekeleza ahadi zake za kukifungua kisiwa cha Pemba kiuchumi na uwekezaji ikiwamo ujenzi wa bandari kuu za kimkakati ikiwamo ya Shumba mjini," alisema.

Naye Mkurugenzi wa ufundi wa Shirika la Bandari, Salum Udi, alisema bandari hiyo itakuwa na urefu wa mita 40 ambapo itakuwa na uwezo wa kutia nanga meli zenye uwezo wa tani 2,000.

Alisema ujenzi huo unatarajiwa kumalizika ifikapo mwakani Oktoba kwa kutoa huduma kwa meli na vyombo vyengine vya usafiri kutia nanga.

Alisema kuwapo kwa bandari hiyo ambayo ni ya kimkakati zaidi itaziwezesha hata meli za nchi jirani ya Kenya kutia nanga na kushusha bidhaa mbalimbali na mizigo.

"Ujenzi huu ni sehemu ya kutekeleza miradi ya kimkakati katika kisiwa cha Pemba katika sekta ya mawasiliano ya bandari ambayo itafungua milango ya biashara kwa wananchi wa pande mbili hizo," alisema.

# Hoteli yaandaa keki maalumu Krismasi na Mwaka Mpya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuwavutia wageni na watalii kwenye msimu wa Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya hoteli ya Maruru Zanzibar, imeandaa keki maalum na kipekee ambayo upishi wake ni tofauti na zilizo zoeleka.

Keki hiyo ni ya kipekee kwa Tanzania ambayo huwa na mchanganyiko wa matunda yaliosindikwa zikiwamo zabibu na korosho, hulowekwa na pombe kwa muda wa siku 21 na kupikwa.

Akizungumza na waandishi wa habari katika maandalizi ya keki hiyo yaliyoanza jana, Meneja wa hoteli hiyo, Philip Mwakimu, alisema kila mwaka hupika keki ya aina hiyo na huwa kivutio kikubwa kwa watalii.

"Kama unavyoona leo hapa tumeanza maandalizi ya upishi huu wa keki na hulowekwa kwa siku 21 ambapo ndani yake kuna mchanganyiko wa nafaka mbalimbali yakiwamo matunda yaliyosindikwa na pombe," alisema.

Alisema maandalizi yake huchukua siku 21 na inatarajiwa Desemba 25 siku ya Krismasi kupewa wageni wote wanaofika katika hoteli hiyo.

Naye Msaidizi wa Mpishi Mkuu wa hoteli hiyo, Muhammed Abdallah, alisema kila inapofika mwanzoni mwa mwezi wa Desemba, hoteli hiyo huanza maandalizi ya upishi wa keki hiyo ambayo huwashirikisha wafanyakazi wote na wageni wa hotelini hapo ili kujifunza upishi wake.

"Hii keki huvumbikwa kwa siku 20 tunaweka pombe kali ili kulainisha matunda yanayotumika katika keki hii. Na hii keki imekuwa ikipendwa na watalii wengi wanaofika hapa," alisema.

Alisema keki hiyo ina uzito wa kilo 30 na ina uwezo wa kuliwa na watu zaidi ya 90 na kwa muda wa miaka mitatu sasa wanapika upishi huo.

Alisema lengo la kupika upishi huo ambao unasifika nchini Sirilanka ni kuwavutia wageni na kuwaonesha utofauti wa vyakula walivyonavyo ambavyo hawavipati katika hoteli zingine.

"Ukila hii keki huna haja tena ya kunywa pombe maana huchanganywa na pombe na kwa wale ambao hawatumii pombe huwa tunawapikia keki nyingine iliyozoeleka," alisema.



Wafanyakazi wa hoteli ya Maruru Zanzibar wakichanganya matunda yaliyosindikwa na pombe kwa ajili ya upishi wa keki ya kipekee yenye ukubwa wa futi 30 ambayo hulowekwa siku 21 kwa ajili ya Sikukuu ya Krismasi kwa wageni na watalii wanaotembelea hoteli hiyo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Sera ya uchumi wa buluu yahimiza usalama baharini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, amesema sera ya uchumi wa buluu imehimiza suala la ulinzi na usimamizi wa bahari ili wakati wote kuwa salama.

Alisema katika kufikia mafanikio ya kukuza uchumi wa buluu lazima bahari ilindwe na mambo mbalimbali ikiwamo uchafuzi wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema hayo mjini hapo wakati akifungua semina kwa wadau wa ulinzi na usalama wa bahari.

Alisema kwa kuwa bahari ina umuhimu mkubwa kwa uchumi wa Zanzibar, wizara imeona haja ya kushirikiana na wananchi wa Zanzibar katika usimamizi na utunzaji wa mazingira wa bahari.

Aidha, alisema hivi sasa hali ya mazingira imeonekana kuwa ni moja ya kikwazo kufikia malengo ya kutunza bahari.

Alisema ujio wa wageni kutoka Uholanzi na kuisaidia Zanzibar katika ulinzi na usalama wa bahari ni moja ya kuondoa changamoto mbalimbli ikiwamo ya ulinzi na usimamizi wa bahari.


Alisema nchi nyingi duniani zilizo zungukwa na bahari zinakabiliwa na changomoto ya kuathiriwa na uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Nchi za visiwa huwa na rasilimali za mafuta na kwa upande wa Zanzibar kipindi kifupi kijacho rasilimali hiyo itachimbwa lakini ikianza tu uchimbaji wa mafuta hata uharibifu wa mazingira huwa unajitokeza, hivyo ni vyema kuwa na mikakati ya kudhibiti hali hiyo," alisema.

Naye komando wa Maritime Capacity Allince, kutoka nchini Uholonzi, Pepijn Verstand, alisema kisiwa cha Zanzibar kimezungukwa na bahari, ulinzi na usalama wa bahari unahitajika wakati wote.

Alisema Zanzibar imebarikiwa kuwa na mazingira mazuri ya kuwekeza katika bahari ili kukuza uchumi na kuongeza pato la taifa nao watatoa kila aina ya ushirikiano ili kuhakikisha bahari inakuwa bora na usalama wakati wote.

Alisema Zanzibar imefanya jambo la busara kwa kuanzisha Wizara ya Uchumi wa Buluu ili kuifanya bahari kuwa kiungo cha kuongeza ajira kwa vijana.



# Wananchi waomba elimu kukabiliana ukatili kijinsia

**Na Shaban Njia,**
SHINYANGA

WANANCHI wa Kata ya Lyamidati, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wameomba kupewa elimu kuhusu upatikanaji wa fomu namba tatu inayotolewa na polisi (PF3) katika ofisi za kata.

Wamesema hatua hiyo itasaidia kukabiliana na vitendo vilivyokithiri vya ubakaji wa watoto wa chini ya miaka 18 pamoja na wanawake ili wajue wapi wanatakiwa kupeleka malalamiko yao wanapofanyiwa ukatili huo.

Hayo waliyabainisha jana mjini hapo wakati wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti.

Mkazi wa Kijiji cha Ihungi, Anita Joramu, alisema hawafahamu hatua za kufuata wanapofanyiwa ukatili wa kubakwa hususani namna ya kupata fomu namba tatu kwa ajili ya kwenda hospitali kupata matibabu.

Alisema wanawake wengi wanapofanyiwa ukatili huo wanaoga na kupoteza ushahidi ambao ungeisaidia mahakama kuwatia hatiani watuhumiwa.

"Matukio haya yanapojitokeza wakati tunajiandaa kwenda kutoa taarifa kwa mtendaji wetu, tunaoga kwanza na tunapofika tunaambiwa tumeharibu ushahidi kwa kuwa tulipaswa kuchukulia vipimo kabla ya kujitakasa na haya tunayafanya kwa sababu hatujui," alisema Joramu.

Chausiku Vumilia, mkazi wa kijiji cha Mwabasi alisema hawafahamu namna ya kuwasilisha ushahidi wa matukio ya ukatili wa kijinsia katika vyombo vya sheria.

Alisema kwa kuwa hawajui wanajikuta wakipoteza ushahidi siku ya kesi wanajificha au kutoroka kwa sababu ya uoga.

Aliomba serikali kuwasaidia katika masuala ya kisheria kwa kuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili watuhumiwa wanawapa vitisho hususani wakati wa kutoa ushahidi mahakamani.

Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Joyce Mahina, aliwashauri wananchi kuondoa uoga wakati wa kutoa taarifa katika ofisi yake.

Akizungumzia suala hilo, Ofisa Maendeleo wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omary, alisema wananchi wanakosa imani baada ya mtuhumiwa kukamatwa na kufikishwa polisi na kisha kuachiwa.

Alisema mtuhumiwa anayo haki ya kupatiwa dhamana na wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wajue utaratibu.

Aliwataka watendaji wa kata kuhakikisha wanawapa mrejesho wananchi kuhusu mashauri mbalimbali yanayoendelea ili wajue yamefikia wapi.

Elimu hiyo inatolewa kwa wananchi kupitia mradi wa Sauti za Kaya na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).



Meneja Mkuu wa Mgodi wa Bulyanhulu, Cheick Sangare (aliyevaa kofia), akikabidhi zawadi ya baiskeli kwa mshindi wa mbio ndefu za kilomita 42, Elias Charles. Mashindano ya Bulyanhulu Healthy Lifestyle Marathon yalifanyika jana katika maeneo ya mgodi huo na kujumuisha wafanyakazi wa mgodi, makandarasi na wakazi wa vijiji jirani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wapanda miti maadhimisho ukatili kijinsia

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MAADHIMISHO ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yamefanyika kwa staili yake katika Kata ya Masengwa, wilayani Shinyanga kwa kupanda miti 65 katika ofisi ya kata na kwenye kaya zao ili kufikisha ujumbe wa kumlinda mtoto wa kike.

Wananchi hao wakiongozwa na Mtendaji wa kata hiyo, Hussen Majaliwa, walifanya maadhimisho hayo ili kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Majaliwa, alisema wameamua kuadhimisha siku hizo 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kwa kupanda miti, huku wakimfananisha mtoto wa kike kama mtu anayepaswa kutunzwa kama mti ili ufikie hatua ya kutoa matunda.

"Mtoto wa kike anapaswa kutunzwa kama mti, ukiumwagilia ni sawa na kumpatia haki yake ya kielimu, ukiulinda usishambuliwe na mifugo ni sawa na kumlinda asitongozwe na wanaume na kuambulia ujauzito, ili atimize ndoto zake sawa na mti kutoa matunda," alisema Majaliwa.

"Wito wangu kwa jamii tumlinde mtoto wa kike kama mti hadi afikie hatua ya kutoa matunda, tuwalinde dhidi ya watu wabaya wala tusiwaozeshe ndoa ya utotoni ili wafikie ndoto zao na kuja kuwa tegemeo katika familia na taifa kwa ujumla," aliongeza.

Aidha, tatizo la mimba kwa wanafunzi katika kata hiyo limekwisha kwa sababu mwaka huu hakuna tukio lililoripotiwa.

Hollo Machiya, mkazi wa kata hiyo, alisema tatizo linalosababisha ukatili dhidi ya watoto wa kike kuendelea katika jamii ni mfumo dume.

Alisema baadhi ya wazazi hawapendi kuwasomesha watoto wa kike huku wakiwageuza vitega uchumi na kuamua kuwaozesha ili wapate utajiri wa mifugo.

# Wataka biashara usafirishaji haramu binadamu ikomeshwe

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WATETEZI wa masuala ya usawa wameiomba jamii kupinga usafirishaji haramu wa binadamu hususani kwa watoto pamoja na kutaka wafanyakazi wa nyumbani kupewa kazi zenye staha.

Hayo yalibainishwa juzi na Meneja wa nyumba salama kutoka Shirika la Wote Sawa, Jaqueline Ngalo, walipoadhimisha Siku ya Ukimwi Duniani.

Alisema watoto wengi wanasafirishwa na kwenda kutumikishwa kwenye kazi za nyumbani na katika biashara za ngono.

Aliongeza kuwa wafanyakazi wengi wa nyumbani wanapitia ukatili wa kingono ambao umewasababishia kupata madhara mbalimbali ikiwamo magonjwa ya zinaa, Ukimwi na wengine kupata mimba zisizotarajiwa.

"Baadhi ya watoto wametumikishwa katika biashara za ngono na kusababisha madhara makubwa ya kiafya huku wengine wakipoteza maisha," alisema Ngalo.

Alisema kuwa shirika hilo limekuwa likiwahamasisha waajiri kuwalinda wafanyakazi wao na kuhakikisha wanafanyakazi katika mazingira mazuri na salama.

Mwanaharakati huyo alisema, wanafanyakazi na wafanyakazi moja kwa moja na kuwapa elimu ya afya ya uzazi kwa sababu wengi wao wanapotoka vijijini kwenda mijini kufanya kazi za nyumbani wanakuwa hawana elimu ya wanavyotakiwa kuishi.

"Wengine wanatoka wakiwa wadogo na waajiri wengi hawachukui nafasi yao ya kuwapa elimu ya afya ya uzazi, hivyo huchangia baadhi yao kupata madhara ambayo ni pamoja kuwasababishia maambukizi ya magonjwa," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alitoa rai kwa jamii kuachana na tabia hatarishi zinazoweza kuchochea maambukizi ya VVU/UKIMWI ili kuepukana na janga hilo.

Alisema kuwa Mkoa wa Mwanza una maambukizi ya asilimia 7.4 ambayo ni zaidi ya asilimia nne ya kitaifa na kwamba kazi iliyo mbele yao ni kuwakinga watoto ambao ni taifa la kesho dhidi ya janga hilo.

Alitoa wito kwa wenye maambukizi kutumia dawa za kufubaza ili kuimarisha afya zao na kuendelea kuzalisha mali na kuboresha maisha yao.

## Iran yavunja kikosi maalumu cha polisi

**TEHRAN,** Iran

MAMLAKA nchini Iran, zimetangaza kukivunja kikosi maalumu cha polisi wa maadili, hatua inayokuja baada ya takribani miezi miwili ya maandamano ya raia, waliokuwa wakipinga mauaji ya msichana Mahsa Amini aliyeuawa akiwa mikononi mwa polisi hao.

Maandamano ya raia dhidi ya polisi hao, yalianza siku chache baada ya taarifa za kuuawa kwa msichana Mahsa Amini, ambaye alikamatwa kwa madai ya kukiuka sheria za mavazi ya wanawake.

Tangu wakati huo, maelfu ya wanawake nchini humo wamekuwa wakijitokeza barabarani, kukashifu polisi hao, huku wakichoma moto hijabu zao na kuimba nyimbo za kuukashifu utawala wa Tehrani.

Kwa mujibu wa mwanasheria mkuu wa Serikali ya Iran, Mohammad Jafar Montazeri, serikali imesikia kilio cha wananchi na kwamba wanakivunja rasmi kikosi hicho alichosema hakina mamlaka kisheria.

Uamuzi huo umepokelewa kwa hisia mseto na mashirika ya kutetea haki za binadamu yanayotaka polisi waliohusika na vitendo vya ukiukaji wa haki za binadamu, kuadhibiwa. **RFI**

## Vikwazo kimataifa vyaendelea kuiumiza Urusi

**WASHINGTON,** Marekani

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken (pichani), amesema vikwazo vya mataifa ya Magharibi kwa Urusi vinaongezeka kila siku na kusababisha kuwa vigumu kwa taifa hilo kutengeneza silaha zaidi ili kuendeleza vita vya Ukraine.

Wakati Urusi ikiwa imewekewa vikwazo vya kibiashara na Marekani pamoja na washirika wake, Blinken alisema kwamba haiwezi kuagiza bidhaa muhimu za kukarabati au kutengeneza silaha zilizoharibiwa wakati wa vita, huku baadhi ya silaha na vifaru vikiachwa na wanajeshi wake baada ya kukabiliwa vikali na vikosi vya Ukraine.



Blinken aliyekuwa akizungumza na televisheni ya CNN katika kipindi cha State of the Union, pia alisema gharama inaendelea kuongezeka kwa Urusi, huku mzigo ukiendelea kuwa mzito kwa taifa hilo.

Pia alisema kwamba washirika wa magharibi wanaendelea kutathmini vikwazo zaidi ili kudumaza juhudi za Urusi zaidi. **VOA**

# OPEC+ yaweka azimio la kupunguza uzalishaji mafuta

**RIYADH,** Saudi Arabia

WANACHAMA wa Umoja wa Mataifa 13 yenye kuzalisha kwa wingi mafuta duniani (OPEC+) yamekubaliana kuendelea kupunguza kiwango cha mafuta wanachokizalisha ili kuendana na hali ya soko duniani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, mataifa yenye nguvu kubwa katika uzalishaji wa mafuta duniani yanayoongozwa na Saudi Arabia na kwa upande mwingine Urusi yamehitimisha mkutano wao kwa kukubaliana kudumisha viwango vyao vya sasa vya uzalishaji wa mafuta.

Makubaliano hayo yalifikiwa baada ya hali ya sintofahamu na ikiwa ni kabla ya kuanza kutekelezwa vikwazo vipya dhidi ya serikali ya Moscow vyenye kutarajiwa kuanza kuanza juma hili.

Mataifa hayo 13 wanachama wa umoja wa OPEC wanaoongozwa na serikali ya Riyadh na washirika wao mataifa mengine 10 yenye kuongozwa na Urusi, kwa ujumla wa mataifa 23 yakijulikana kama OPEC+, ambapo waliamua kuzingatia makubaliano ya Oktoba mwaka huu ya kupunguza uzalishaji wa mapipa milioni mbili kwa siku hadi mwishoni mwa 2023.

**Ilibainishwa kuwa mkutano unaofuata wa ngazi wa uwaziri kwa OPEC+ umepangwa kufanyika mwezi Juni 2023.**

**HATUA ZA DHARURA**

Vile vile, ilielezwa kuwa katika mkutano huo mataifa hayo yalikubaliana kukutana muda wowote kuanzia sasa na kufanya mabadiliko yanayohitajika kwa kutegemea mahitaji ya soko.

Mchambuzi katika masuala ya nishati kutoka Taasisi ya ABN AMRO, Hans van Cleef, alisema uamuzi huo wa mataifa hayo ulitegemewa na kwamba hakukuwa na la kushangaza, ikizingatiwa hali ya kudorora kwa uchumi, hatua ambayo imeshusha bei ya pipa la mafuta kufikia dola 90 pamoja na kupunguzwa huko kwa viwango vya uzalishaji.

Muungano huo wa OPEC+, ulisema uamuzi wake wa Oktoba wa kupunguza uzalishaji ulisukumwa na hali ya soko, na kuongeza kwamba umekuwa lazima kuwapo kwa njia ya lazima na stahiki katika kuleta hali tulivu katika soko kote duniani.

Inaelezwa kuwa, hatua ya upunguzaji wa uzalishaji mafuta kwa mataifa hayo yenye nguvu katika nishati hiyo, inaakisi kiwango kikubwa zaidi cha punguzo tangu kuongezeka kwa janga la UVIKO-19 mwaka 2020, hatua iliyopingwa vikali la Marekani katika makabiliano yake na Urusi.

Ilibainishwa kuwa mkutano unaofuata wa ngazi wa uwaziri kwa OPEC+ umepangwa kufanyika mwezi Juni 2023. Huku muungano huo ukisema uko tayari kukutana wakati wowote na kuchukua hatua za ziada na haraka kushughulikia mwenendo wa soko na kusaidia soko la mafuta ikiwalazimu.

Hata hivyo, Ijumaa iliyopita Umoja wa Ulaya (EU), na nchi tajiri yaani G7 na Australia zilikubaliana kuweka ukomo wa bei ya mafuta kwa mafuta ya Urusi. Pia zilikubaliana bei ya kikomo iwe dola 60 kwa pipa ambayo ilipendekezwa kutumia kuanzia wiki hii au baadaye kidogo baada ya kuanza kutekelezwa marufuku ya usafirishaji wa mafuta ghafi ya Urusi.

Marufuku hiyo itazuia usafirishaji wa mafuta ghafi ya Urusi kupitia bahari kuelekea ulaya ambayo yanakadiriwa kuwa theluthi mbili ya uagizaji wa umoja huo, jaribio ambalo linalengo la kuipunguzia serikali ya Urusi nguvu ya kifedha, katika kushiriki vita vya Ukraine kwa kukosa mabilioni ya Euro. **DW**



Waumini wa Kanisa Katoliki nchini Congo (DRC) wakiongoza maandamano kupinga waasi wa M23. **PICHA: BBC**

# DRC yatangaza siku 3 za maombolezo

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ametangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa kwa waathiriwa wa mauaji yanayodaiwa kutokea mashariki mwa nchi hiyo.

Inaelezwa kuwa ni hatua isiyo ya kawaida baada ya miaka mingi ya machafuko katika eneo hilo, ambapo Felix Tshisekedi, alisema zaidi ya watu 100 wameuawa katika kijiji cha Kishishe.

Pia aliwalaumu waasi wa M23 kwa mauaji hayo, jambo ambalo wanalikanusha, huku ikibainishwa kwamba kumekuwa na milipuko ya ghasia kali tangu DRC na Rwanda kukubaliana kusitisha mapigano wiki iliyopita.

DRC, Marekani na Umoja wa Mataifa (UN) zimeishutumu Rwanda kwa kuunga mkono kundi la M23, huku Kigali ikikanusha madai hayo.

Vile vile, inaelezwa kuwa kuna juhudi za kuleta amani mashariki mwa nchi hiyo zinazoendelea nchini Kenya, na kwamba tayari mataifa ya kanda ya Afrika Mashariki yametuma vikosi ili kupambana na makundi yenye silaha nchini DRC. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1107 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late**
**FRANK ERASTO MBUNDA**
**and**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**EUNICE ARTHUR CHITEMBO, ASHERI FRANK MAPUNDA AND JOFREY DENICY MAPUNDA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 27TH day of January, 2023

Dated at DAR ES SALAAM this 30th day of November, 2022.

............................................
*Senior Resident Magistrate*

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANITHA NEEMA MAGNUSON,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha Sita chenye Index No S.4084-0507 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia shule ya NYAILIGAMBA SECONDARY SCHOOL Mwaka 2019. Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi.
**TAARIFA YA POLISI: DOD/DOD/RB/467531/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIAS MICHAEL MJENGI**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLLA** yenye usajili namba:**T 651 AJH**, CHASSIS NAMBA: **AE1115055384** na ENGINE NAMBA: **4AM206322**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/469701/2022**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 69/2014**
**BENEDICT MABALANGANYA ––––- MUOMBAJI**

**DHIDI YA**
1. **ROMWALD SANGA**
2. **NYAMAKO AUCTION MART**
3. **THE REGISTERED TRUSTEES OF THE ROMAN CATHOLIC ARCHDIOCESE OF SONGEA**
4. **HALIFA NIHAMBA –––––– WAJIBU MAOMBI.**

**WITO/KUITWA SHAURINI**
Mjibu maombi namba Moja unataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako .Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako ,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 19/12/ 2022 saa 2.00 asubuhi kusikiliza Hukumu hapa Barazani.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusoma Hukumu upande mmoja bila kujali uwepo wako.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo 29/11/2022.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**SONGEA.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SINGIDA**
**LILILOPO SINGIDA**
**Shauri la maombi madogo na. 175 ya 2018**
**MWANAHAMISI SELEMANI.......MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**JOHN MOHAMED HONGOA.......MJIBU MAOMBI NA. 1**
**IBRAHIM GHAMBI.........MJIBU MAOMBI NA. 2**
**JUMANNE ISSA.........MJIBU MAOMBI NA. 3**
**SALUMU ATHUMAN.........MJIBU MAOMBI NA. 4**
**HASSAN SHABANI.........MJIBU MAOMBI NA.5**
**AHMED DAUDI.........MJIBU MAOMBI NA. 6**
**KWA: JOHN MOHAMMED HONGOA**
**NA**
**AHMED DAUDI, POPOTE WALIPO TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI:**
Kwa kuwa muombaji tajwa hapo juu ameleta maombi yake hapa hapa barazani ambayo maelekezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi, ambayo yanaweza kupatikana katika baraza hili. Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria hapa barazani tarehe 12/12/2022 saa 2:00 asubuhi siku ya kutajwa kwa shauri hilo.
Mnatakiwa muhudhurie wenyewe au wawakilishi wenu wanaotambuliwa kisheria siku na saa tajwa hapo juu.
ANGALIA: Kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itapangwa na kusikilizwa ikiwa na wajibu maombi namba 2,3,4 na namba 5 tu na uamuzi kutolewa bila ya nyie au wawakilishi wenu kuwepo.
**HATI** hii imetolewa kwa AMRI yangu na **CHAPA** ya **BARAZA** hii leo tarehe 29 Mwezi wa Novemba, mwaka 2022.

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 136 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late**
**MWIGULU KINYAU MADALLA**

**By 1. NAZAEL AMOS MADALLA**
**2. .................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **13rd** day of **December / 2022.**
Dated at **Morogoro**, this **1st** day of **DECEMBER 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 135 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late**
**SERGIO FALAMEO KAKINGO**

**By 1. ZIADA SERGIO KAKINGO**
**2. .................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **13rd** day of **December / 2022.**
Dated at **Morogoro**, this **1st** day of **DECEMBER 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AMINI MUSSA KILUWA**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC876CXY.**
Chasses Namba **MD6M14PA2M4D07295,** Engine Namba **AK4DM4407030**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
**Polisi Taafifa :**
**KIL/MOS/RB/461269/2022**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MBINGA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 68/2021**
**Makisensia Mbele -MRUFANI**
**DHIDI YA**
**Emmanuel Mbele - MRUFANIWA**

**WITO WA KUITWA SHAURINI**

**MDAIWA Emmanuel Mbele POPOTE ALIPO .**
BW/BI, Makisensia Mbele amefungua Shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo (Boma) Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 12 /12/2022 Hivyo basi unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili kutolewa.Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Mbinga ,endapo hutatekeleza haya Shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo hii tarehe 18 mwezi 10 mwaka 2022.

____________
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DIANA ERNEST MWAKADINDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2376/0016 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MUGABE SECONDARY SCHOOL mwaka 2011. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**DAR/KIM/RB/439951/2022**

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Dimpoz, Sultan wamwomboleza mpenzi wao

**Na Mwandishi Wetu**

WASANII Ommy Dimpoz na Idris Sultan, wanaomboleza kifo cha mpenzi wao wa zamani ambaye ni mfanyabiashara wa vipodozi, Maya Mia, aliyefariki kwa kujipiga risasi.

Mia aliwahi kuwa na mahusiano ya kimapenzi kwa nyakati tofauti na mchekeshaji Sultan na mwimbaji Dimpoz.

Mia ambaye ni raia wa Macedonia ambaye kwa sasa alikuwa akiishi nchini Afrika Kusini, alichumbiana na Sultan mwaka wa 2018 na baadaye mwaka 2020 akawa na uhusiano wa kimapenzi na Ommy Dimpoz.

Mia alizaliwa Macedonia, lakini alikuwa ameishi Tanzania kwa zaidi ya mwongo mmoja.

Dimpoz alithibitisha kifo cha mpenzi huyo wake wa zamani na kumwomboleza akichapisha picha kadhaa za kumbukumbu zao.

"R.I.P mpenzi wangu," aliandika Dimpoz na kuambatanisha ujumbe wake na emoji inayoashiria kuvunjwa moyo.

Pia alibadilisha picha yake ya Instagram na kuweka selfie yake na marehemu Maya wakiwa pamoja.

Sultan aliweka video ya kumbukumbu zake maalum na kuandika "Innalillahi wainna illaihi rajighun."



# AKOTHEE AJIVUNIA MPENZI MZUNGU



**Nairobi,** Kenya

MWIMBAJI na mjasiriamali wa Kenya, Esther Akothe maarufu Akothee, ameendelea kujigamba kuhusu mahaba na mchumba wake mzungu.

Wikendi aliandamana na mzungu huyo kwenye hafla ya Pwani Golden Awards ambayo iliandaliwa jijini Mombasa.

Akothee alibainisha kuwa mpenzi wake huyo kijana alichagua kuwa pale kwa ajili yake.

"Eish, anafanya nijisikie mchanga," aliandika. Nitakulinda, nitakuwa hapo kwa ajili yako, ninajivunia wewe."

Mwimbaji huyo mwenye umri wa miaka 42, ambaye alikuwa amealikwa kutumbuiza katika hafla hiyo ya Jumamosi, pia alijivunia jinsi waandishi wa habari walivyotaka sana kumhoji yeye na mpenzi wake.

Akothee alimtambulisha mzungu huyo kama mpenziwe mpya mnamo Septemba, miezi kadhaa baada ya kutengana na Nelly Oaks.

# *Foby afunguka madai ya kulelewa*

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva, Foby, amefungukia madai ya kuwa alikuwa akiishi na mzungu ambaye ndiye alikuwa akimweka mjini.

Foby amefunguka hayo alipokuwa akifanya mahojiano kuhusu wimbo wake mpya unaokwenda kwa jina la 'Emoj' ambapo alitumia nafasi hiyo kumwongelea pia mzungu huyo ambaye alikuwa mpenzi wake.

Alisema mzungu huyo ambaye kwa sasa wameshaachana naye, kwake hakuwa akilelewa zaidi ya wao kushea na kwamba ndiye mpenzi wake wa kwanza.

"Nilimpenda kweli na hakuwa akinipa fedha, hadi bili tulikuwa tunashea. Mnaweza mkatoka out mkishakula anakuambia kabisa leo zamu yako kulipia," alisema Foby.



# SABABU MKWASA KUACHANA NA RUVU SHOOTING HIZI HAPA

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Boniface Mkwasa, ametangaza kujiuzulu kuifundisha timu hiyo kutokana na mwenendo usioridhisha wa timu hiyo ambayo imecheza mechi 10 mfululizo bila kupata ushindi.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkwasa alisema ameamua kukaa kando baada ya kuona falsafa anazozitoa kwenye kikosi chake hazieleweki vema na wachezaji, hivyo kuifanya timu hiyo isifanye vizuri.**

Mkwasa ameamua kubwaga manyanga siku mbili tu baada ya kupokea kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida, Jumamosi, akiwa ameiongoza timu hiyo mechi zote za mzunguko wa kwanza, ikishinda tatu, sare mbili na kupoteza michezo 10.

"Tumejitahidi kufundisha, nimejitahidi kuweka falsafa, lakini kila tukiingia kuna makosa yanafanywa tunafungwa, labda falsafa zangu hazieleweki vema, kwa hiyo nimeamua kukaa pembeni ili atafutwe mtu ambaye anaweza kuendelea nayo. Maana kushindana ni kwamba ushinde na wewe ushindwe, lakini kushindwa kila mechi ni tatizo," alisema Mkwasa.

Mara ya mwisho Ruvu Shooting kushinda ilikuwa Septemba 29, mwaka huu ilipoichapa Coastal Union mabao 2-1, lakini baada ya hapo imecheza mechi 10 mfululizo bila kupata ushindi, ikifungwa nane na sare mbili.


Baada ya kupata ushindi dhidi ya Coastal, ilichapwa mabao 2-1 dhidi ya Yanga, ikatoka suluhu dhidi ya KMC, ikapokea kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Kagera Sugar na ikafungwa kwa idadi hiyo hiyo ya mabao dhidi ya Gaita Gold.

Kama vile haitoshi ikaruhusu kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Mbeya City, ikatoka sare ya 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons.

Baada ya sare hiyo, Ruvu Shooting ikapokea vipigo vingine vinne mfululizo na kumfanya Mkwasa aamue kujiweka kando, ambavyo ni dhidi ya Azam ilifungwa bao 1-0, ikararuriwa mabao 4-0 dhidi ya Simba, bao 1-0 dhidi ya Singida Big Stars, kabla ya Jumamosi kupoteza tena 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji.

Timu hiyo ipo nafasi ya 15 katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 11 na tayari imemaliza mechi zake15 za mzunguko wa kwanza.

HESABU...




Winga wa Yanga, Tuisila Kisinda, akipiga hesabu ya kuwapenya walinzi wa Tanzania Prisons kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na kumalizika kwa wenyeji kushinda bao 1-0. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Ubora Simba Queens waitisha JKT Queens

Na Saada Akida

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens wanafungua rasmi pazia la ligi hiyo leo wakiwakaribisha Maafande wa JKT Queens katika Uwanja wa Mo Simba Arena ulioko Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Simba Queens wanashuka dimbani wakijivunia usajili walioufanya kwa kuimarisha safu yao ya ushambuliaji inayoongozwa na mchezaji bora wa CECAFA, Vivian Corazone, akisaidiana na Oppa Clement na Jentrix Shikangwa.

Wekundu wa Msimbazi hao wanahitaji kuendelea kutawala ligi hiyo kwa kuhakikisha wanapata pointi tatu katika mchezo huo dhidi ya wageni wao, JKT Queens.

Kuelekea mchezo huo wa leo, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kuanza vizuri msimu kwa kusaka ushindi katika mchezo huo.

Alisema anajivunia kuwa na wachezaji wazuri na bora watakaoweza kumpa pointi na anaimani amepata timu ya ushindani ambayo itamletea matokeo chanya katika michezo iliyoko mbele yao ili kufikia malengo waliyojiwekea.

"Wachezaji wangu wako tayari kwa ajili ya kupambania timu kupata matokeo mazuri, mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu tunahitaji ushindi na wapinzani wetu nao wanahitaji matokeo pia," alisema Lukula.

Alisema watacheza mchezo huo kwa nidhamu na kuwaheshimu wapinzani wao ili kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo wanayoanzia nyumbani.

Kocha Mkuu wa JKT Queens, Haule Grayson, alisema wamefanya maandalizi mazuri, kuelekea mechi hiyo ambayo alidai itakuwa ngumu kwa sababu ya ubora wa Simba Queens pamoja na ushiriki wao kwenye michuano ya kimataifa.

Alisema baada ya maandalizi ya uwanjani wamelazimika kuwaandaa wachezaji wao kisaikolojia kwa kuwaondoa hofu juu ya ubora wa wapinzani wao.

"Utakuwa mchezo mgumu kwa sababu Simba Queens imetoka katika mashindano makubwa na kufanya vizuri, hatuwaogopi zaidi ya kuwaheshimu na kwenda kusaka pointi tatu mbele ya wenyeji wetu," alisema Haule.

## Singida Big Stars kusajili majembe

Na Hadija Mngwai

SINGIDA Big Stars imedhamiria kufanya vizuri katika Ligi Kuu Bara msimu huu ili kuweza kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa, na katika hilo imepanga kuongeza nyota wengine kwenye usajili wa dirisha dogo linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu.

Singida Big Stars ambayo ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ina nyota 12 wa kigeni na sasa inahitaji kuimarisha kikosi chake katika usajili wa dirisha dogo.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, alisema tayari Kocha Mkuu, Hans van Pluijm, amewasilisha ripoti ya nyota anaowahitaji kusajiliwa, kwa uongozi na sasa anasubiri utekelezaji tu baada ya dirisha kufunguliwa.

"Kocha amewasilisha ripoti kwa uongozi ya kuhitaji kuongeza wachezaji kadhaa katika timu na kwa sasa ripoti hiyo inafanyiwa kazi ambayo inaonyesha maeneo yanayotakiwa kufanyiwa kazi," alisema Massanza.

## Bonnah Segerea Cup kuanza J'pili

Na Shufaa Lyimo

MASHINDANO ya Bonnah Segerea Cup yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Jumapili wiki hii katika viwanja mbalimbali vya Jimbo la Segerea.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mbunge wa Jimbo la Segerea, Bonnah Kamoli, alisema michuano hiyo itachezwa kwenye viwanja nane vilivyoko jimboni hapo.

Mbunge huyo alisema mashindano hayo yatachezwa kwa mfumo wa mtoano na kudai mshindi wa kwanza ataibuka na kitita cha Sh. 5,000,000, wa pili Sh. 3,000,000 na wa tatu akiondoka na Sh. 2,000,000 wakati mlinda mlango bora akizawadiwa Sh. 50,000.

"Nimeamua kuandaa mashindano haya kwa ajili ya kuinua vipaji vya vijana badala ya kukaa mitaani wanapaswa kujiunga kwenye michezo kwa kuwa inajenga afya," alisema.

Kwa upande wa Mratibu wa timu ya Msimbazi Magharibi (Tabata), Harun Adam, alisema wamejiandaa vizuri kukutana na timu ya Kisiwani (Buguruni) katika mchezo wao wa awali utakaopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Wazazi ulioko Kimanga, Dar es Salaam.

"Timu yetu inaendelea na mazoezi ikiwa chini ya Kocha Mkuu, Yahaya Lwambano, tunaamini tutafanya vizuri katika mchezo wetu huo," alisema Adam.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GAKPO ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United iko tayari kumnunua Cody Gakpo, 23, Januari kwani PSV Eindhoven imekubali kumuuza mshambuliaji huyo kutokana na kiwango chake kizuri kwenye Kombe la Dunia. ***(Sun)***

### BUSQUETS NA BARCA

KLABU ya Barcelona inataka mbadala wa muda mrefu wa kiungo wa kati wa Hispania, Sergio Busquets, 34 na wanavutiwa na Youri Tielemans wa Leicester, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Marca)***

### BELLIRIN KUTUA ROMA

MLINZI wa Hispania, Hector Bellerin, 27, anakaribia kujiunga na AS Roma kwa mkopo kutoka Barcelona. ***(Clciomercato)***

### LEAO NAYE ATAKIWA

MANCHESTER United watalazimika kulipa pauni milioni 50 kumnunua Cody Gakpo - mara mbili ya ile PSV ilitaka msimu wa majira ya joto - hivyo huenda ikaelekeza mawazo yao kwa mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao, 23. ***(Mirror)***

### MADRID NAO WAJITOSA

RAFAEL Leao alitarajiwa kujiunga na Real Madrid msimu wa majira ya joto, lakini sasa analengwa kama shabaha ya 2024 na mabingwa hao wa Hispania, wengine ni mshambuliaji wa Manchester City na Norway, Erling Haaland, 22 na mshambuliaji wa Palmeiras, Mbrazil Endrick, 16. ***(Sport)***

### KUDUS AWANIWA BARCA

BARCELONA wanamtaka Mohammed Kudus, 22, lakini kiungo huyo wa kati wa Ghana yuko tayari kuhamia Ligi Kuu England na huenda Ajax wakataka euro milioni 40. ***(Sun)***

### CUNHA AGOMBEWA EPL

KLABU za Everton na Leeds United zimeungana na Aston Villa na Wolves katika kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid na Brazil, Matheus Cunha, 23. ***(Relevo)***

### JESUS NJE MIEZI MITATU

GABRIEL Jesus amerejea London na atajua ukubwa wa jeraha lake kutokana na mashauriano na madaktari wa Arsenal, huku baadhi ya ripoti zikisema atakuwa nje kwa miezi mitatu. ***(Sun)***

### KESSIE AFUATILIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imeungana na Aston Villa, Fulham na Inter Milan kufuatilia hali ya kiungo wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie, 25, katika klabu ya Barcelona. ***(Mundo Deportivo)***

### FELIX KUONGEZA THAMANI

KLABU ya Atletico Madrid inatumaini, Joao Felix, 23, anaweza kuongeza thamani yake wakati huu wa Kombe la Dunia kabla ya kutaka kumuuza. ***(Marca)***

### KONE KUTUA WATFORD

KLABU ya Watford iko mbioni kukamilisha usajili wa kiungo wa Canada, Ismael Kone, 20 kutoka CF Montreal kwa mkataba wa miaka minne na nusu. ***(Mirror)***

## DONDOO ... A MAGAZETI ... YA




# SOUTHGATE AWAVULIA KOFIA WACHEZAJI VIJANA ENGLAND

**DOHA,** Qatar

●●● Bukayo ana mechi 20 ambazo zinakuja kwenye mashindano kama haya, tulitaka...

GARETH Southgate amewasifia wachezaji vijana kwa kuiwezesha England kupata ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya Senegal na kutinga robo fainali ya Kombe la Dunia 2022.

**Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, alikuwa kwenye orodha ya asisti huku Bukayo Saka na Phil Foden - waliochaguliwa mbele ya Marcus Rashford na Jack Grealish - wakichangia ushindi huo wa England kwenye Uwanja wa Al Bayt nchini Qatar.**

Matokeo hayo yanaifanya England kukabiliana na bingwa mtetezi wa michuano hiyo, Ufaransa kwenye robo fainali, Jumamosi.

Bellingham na Foden mwenye umri wa miaka 22, walitengeneza pasi za mabao mawili ya kwanza ya England, yaliyofungwa na Jordan Henderson na Harry Kane, huku Saka mwenye umri wa miaka 21, akifunga la tatu kutokana na krosi nyingine ya Foden.

Ilikuwa ni usiku wa kuridhisha kwa kocha Southgate, huku Bellingham ikionyesha kiwango cha kuvutia zaidi.

"Sidhani kama tungeweza kutabiri jinsi angepevuka haraka, hata katika miezi mitatu iliyopita ambayo imekwenda kwa kiwango kingine," alisema Southgate kuhusu kiungo huyo wa Borussia Dortmund.

"Tulitaka kuwekeza kwa wachezaji wachanga kwa msingi ambao tulihisi wanaweza kuwa kitu maalum katika siku zijazo. Inamaanisha kuwa watu kama Bukayo ana mechi 20 ambazo tayari zinakuja kwenye mashindano kama haya."

Ufaransa itatoa changamoto tofauti kabisa na Senegal na Southgate anakipenda sana kikosi cha Didier Deschamps.

"Ni mtihani mkubwa tunaoweza kukumbana nao," alisema Southgate. "Ni mabingwa wa dunia, wana vipaji vya ajabu na wachezaji bora ambao ni vigumu sana kucheza nao. Ni changamoto kubwa."

Kylian Mbappe alifunga mabao mawili katika ushindi wa 3-1 wa Ufaransa dhidi ya Poland mapema Jumapili na kumfanya afikishe mabao matano kwenye michuano hiyo, na ndiye atakuwa mtu ambaye England itapaswa kumtazama kwa karibu zaidi.

Southgate alisema: "Yeye ni mchezaji wa kiwango cha kimataifa, tayari amefanya matukio makubwa katika mashindano haya na mashindano mengine.

"Pia wana (Antoine) Griezmann ambaye ameichezea Ufaransa zaidi ya mechi 70 mfululizo, ni mchezaji wa ajabu, tunamfahamu Olivier Giroud vizuri, na wana wachezaji bora wa kati vijana."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 417

MECHI KALI
MOROCCO
VERSUS
SPAIN
1 | 6.19
X | 3.64
2 | 1.58

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GIROUD AVUNJA REKODI YA UFUNGAJI UFARANSA



**DOHA,** Qatar

OLIVIER Giroud aliingiza jina lake kwenye vitabu vya historia ya Ufaransa alipokuwa mfungaji bora wa muda wote wa 'Les Bleus' hao baada ya kutikisa nyavu dhidi ya Poland kwenye Kombe la Dunia.


Bao hilo limemfanya Giroud kufikisha mabao 52 aliyoifungia Ufaransa na kumpiku Thierry Henry.

Mshambulizi huyo wa AC Milan, alifikia rekodi ya Henry ya mabao 51 kwa mabao mawili katika ushindi wa 4-1 dhidi ya Australia katika mechi ya kwanza ya Kombe la Dunia la taifa lake.

Giroud, mwenye umri wa miaka 36 na siku 53, sasa ni mchezaji wa pili kwa umri mkubwa kufunga mabao mawili kwenye Kombe la Dunia, baada ya Roger Milla, aliyefanya hivyo mwaka 1990 akiwa na Cameroon, wakati huo akiwa na umri wa miaka 38.

Giroud alivunja rekodi hiyo kwa kufunga bao la kwanza katika mechi ya hatua ya 16-bora dhidi ya Poland, akiunganisha pasi ya Kylian Mbappe na kuwatangulia Les Bleus.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Chelsea na Arsenal huenda hangeanza kuichezea timu ya Didier Deschamps kama isingekuwa majeraha ya Karim Benzema na Christopher Nkunku kabla ya michuano hiyo.



# Lewandowski: Naweza kucheza mpaka 2026

**DOHA,** Qatar

ROBERT Lewandowski "haogopi" kucheza kwenye Kombe lingine la Dunia, lakini nahodha huyo wa Poland alikiri kuwa timu yake inahitaji mabadiliko katika mbinu.

Fowadi huyo alishuhudia timu yake ikichapwa 3-1 na Ufaransa katika mchezo wao wa hatua ya 16-bora na kuondoka nchini Qatar.

Lewandowski alifunga bao lake la pili la michuano hiyo kwa mkwaju wa penalti likiwa ni la kufutia machozi kwa Poland.

Lakini alipoulizwa kama bado atakuwa kwenye mfumo wa kushiriki katika michuano ya mwaka 2026 wakati ambapo atakuwa na umri wa miaka 37, -mkongwe huyo alisema haogopi.

"Kuna mambo mengi ya kusimamia kwanza. Ni vigumu kusema kwa sasa. Kiuchezaji, hainitishi, lakini bado kuna mambo mengi ya ku tokuwa na uhakika."

"Bado ni safari ndef na ni wazi, unahitaji ku furahia mchezo," alisema.

"Tukishambulia, tuk jaribu kushambulia, tofauti kidogo. Lakin tukicheza kwa kujilind hakuna furaha."

Lewandowski am kubali kwamba kiko chao kitakuwa na pan bano kila mara mikon ni mwao, akiongeza: "N mechi ngumu, kuchez dhidi ya Ufaransa."

## HABARI MICHEZO

,515,870

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 07/12/22 | 21:00 | Huesca vs FC Andorra | 2.57 | 2.87 | 2.92 |
| 2. 07/12/22 | 23:00 | Tenerife vs Alaves | 2.46 | 2.83 | 3.13 |
| 3. 08/12/22 | 16:00 | Burgos vs Eibar | 2.98 | 2.93 | 2.48 |
| 4. 08/12/22 | 17:00 | Modena vs Venezia | 2.34 | 3.12 | 3.02 |
| 5. 08/12/22 | 17:00 | Reggina vs Frosinone | 2.63 | 2.78 | 2.93 |
| 6. 08/12/22 | 17:00 | Cittadella vs Bari | 2.46 | 2.92 | 3.02 |
| 7. 08/12/22 | 18:15 | Lugo vs Sporting Gijon | 2.93 | 3.08 | 2.42 |
| 8. 08/12/22 | 20:30 | UD Ibiza Eivissa vs Racing Santander | 2.62 | 2.97 | 2.77 |
| 9. 09/12/22 | 11:45 | Brisbane Roar vs Adelaide United | 2.45 | 3.48 | 2.63 |
| 10. 09/12/22 | 21:30 | Villefranche Sur Saone vs Chateauroux | 2.39 | 3.15 | 3.00 |
| 11. 09/12/22 | 21:30 | Sedan vs Cholet | 2.34 | 3.15 | 3.10 |
| 12. 09/12/22 | 21:30 | Avranches vs Nancy | 2.30 | 3.10 | 3.05 |
| 13. 09/12/22 | 22:00 | Netherlands vs Argentina | 3.35 | 3.15 | 2.21 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 06/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2040 | Fuenlabrada vs Merida UD | 2.15 | 3.06 | 3.25 |
| 14:00 | 2063 | Unionistas CF vs Alcorcon | 2.98 | 3.08 | 2.28 |
| 14:00 | 4119 | Ethiopia Bunna SC vs Hadiya Hosahina FC | 2.83 | 2.54 | 2.83 |
| 14:30 | 1274 | Persis Solo vs Rans Nusantara | 2.20 | 2.92 | 3.31 |
| 14:30 | 1848 | Persija Jakarta vs Pusamania Borneo | 2.22 | 3.10 | 3.05 |
| 15:30 | 1641 | CO Mednine vs ES Jerba Midoun | 2.62 | 2.62 | 2.96 |
| 15:30 | 1926 | CS Korba vs CS Bembla | 2.09 | 2.58 | 4.29 |
| 15:30 | 4150 | CD Mensajero vs Lanzarote | 1.69 | 3.35 | 4.76 |
| 15:30 | 5824 | ES Rades vs JS Kairouanaise | 2.40 | 3.06 | 2.81 |
| 15:45 | 5462 | Al Masry Club vs National Bank | 2.05 | 3.09 | 3.79 |
| 16:00 | 4537 | Adama City FC vs Legetafo Legedadi | 1.47 | 3.65 | 6.82 |
| 16:00 | 4544 | ND Gorica vs ASK Bravo | 3.26 | 3.16 | 2.10 |
| 16:30 | 5043 | Churchill Brothers vs Mohammedan SC | 2.81 | 3.25 | 2.29 |
| 17:00 | 5965 | Wolkite City FC vs Ethiopian Medhin | 2.77 | 2.97 | 2.48 |
| 18:00 | 1316 | Qalali vs ISA Town | 2.83 | 3.21 | 2.30 |
| 18:00 | 1502 | Morocco vs Spain | 6.19 | 3.64 | 1.58 |
| 19:00 | 3066 | Bahir Dar Kenema FC vs Saint George FC | 4.19 | 3.02 | 1.89 |
| 20:00 | 2202 | Unirea Slobozia vs Dinamo Bucuresti | 2.58 | 3.02 | 2.63 |
| 20:00 | 4644 | Petrolul Ploiesti vs U Craiova SA | 2.77 | 3.06 | 2.43 |
| 20:00 | 4803 | Maribor vs NK Radomlje | 1.45 | 4.18 | 5.84 |
| 20:00 | 5677 | Sepsi Osk vs Voluntari | 1.86 | 3.16 | 4.08 |
| 21:00 | 1579 | Real Oviedo vs Las Palmas UD | 3.08 | 2.88 | 2.45 |
| 21:00 | 5353 | Leganes vs Mirandes | 1.99 | 3.07 | 3.96 |
| 22:00 | 2095 | Portugal vs Switzerland | 1.91 | 3.30 | 4.10 |
| 22:00 | 4567 | CD Badajoz vs Deportivo La Coruna | 3.51 | 3.12 | 2.03 |
| 22:45 | 1161 | Kettering Town vs Gloucester City | 2.78 | 3.26 | 2.31 |
| 22:45 | 1182 | Spennymoor Town vs Boston Utd | 2.28 | 3.26 | 2.82 |
| 22:45 | 1525 | Hereford United vs Chorley | 2.52 | 3.25 | 2.52 |
| 22:45 | 1869 | Worthing vs Ebbsfleet | 3.60 | 3.55 | 1.85 |
| 22:45 | 2268 | Hemel Hempstead vs Bath City | 2.26 | 3.31 | 2.82 |
| 22:45 | 2396 | Cheshunt vs Dover | 2.97 | 3.36 | 2.14 |
| 22:45 | 2458 | Curzon vs Darlington | 2.49 | 3.22 | 2.58 |
| 22:45 | 2512 | Cliftonville Belfast vs Coleraine FC | 2.00 | 3.35 | 3.31 |
| 22:45 | 2829 | Halifax vs Dorking Wanderers | 1.98 | 3.60 | 3.30 |
| 22:45 | 2855 | Boreham Wood vs Oldham | 1.86 | 3.40 | 3.94 |
| 22:45 | 2936 | Bracknell Town vs Plymouth Parkway | 1.72 | 4.26 | 3.54 |
| 22:45 | 3285 | Needham Market vs Hednesford Town | 1.96 | 3.55 | 3.26 |
| 22:45 | 3723 | Yate Town vs Chesham Utd | 3.16 | 3.79 | 1.92 |
| 22:45 | 3806 | Glentoran Belfast vs Linfield Belfast | 2.25 | 3.20 | 2.91 |
| 22:45 | 4001 | Whitby Town vs Hyde United FC | 2.68 | 3.31 | 2.36 |
| 22:45 | 4326 | Marske United FC vs Liversedge | 1.79 | 3.69 | 3.69 |
| 22:45 | 4393 | Basford United vs Kings Langley | 1.89 | 3.55 | 3.45 |
| 22:45 | 4448 | Rushall Olympic vs Leiston | 2.28 | 3.41 | 2.72 |
| 22:45 | 5031 | Coalville Town vs Nuneaton | 1.83 | 3.79 | 3.45 |
| 22:45 | 5087 | Hastings United vs Canvey Island | 2.10 | 3.47 | 2.98 |
| 22:45 | 5435 | Braintree vs Oxford City | 3.06 | 3.40 | 2.09 |
| 22:45 | 5483 | Farsley Celtic vs Kings Lynn | 4.28 | 3.60 | 1.70 |
| 22:45 | 5972 | Alvechurch vs Stratford Town | 1.72 | 3.88 | 3.84 |
| 23:00 | 4709 | Albacete Balompie vs Zaragoza | 2.43 | 3.02 | 2.97 |
| 23:45 | 2947 | GD Estoril vs SCU Torreense | 1.73 | 3.51 | 4.19 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# LIGI KUU WANAWAKE Z'BAR KUANZA KESHO, NNE ZAJITOA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu ya Wanawake Zanzibar kwa msimu wa 2022/23, inatarajia kuanza kutimua vumbi kesho, Jumatano kwa Mabingwa Watetezi, Warriors Queens kuwakaribisha UMZ Queens katika mchezo utakaopigwa Dimba la Mau Ze Dong majira ya saa kumi alasiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Soka la Wanawake wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Khatma Mwalimu, alisema katika msimu huu jumla ya timu saba ndizo zitakashiriki ligi hiyo tofauti na msimu uliopita ambao ulikuwa na timu 10.

Alisema timu nne ambazo ni Wete Star, Future Queens, Mkoni Queens na Bungi Sisters, zilishindwa kuthibitisha kushiriki ligi hiyo hadi hatua ya mwisho wakati kamati ya mashindano inapanga ratiba.

**Alisema sababu kubwa zilizotajwa na viongozi wa timu hizo ni kukosa wafadhali wa kuwasaidia fedha za kuendesha timu hizo hususan katika kipindi cha ligi.**

Mwalimu alisema kwa upande wa timu mbili za Pemba, Mkoni Queens na Wete Star nazo zimeshindwa kumudu gharama za usafiri pamoja na malazi katika kipindi chote watakachokuwa Unguja kwa ajili ya ligi hiyo.

Aidha, alisema kamati hiyo kwa kushirikiana na ZFF walijitahidi kuhakikisha wanawatafutia watu ambao watazisaidia timu hizo, lakini ilishindikana.

"Tunacheza ligi tukiwa na timu saba tu, timu nne zimeshindwa kwa kuwa hazina fedha kama unavyojua kwa Zanzibar timu za wanawake wasimamizi ni wanawake wenyewe na uchumi wao unajulikana, hivyo inakuwa vigumu kumudu gharama zote za uendeshaji timu peke yao," alisema.

Timu zitakazocheza ligi hiyo msimu huu ni Warriors Queens, New Generation, UMZ Queens, Yellow Queens, Green Queens, Dunga Queens huku ingizo jipya likiwa ni PDS Princess.



Kylian Mbappe (kulia), akimpongeza Olivier Giroud baada ya kuifungia Ufaransa bao la kwanza kabla ya yeye kutupia mengine mawili na kuiwezesha kushinda 3-1 dhidi ya Poland kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia nchini Qatar juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yataka 12 kufunga mwaka

INATOKA UKURASA 32

pungufu na kuimarisha ubora ulioko ndani ya kikosi hicho ili kuhakikisha wanaendelea kutafuta pointi kila mechi kwa ajili ya kufikia malengo yao.

"Ligi imekuwa ya ushindani mkubwa, kila timu imejiandaa kutaka kufanya vizuri katika kila mechi, tunahitaji kupambana na kujitoa ili kufikia malengo yetu ya kushinda michezo iliyoko mbele yetu kwa kupata pointi 12 na kushinda mchezo wa FA," alisema Mgunda.

## *Mayele airudisha Yanga sokoni*

INATOKA UKURASA 32

wa kuzitumia.

Alisema wachezaji walipambana katika kipindi cha kwanza na kuwazuia Yanga wasipate nafasi ya kufika langoni mwao, lakini kutokuwa makini kwa mabeki wao ndio sababu ya kuruhusu bao hilo.

"Tulitengeneza nafasi kipindi cha kwanza lakini vijana wangu hawakuwa makini, kwetu haikuwa siku nzuri, Yanga walituzidi umakini na kumiliki mpira, kutafuta mianya ya kutafuta bao na walifanikiwa kupata ushindi," alisema Mtupa.

Michezo

Jumanne Desemba 6, 2022

Nipashe



Southgate awavulia kofia wachezaji vijana UKURASA 29

MTU KATI...



Mshambuliaji wa Senegal, Bamba Dieng, akiwekwa mtu kati na mabeki wa England Harry Maguire (kulia) na John Stones katika harakati za kutaka kufunga kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia iliyopigwa Uwanja wa Al Bayt, Qatar juzi usiku. England ilishinda mabao 3-0 na kutinga robo fainali ambapo sasa itakutana na Ufaransa iliyoifunga Poland 3-1. **HABARI UK. 29**

# MAYELE AIRUDISHA YANGA SC SOKONI

**Na Saada Akida**

## ●●● Kocha asema straika huyo akikosekana uwanjani wanapata tabu sana, aitaja michuano CAF...

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema kwa sasa wanaangalia uwezekano wa kusajili mshambuliaji wa kati ambaye atakuja kuongeza nguvu kikosini na kuisaidia timu hiyo kwenye Ligi Kuu Bara na michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Ikicheza bila mshambuliaji wao namba moja na mbili, Fiston Mayele na Heritier Makambo, Yanga juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons kwa tabu, mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, bao pekee likifungwa na Feisal Salum 'Fei Toto' dakika ya 89.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema kukosekana kwa mshambuliaji alisema kutokuwapo kwa washambuliaji wao wawili, Mayele na Makambo, kulilazimu benchi la ufundi kusugua kichwa kubadili mbinu kwa kuwatumia baadhi ya wachezaji walikuwapo kwenye benchi.

Alisema walilazimika kumtumia Bernard Morrison, ambaye hakuwa fiti na kutakiwa kucheza dakika 15.

"Morrison hakuwa fiti kabisa na madaktari walimruhusu kucheza dakika 15 tu, tumelazimika kumtumia nyota huyo kwa sababu hatukuwa na washambuliaji ambao wangeweza kufanya mikimikiki eneo la wapinzani wetu," alisema Kaze.

Alisema mchezo ulikuwa mgumu kwa sababu wamekutana na timu ambayo inacheza kwa kuzuia sana hasa wanapokosa mpira na kushambulia wote wanapokuwa na mpira.

"Katika kipindi cha kwanza tulikuwa tunafika hadi mita 30 za mwisho, washambuliaji hawakuwa na maamuzi ya kufunga hasa kutokuwa na umakini.

"Kuna umuhimu wa kuwa na mshambuliaji ambaye amezoea mikimikiki ya mabeki wa aina ya Prisons ambao wanacheza kwa kuzuia zaidi," alisema Kaze.

Alisema wanakuwa na kazi kubwa wanapokutana na timu za aina ya Prisons kwa sababu uchezaji wa Yanga ni wakutumia zaidi ufundi.

"Niwapongeze wachezaji wamepambana kwa sababu kucheza na timu inayozuia ni ngumu sana, ufundi unatakiwa kuwa mkubwa, kipindi cha kwanza hatukucheza vizuri kulingana na wapinzani wetu walivyokuwa wakicheza," alisema Kaze.

Kocha Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shaban Mtupa, alisema walipoteza kwa sababu haikuwa bahati yao kutokana na kutengeneza nafasi nyingi na kushind-

INAENDELEA UK. 31

# Simba yataka 12 za kufunga mwaka

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata pointi tatu kwa ushindi wa mabao 3-0 juzi dhidi ya Coastal Union, Simba sasa hesabu zao ni kusaka pointi 12 katika michezo minne ya Ligi Kuu Tanzania Bara ndani ya mwezi huu.

Simba juzi walifanikiwa kuondoka na ushindi huo ugenini katika Uwanja wa Mkwakwani na tayari wamerejea jijini Dar es Salaam kujiandaa na mchezo wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) dhidi ya Eagle SC utakaopigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Katika michuano hiyo ya Kombe la FA, msimu uliopita Simba ilishindwa kutetea taji hilo baada ya kutolewa hatua ya nusu fainali mchezo uliopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Baada ya mchezo huo wa FA, Simba itaanza kupambani pointi 12 ndani ya mwezi huu kwenye Ligi Kuu mzunguko wa pili kwa kuifuata Geita Gold FC Desemba 18 na 21 watakuwa ugenini tena kwa 'Wakulima wa Miwa' wa Kagera Sugar kabla ya Desemba 26 kuvaana na KMC FC.

Mechi itakayofuata itakuwa dhidi ya Tanzania Prisons katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Desemba 30, ambayo itakuwa yakufungia mwaka 2022 na kupiga hesabu zao kama malengo yao ya kukusanya pointi 12 mwezi huu yametimia ama la.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema anaamini hakutakuwa na mchezo rahisi lakini anawaamini vijana wake wataendelea kupambana katika kila mechi kwa ajili ya kupata matokeo chanya.

Alisema kazi kubwa iliyoko ni kuendelea kufanyia kazi ma-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >